Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

### Kikao cha Nane - Tarehe 13 Novemba, 2003

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of The Presidential Parastatal Sector Reform Commission for the Year ended 30th June, 2002).*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Harbours Authority for the Year ended 30th June, 2002).*

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

### Kujenga Ukumbi wa Bunge - Zanzibar

**MHE. ALI SAID SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni Jamhuri ya Muungano wa Nchi mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar; na kwa kuwa tunao Ukumbi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Mjini Dodoma; je, kwa nini Serikali isifikirie kujenga Ukumbi wa Bunge huko Tanzania Zanzibar ili kwa nyakati mbalimbali Mikutano ya Bunge iweze kufanyika huko?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salum, Mbunge za Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Tanzania ni Jamhuri ya Muungano wa nchi mbili, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani na kwamba siku zote Shughuli za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hukutana Dodoma katika Ukumbi tuliopo sasa.

Aidha, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Ibara ya 20(1) Mikutano yote ya Bunge itafanyika katika Ukumbi wa Bunge Mjini Dodoma. Hata hivyo Ukumbi huu kwa sasa kama unavyouona ni mdogo na haukidhi mahitaji ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo, Serikali kupitia Ofisi ya Bunge inakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa Ukumbi mpya wa Bunge hapa Dodoma ambao utakidhi matakwa na mazingira muhimu ya Ukumbi wa Bunge kwa kipindi kirefu. Pamoja na jukumu hilo, Serikali inakarabati majengo ya Ofisi Ndogo zilizopo Jijini Dar es Salaam na kujenga Ofisi za Bunge Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa Taifa wa kuwa na Kumbi za Bunge zaidi ya mmoja haupo. Ingawa ni kweli kwamba baadhi ya nchi nyingi duniani huwa na jengo la pili la Bunge sehemu moja ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga Ukumbi mwingine wa Bunge Zanzibar, kutokana na sababu nilizozitoa lakini pia kwa kuwa Mikutano yote itaendelea kufanyika hapa Dodoma.

**MHE. ALI SAID SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ni kawaida ni utaratibu wa Mikutano ya Bunge hutangulia na vikao vya Kamati mbalimbali za Bunge; na kwa kuwa ziko hizo Kamati kwa mujibu wa uzoefu karibu vikao vyote vinafanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Je, ni sababu ipi ya msingi ambayo haipelekei baadhi ya vikao hivi kufanyika Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Hilo la kwanza?

La pili, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika muafaka kwa vikao hivi vya Kamati kufanyika Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vikao vyote vya Kamati hivi sasa kutokana na utaratibu huu mpya vinafanyika Dar es Salaam. Hapo nyuma vimekuwa vinafanyika hapa hapa Dodoma. Lakini kwa sababu ya utaratibu huu mpya wa Muundo wa Kamati za Kisekta zinazoendana na Wizara tumeamua kwa pamoja kufanyia Dar es Salaam ili kurahisisha mawasiliano kati ya Serikali na Wabunge. Kwa sababu Kamati za sasa zimezama zaidi na zina mahusiano ya karibu sana na Wizara. Wizara nyingi ziko Dar es Salaam. Tulifikiri ni busara kufanya kule Dar es Salaam ili Waheshimiwa Wabunge wapate faida maradufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili analozungumza linazungumzika. Sisi ndio tulioamua kufanyia vikao Dar es Salaam na sisi ndio tulioamua sasa hatua ya kwanza kujenga Ofisi ya Bunge Zanzibar. Tumalize huu mradi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar, wenye uwezo wa kuamua ni sisi lakini hata hivyo sababu ya msingi niliyoitoa mwanzo ni lazima izingatiwe. *(Makofi)*

Na. 101

**Wizara Kutumia Jengo la Chimwaga**

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA (K.N.Y. MHE. LEKULE M. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri Mkuu aliwahi kulieleza Bunge hili kwamba, baadhi ya Wizara zitahamia kwenye Jengo la Chimwaga baada ya Jengo hilo kukamilishwa:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, jengo hilo liko mbali na wananchi?

(b) Je, wananchi watafikaje kwenye Wizara hizo zilizo porini mbali na Mji Mkuu au Makazi ya watu?

(c) Je, Ofisi ya Waziri Mkuu kukaa mbali na wananchi si kuwatesa wananchi wanaohitaji huduma katika Ofisi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kwanza nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kutamka hapa Bungeni kwamba baadhi ya Wizara zitahamia katika Jengo la Chimwaga hapo litakapokamilika. Kauli hiyo ilitokana na upembuzi wa matumizi mbadala ya jengo hilo baada ya kubainika kwamba jengo hilo lisingeweza kufaa kwa matumizi ya Bunge lako Tukufu.

Hata hivyo, Serikali imechukua hatua za makusudi kabisa za kuboresha na kuendeleza huduma za kijamii katika maeneo ya Chimwaga. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na upimaji wa viwanja katika eneo hilo ili wananchi waweze kujenga na pia kupeleka huduma muhimu za msingi. Aidha, barabara ya kwenda Chimwaga imechongwa na inapitika majira yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Jengo la Chimwaga halipo mbali sana na wananchi ikizingatiwa kwamba huduma muhimu kama vile barabara, simu, maji na umeme vipo na viwanja vingi vimekwishapimwa kuelekea maeneo ya Chimwaga na wananchi wengi sana wameshaanza kuendeleza maeneo karibu na Chimwaga. Uendelezaji wa ujenzi wa viwanja hivi kutawafanya wananchi watumie huduma muhimu ambazo zimekwisha pelekwa Chimwaga. Umbali kutoka Mjini hadi Chimwaga ni kilomita 6 tu ambazo wananchi watakaojenga karibu na Jengo la Chimwaga na wale watakaohitaji kupata huduma kwenye Wizara zitakazotumia jengo hili watafika kwa urahisi kwa sababu barabara iendayo huko imeimarishwa na hivyo kuwezeshwa kuwepo kwa usafiri wa kuaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nilieleza Bunge lako Tukufu kwamba kuhamishia baadhi ya Wizara katika jengo la Chimwaga ni moja kati ya matumizi mbadala ya jengo hilo. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Bajeti iliyopita Ofisi ya Waziri Mkuu ulitenga shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya matayarisho ya kuhamia jengo hilo la Chimwaga. Nataka kuuliza, je, sasa kuna nini kinaendelea katika fedha hizo? *(Makofi/Kicheko)*

Pili, kwa kuwa katika miaka ya nyuma zilitengwa viwanja vingi sana Mabalozi na kadhalika na halijafanyiwa kazi. Je, utaratibu huu wa kutengatenga viwanja na kutumia fedha za umma na Wizara hazihamii si ubabaishaji tu. Ni lini tatizo hili la kudanganya wananchi litaisha? (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kipindi cha Bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga Bajeti iliyopitishwa na Bunge hili imetoa shilingi 500,000,000/= si

kwa ajili ya kuhamishia Wizara Chimwaga ila ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Chimwaga.

Pili, ni kweli kwamba Serikali tangu ilipoamua kuhamia Dodoma kazi nyingi za msingi zilifanywa kama sehemu ya maandalizi ya uhamiaji Dodoma. Imepima viwanja vya kutosha na hata hivyo vya Mabalozi kweli vilipimwa na vya kujenga wananchi vilipimwa. Ilikuwa ni muhimu kuanza na haya maandalizi ya miundombinu ili kurahisisha uhamiaji wa watu Dodoma. Viwanja hivi havikupimwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali tu.

Mji mzima unaona Dodoma nilishawahi kusema hapa Dodoma ni Mji ambao umepimwa na umejengwa kisasa kuliko miji mingi ya Tanzania kwa sababu ya maandalizi yake. Viwanja vingi vimepimwa, miundombinu imetengenezwa. Kama mmetembelea maeneo mbalimbali huko utakuta barabara mpaka za mitaani zimetiwa lami. Ni maandalizi mazuri ya kuhamia Dodoma.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Benedict Losurutia, hakuna ubabaishaji hapa. Serikali imedhamiria na hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi, tutakwenda hatua kwa hatua na lazima Serikali itahamia hapa Dodoma.

Pamoja na maandalizi hayo Serikali imeonelea pia kuimarisha huduma. Hivi sasa tunashuhudia huduma za maji zimefurika kuliko uwezo wa watu wa Dodoma. Hivi sasa tunapima viwanja vingine 300 Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi iweze kujenga nyumba za makazi ya watumishi wa Serikali ambao wanaotakiwa kuja hapa Dodoma.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Losurutia, nataka kukuhakikishia kwamba jambo hili linatekelezwa kwa mujibu na utaratibu uliopangwa na hakuna ubabaishaji wowote wala udanganyifu kwa wananchi.

Na. 102

**Marupurupu ya Wenyeviti wa Halmashauri za Maendeleo ya Wilaya**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya wana majukumu na wajibu unaolingana na Meya wa Jiji na Miji; na kwa kuwa kwa sehemu kubwa Wenyeviti hao wanayo maeneo makubwa na magumu zaidi kiutawala kuliko Majiji na Manispaa:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya marupurupu yanayolingana na yale ya Meya, kama vile gari kwa ajili ya kazi za kiofisi na kupeperusha bendera?

(b) Je, kwa nini mpaka sasa Serikali haitoi ruhusa kwa Wenyeviti wa Halmashauri husika inapokuwa na uwezo kifedha au inao wahisani ambao wangeweza kuwapatia magari?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa Waraka wenye Kumb. Na. *PMC/2/A.100/1/18* wa tarehe 30 Juni, 1997 wenye kuelezea stahili za Madiwani, Wenyeviti na Mameya wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Waraka huu uliwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu malipo ya posho kwa Madiwani, Wenyeviti na Mameya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafiri, Halmashauri zimeendelea kutoa magari kwa Wenyeviti na Mameya wa Halmashauri kwa ajili ya shughuli za Kikazi ikiwa ni pamoja na kuhudhuria Vikao na kuhamasisha na kukagua shughuli za maendeleo na si vinginevyo. Wenyeviti wa Halmashauri za Miji na Wilaya kama walivyo Mameya wa Manispaa na Majiji wanaruhusiwa kupeperusha bendera za Halmashauri zao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zote hupanga kutekeleza shughuli zake kulingana na vipaumbele vyake na hali ya kifedha. Kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), Halmashauri zina utaratibu wa kuhakikisha kwamba Wenyeviti wao wanakuwa na magari ambayo watayatumia kwa ajili ya shughuli za Kikazi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Halmashauri haina gari kwa ajili ya matumizi ya Mwenyekiti wa Halmashauri, ni jukumu la Halmashauri husika kupitia vikao halali kuamua juu ya suala hili. Hata hivyo maamuzi yatakayofikiwa ni lazima yazingatie vipaumbele vya Halmashauri.

Na. 103

**Barabara ya Heru Juu Hadi Katundu**

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE (k.n.y. MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Heru Juu - Muyama - Migongo - Kilelema - Mugera hadi Katundu hazijafanyiwa matengenezo mazuri kwa muda mrefu; na kwa kuwa barabara hiyo ina mashimo makubwa hasa kutoka Migingo hadi Kilelema na Migingo hadi Mugera mpaka Katundu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitengeneza barabara hizo ambazo ni kero kubwa kwa wananchi na zimekuwa hazipitiki hasa kwa nyakati za mvua?

(b) Kwa kuwa barabara hizo ni kiungo kikubwa kati ya Makao Makuu ya Wilaya ya Kasulu na Kata za Heru Juu, Munyegera, Nyanga, Kilelema na Kaja, Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza madaraja yanayounganisha Vijiji vya Mugera na Katundu?

(c) Ili kupunguza malalamiko yanayohusu ujenzi wa barabara za namna hiyo, na kwa kuwa barabara ni maendeleo, na kwa kuwa hivi sasa ziko fedha za kujenga barabara kila mwezi; je, Serikali haioni kwamba ingekuwa vizuri sana kama pangekuwepo na *A Comprehensive Road Construction Programme* kwa nchi nzima ambayo inakarabati barabara zote kwa awamu ili kuepuka kukaa muda mrefu bila kutengenezwa kwa barabara nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaelewa tatizo la barabara hizo na jinsi zilivyo na kero kubwa kwa wananchi na ndiyo maana barabara hizo ni moja kati ya zile zilizoingizwa kwenye Mpango wa *HIPC* wa matengenezo kwa mwaka wa fedha 2000/2001.

Hata hivyo, mpango huo hatukuweza kuutekeleza kwa kuwa fedha hazikutolewa. Vile vile barabara ya Heru Juu hadi Kitanga (km 68) ilifanyiwa tathmini ya matengenezo na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ili iweze kujumuishwa kwa pamoja na barabara za mpakani. Tathmini ilionyesha kuwa jumla ya shilingi 861,925,000/= zilihitajika kwa wakati huo kutengeneza barabara hizo.

Pamoja na jitihada zote nilizozitaja zikiwa zinaendelea, Halmashauri ya Kasulu imepanga kuikarabati barabara hiyo kwenye mpango wake wa matengenezo kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Maandalizi ya awali yamefanyika na gharama kamili za matengenezo zitajulikana wakati wa Bajeti ya mwaka ujao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa matengenezo ya madaraja yanayounganisha Vijiji vya Mugera na Katundu ni kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwenye barabara ya Mugera - Katundu, kutajengwa darala la zege kwenye Mto Mlangizi ambalo litagharimu kiasi cha shilingi 9,500,000/=. Vile vile kutajengwa madaraja mawili yenye thamani ya shilingi 16,060,000/= kijijini Kajana kwenye barabara ya Mugama - Kajana.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchagua barabara za kutengeneza, kuna mambo mengi yanayoangaliwa kabla ya kutoa kipaumbele cha kutengeneza barabara

fulani. Mambo hayo ni kama umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi, *Class* ya barabara hiyo (Barabara Kuu, za Mikoa au Wilaya), wingi wa magari yanayopita kwenye barabara hizo na kadhalika.

Kwa mantiki hiyo, Serikali ina *Comprehensive Road Construction Programme* ya fedha zake inazozitenga kila mwezi na ndiyo maana kipaumbele chake cha kwanza ni kuweka lami barabara zote zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania Bara na baada ya hapo zitafuata barabara nyingine muhimu zaidi.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ambazo zinazungumziwa ni barabara ambazo kiuchumi inaweza kuonekana zisiwe na umuhimu sana. Lakini sababu ni barabara ambazo ziko mpakani na nchi ya Burundi ambapo kuna matatizo ya vita na nchi ya Tanzania. Kwa nini Serikali isitoe kipaumbele kutengeneza barabara hii kwa maana ya barabara za usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kwa kuwa asilimia 70 kwa Wilaya ya Kibondo imetengwa kwa ajili ya hifadhi; na kwa kuwa barabara zilizoko hivi sasa nyingi zinatengenezwa na Halmashauri. Kwa nini basi ili kufidia na Serikali ikawa na eneo kubwa la kutengeneza kwa nini barabara zote za Mpakani zisiingizwe katika barabara ambazo zinatengenezwa na Serikali Kuu badala ya Halmashauri ambayo haina pesa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Wilaya hizi zinazozungumzwa ni barabara za Mpakani. Sasa hivi tunao mkakati wa kuangalia jinsi gani Serikali itashughulikia barabara hizi za Mpakani. Naomba Mheshimiwa Mbunge asubiri ataona matokeo yake tutaleta taarifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri. Kwa manufaa ya *Hansard,* napenda kutoa maelezo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni Serikali ambayo inaishi kwa amani, utulivu na upendo na majirani zake. Tanzania haijavamia nchi yoyote isipokuwa ilipovamiwa ilionyesha uwezo wake mkubwa sana. Kwa hiyo basi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania haina vita na Serikali ya Burundi. Tatizo la Burundi ni tatizo lao wamalize tatizo hilo na wakijaribu kuleta matatizo hayo ndani ya nchi yetu tutalinda mipaka yetu. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 104

**Sheria ya Usalama Barabarani**

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Usalama Barabarani ina mnyima haki mwenye gari ambaye amegongwa na gari lingine lakini siyo kwa makosa ya aliyegongwa; na kwa kuwa dreva mwenye makosa akifikishwa Mahakamani, sheria inampa adhabu ya tozo linaloanzia shilingi 10,000/= na kuendelea:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, mwenye gari lililoharibiwa kwa makosa ya mtu mwingine anapata gharama za matengenezo ambayo wakati mwingine huwa kubwa sana?

(b) Je, Serikali haioni kwamba sheria hiyo inawakandamiza wenye magari wasio na hatia?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba hali hiyo inachochea ajali nyingi za barabarani, kwa vile madereva wasiojali huwa wanafanya makosa ya wazi, kukiri kosa haraka na kuishia kulipa faini ya shilingi 10,000/= tu.?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mwenye gari lililoharibiwa kwa makosa ya mtu mwingine anapata gharama za matengenezo ambayo wakati mwingine huwa kubwa sana. Kutokana na hali hiyo ndiyo maana Serikali ikatunga Sheria ya Bima za Magari *(Motor Vehicle Insurance Act; Cap 169)* ili gharama hizo ziweze kugharamiwa na Bima.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973 ilitoa adhabu ya kati ya shilingi 10,000/= na shilingi 30,000/= kwa mtu aliyesababisha ajali. Sheria hiyo ilirekebishwa na Sheria Na. 16 ya mwaka 1996 ambapo sasa adhabu imeongezwa na kuwa kati ya shs.15,000/= na shs.50,000/=. Sheria hii hailengi kuwakandamiza wenye magari waliosababisha ajali na mtu mwingine. Lengo la Sheria hiyo ni kuwadhibiti na kuwaadhibu madereva wanaosababisha ajali. Wenye magari yaliyosababishiwa ajali wanalindwa na sheria ya kupewa haki ya kulipwa fidia na Bima ya gari lililosababisha ajali.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa adhabu inayotolewa kwa madereva wanaosababisha ajali za barabarani ndogo. Ni kutokana na ukweli huo Serikali hivi sasa inaangalia uwezekano wa kuongeza viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba kuna fidia ya Bima lakini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Bima haitoi tu malipo mpaka pale inaporidhika kuwa aliyegonga ndiyo ana makosa na yeye vile vile ana Bima; na kwa kuwa wapo wachache ambao hawana Bima, kwa hiyo, mwenye gari anapata hasira.

Pili, kwa vile adhabu zimeongezwa kutoka shilingi 15,000/= mpaka shilingi 50,000/= anakubaliana na mimi kwamba kwa kuwa gharama zimepanda sana hata hizo shilingi 50,000/= sasa hivi hazifai chochote na kwamba lini ataleta mapendekezo hapa Bungeni ili kuweza kuibadili sheria hiyo iende na wakati? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba fidia haitolewi mpaka kuwepo na uthibitisho na kwamba yule aliyegongwa kama hakuwa na makosa basi yule aliyemgonga anatakiwa Bima yake itengeneze gari la huyu aliyegongwa. Kama aliyegongwa ndiyo mwenye makosa naye vile vile ana Bima, Sheria ya Bima inataka kila mwenye gari lazima awe na Bima. Kwa hiyo, hata huyu aliyegongwa kama yeye ndiyo mwenye ana makosa bado ana Bima yake ambayo inalinda gari lake.

Kuhusu faini ya shilingi 50,000/= kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba ni kweli shilingi 50,000/= ni adhabu ndogo sana na hivi sasa Serikali inatazama namna ya kuongeza adhabu hizi. Sasa Mheshimiwa Mbunge atasema lini anataka nitaje tarehe. Sina tarehe sasa hivi lakini nataka nimwambie kwamba mapema kadri itakavyowekana.

Na. 105

**Vitambulisho vya uraia**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza: -

Kwa kuwa uraia wa Watanzania walio wengi ni wa kuzaliwa na sio wa kuandikishwa na kwa kuwa kutokuwepo kwa daftari rasmi la uraia wa Tanzania na ukosefu wa vitambulisho vya uraia kumelalamikiwa na Wabunge wengi kwa miaka mingi sasa: -

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kipindi kirefu imekuwa ikitoa mwanya kwa raia wa nchi nyingine na hasa wahalifu kujipenyeza kwa urahisi na kujipatia urahisi na kujipatia uraia wa nchi yetu bila jasho lolote na kusababisha hasara kwa nchi?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, ukosefu wa vitambulisho kwa Watanzania wote ni tatizo kubwa kwani hata ilipotokea ajali ya treni Dodoma tulizika watu wengine ambao hawakuwa raia wa Tanzania bali kutoka Kongo, Burundi, Rwanda na kadhalika kulikotokana na mapungufu hayo?

(c) Kutokana na sababu kwenye sehemu (a) na (b) ya swali hili, je, Serikali itakuwa tayari kutengeneza daftari la raia wake na kuanza kutoa vitambulisho mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kukosekana kwa vitambulisho vya Kitaifa kunasababisha uwepo ugumu wa kutambua nani ni raia wa Tanzania na nani sio raia; hivyo kuweka mwanya kwa baadhi ya wageni waweze kujipenyeza na kujipatia haki wasizostahili kikatiba na wengine hata kufanya vitendo vya uhalifu.

Katika kubabiliana na hali hii, Serikali kwa kutumia Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 imekuwa inaendesha misako ya mara kwa mara na kuwabaini wageni haramu. Kwa mfano, kipindi cha Januari hadi Desemba, 2002 jumla ya wageni haramu 1,768 walinaswa na kuchukulia hatua za kisheria. Vile vile, kipindi cha Januari hadi Agosti 2003 jumla ya wageni haramu 2,663 walinaswa katika misako hiyo na kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa upo umuhimu kwa Serikali kutoa vitambulisho vya Kitaifa mapema iwezekanavyo. Hata hivyo kama ambavyo tulikwishaeleza huko nyuma, tatizo linalochelewesha kazi hii ni ukosefu wa fedha. Kazi hii inahitaji gharama kubwa sana. Sio chini ya shilingi bilioni 100. Fedha za kugharamia mradi huu zinatafutwa humu nchini na kwa kushirikisha nchi wahisani. Mara zitakapopatikana kazi hii itaanza.

Aidha, wakati tunasubiri fedha kwa ajili ya mradi huu, kazi imeanza ya kuwaorodhesha wageni wote kutoka nchi za nje katika daftari maalum, kazi hii imeanza Mikoa ya Mipakani.

Mheshimiwa Spika, zoezi la uandikishaji wageni likikamilika, linatarajia kurahisisha pia utoaji wa vitambulisho vya Kitaifa mradi huo utakapoanza.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi kwa majibu aliyoyatoa.

(a) Serikali imekiri kwamba kweli kuna matatizo kutokana na kutokuwa na vitambulisho, lakini mimi nasema wakati mwingine Serikali inafanya kazi bila kuwa na *coordination.* Mwaka jana tulikuwa na sensa na sensa ilikwenda karibu kila pembe ya Tanzania na tungeweza kuitumia sensa hiyo ili kuweza kupata daftari la Wananchi wa Tanzania na tukawa tumeishatengeneza vitambulisho. Ni kwa nini Serikali haikutumia

nafasi ya sensa ili kuweza kupunguza gharama za kutoa vitambulisho kwa Watanzania? *(Makofi)*

(b) Inaeleweka kwamba Serikali imekuwa na kigugumizi kuhusu suala hili, si suala tu la fedha kwa sababu yupo mtu au ipo Kampuni ambayo ilikuwa imepewa kazi hii ya kutengeneza vitambulisho, lakini mambo yanavyokwenda hayaeleweki, mara kesi iko mahakamani, huyo kashinda, je, Serikali inatoa tamko gani? Tunataka vitambulisho ili watu wa nje wasiwe wanakuja kutupigia kura hasa wengine wa huko mipakani. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba tungeunganisha zoezi la sensa na zoezi la kutoa vitambulisho, hayo ni mazoezi mawili tofauti. Sensa unahesabu kila mtu, Mtanzania, mgeni, nani, yeyote yule ambaye alilala Tanzania katika wiki ile, wote wanahesabiwa na vitambulisho vinalenga Mtanzania tu. Kwa hiyo, haingekuwa rahisi kuunganisha mazoezi haya, isipokuwa zile takwimu za sensa zinatusaidia katika kuandaa hili zoezi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba Serikali ina kigugumizi katika suala hili, Serikali haina kigugumizi. Kama ambavyo tumekuwa tunaarifu Bunge hili mara kwa mara, ni kweli tuliwahi kutangaza tenda katika kazi hii, ni kweli kuna Kampuni *RSL* ilishinda *tender hii*, baada ya kushinda *tender* wakaingiza mambo ambayo hayakuwemo kwenye *tender.*

Kwa hiyo, kukawa na mgogoro ambapo baadaye tulifika mahakamani, tumekuwa mahakamani karibu miaka miwili, baada ya kutoka mahakamani, mahakama ikasema nendeni mkazungumze na kama mazungumzo yakishindikana huyu bwana ndipo anyang'anywe hiyo *tender.* Tumezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu, Waziri alitangazia Bunge hili kwamba, mazungumzo na huyu bwana yameshindikana na hivyo tumeishaachana naye. Baada ya kuachana naye, sasa tumeanza upya zoezi hili na tunataka tulianze vizuri zaidi. Sasa hivi inatangazwa *tender* ya Kampuni ambayo itafanya kwanza upembuzi yakinifu *(feasibility study).* Wakati *feasibility study* inafanyika kazi ile ya kuorodhesha wageni katika Mikoa yote nayo itakuwa inafanyika, kwa sababu leo hii tukipata vitambulisho tukaenda pale Kigoma tukaanza kuvigawa tunaweza kukuta asilimia 30 tumegawia wageni, ndiyo maana hili zoezi kwanza la kuwabaini wageni ni muhimu sana tulifanye kabla ya kuanza kutoa vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jumla nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, nia ya Serikali kutoa vitambulisho iko pale pale na kwamba fedha zikipatikana tutaanza mara moja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na swali zuri alilouliza Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, linalohusu haya mambo ya uraia na kutokana na majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri na amegusia Mkoa wa Kigoma, kwamba unaonekana kuwa ndiyo wenye tatizo la wageni na hata sasa hivi kuna watu ambao wamewekwa ndani ambao ninawajua kwamba ni raia, wako kule mahabusu na ambao ninajua kuwa ni wapigakura wa muda mrefu tu tena hata kabla ya uhuru. Kama utaratibu huu wa kuwapatia vitambulisho ambavyo vinatafutwa kwa muda mrefu, vinaendelea kusuasua pasipo kueleweka: -

(a) Je, Waziri haoni kwamba hili tatizo ni sugu kulinganisha na Mikoa mingine kwani Mmakonde na Mngoni wao wanahesabika kama bado ni raia, lakini walivuka Mto Zambezi?

(b) Je, Waziri haoni kama huo ni uonevu unaofanyika katika Mkoa wa Kigoma? Naomba hao walioko ndani watoke mara moja. Hapo sasa! *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika jibu langu la msingi nimetoa mfano wa Mkoa wa Kigoma kwa sababu ya ukweli tu kwamba, ni moja ya Mikoa ambayo tunayo matatizo. Pia, ni kweli kwamba tukipata Vitambulisho vya Kitaifa kuwatambua kwa haraka zaidi Watanzania inakuwa ni jambo jepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunachofanya katika Mikoa hiyo yenye matatizo ni kutumia Sheria ya Uraia, mtu ambaye si raia anakamatwa pamoja na hao ambao wako mahabusu watachekechwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao watathibitika kwamba ni Watanzania na uthibitisho upo wa kutosha na ukoo wake uko katika Kijiji au Kitongoji fulani watachekechwa. Wale ambao wako katika mchekecho huo na wakaonekana kwamba ni Watanzania wataachiwa na wale ambao katika mchekecho huo watajulikana kwamba si Watanzania watarudishwa kwao kwa sababu wana kwao.

Na. 106

**Tatizo la Dawa na Mbolea Zilizokwisha Muda Wake**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza: -

Kwa kuwa tatizo la kuwepo kwa dawa za kuulia wadudu na mbolea zilizokwisha muda wake wa kutumika ambazo zimehifadhiwa katika maghala ni kubwa na Serikali katika Mkutano wa Bunge wa Kumi ilieleza wazi kuwa kwa sasa inatafuta njia salama ya kuziteketeza: -

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya dawa/mbolea za namna hiyo ambazo zinatakiwa ziwe zimeteketezwa, lakini bado zimo mikononi mwa wakulima?

(b) Kwa kuwa maelezo juu ya muda wa matumizi ya dawa zilizo nyingi kati ya hizo zilizokwisha muda wake wa matumizi yameandikwa kwa lugha za kigeni ambazo hazieleweki kwa baadhi ya watumiaji na hivyo kusababisha matumizi yasiyo salama. Je, Serikali inawasaidiaje wakulima na walaji wasiozielewa lugha hizo kwa lengo la kuwanusuru na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Kati ya mwaka 1998 na 2000 Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi ilifanya uchunguzi wa kina ili kujua kiasi cha madawa ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao na magonjwa ya mifugo yaliyokwisha muda wake wa kutumika yaliyoko nchini kwa madhumuni ya kutafuta njia salama ya kuyateketeza.

Uchunguzi huo ulibaini kuwa kuna kiasi cha tani 1,200 za madawa ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao na tani zipatazo 200 za madawa za kudhibiti magonjwa ya mifugo yaliyokwisha muda wake au yanakatazwa kutumika kutokana na madhara yake kwa mazingira. Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* limeandaa program ya kuteketeza madawa hayo yaliyokwisha muda wake wa kutumika au yanayokatazwa.

Programu hiyo inajulikana kama *African Stockpiles Program.* Katika awamu ya awali kati ya tarehe 6 na 16 Oktoba, 2003, programu hiyo ilitoa mafunzo kwa wataalam 50 watakaohusika na ukusanyaji na usafirishaji wa madawa hayo. Kazi ya kuteketeza madawa hayo zinatarajiwa kuanza katikati ya mwezi Mei 2004 na zinatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi minne. *African Stockpiles Program* imetenga Dola za Marekani 500,000 kugharamia maandalizi ya mpango wa kuteketeza madawa hayo katika nchi 15. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango huo itahusisha nchi za Tanzania, Ethiopia, Mali, Senegal na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Kwa sasa hatuna taarifa za madawa yaliyokwisha muda wake wa kutumika ambayo yako mikononi mwa wakulima. Hii inatokana na ukweli kwamba wakulima hununua kiasi kidogo cha madawa kukidhi mahitaji yao.

(b) Kutokana na kifungu Na. 20 cha Sheria ya Kudhibiti Visumbufu vya Mimea Na. 13 ya mwaka 1997 *(The Plant Protection Act, 1997)* maelezo kuhusu aina ya dawa, matumizi yake na tahadhari za kuchukuliwa wakati wa kuzinunua ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kwa Kiingereza ili kuwawezesha watumiaji wengi kusoma na kuelewa matumizi sahihi ya dawa husika.

Kwa hiyo, mtu au mfanyabiashara yeyote anayeuza viatilifu ambavyo havina maelezo kwa lugha hizo mbili anavunja sheria. Watumiaji wa viatilifu watoe taarifa kwa wakaguzi wa madawa walio chini ya Halmashauri za Wilaya na Miji mara wanapoona

dawa hizo zenye maelezo ya matumizi yaliyoandikwa kwa lugha isiyoeleweka ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika swali langu la msingi niliomba kupewa taarifa kuhusu dawa na mbolea ambazo zimepita muda wake wa kutumika, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamejikita katika suala zima la madawa tu na siyo mbolea. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari pia kutoa taarifa ya mbolea zilizopitwa muda wake wa kutumika ambazo bado ziko katika maeneo tofauti? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa njia nyingine rahisi kabisa ya kuhakikisha kuwa tatizo hilo la mlundikano wa dawa zilizokwisha muda wake ama mbolea linatatuliwa ni kuwa na utaratibu mzuri wa kufikisha pembejeo kwa wakulima kwa muda unaotakiwa na kwa hitaji muafaka linalohitajika. Je, Mheshimiwa Waziri ananiambia nini kuhusu tamko la Serikali la kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa Mikoa ya Kusini kama njia nyingine mojawapo itakayosaidia kutatua tatizo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyosema, wakulima wengi hununua mbolea kwa kiasi kidogo. Kwa hiyo, walio na mbolea ya ziada ni wafanyabiashara ambao taarifa zao hatunazo. Hiyo nimeeleza dhahiri katika jibu langu la msingi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa zilizopitwa na wakati wa matumizi au mahitaji ya mbolea anayohitaji Mheshimiwa Mbunge, tamko la Serikali litatolewa leo rasmi baada ya kipindi cha maswali. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa kuna dawa ambazo ziliwahi kutolewa na zikaharibu mimea, kwa mfano dawa zilizotolewa kwenye kahawa *(red copper)* ikaharibu na kuwapa wananchi hasara. Je, Serikali ina mpango gani wa kufidia watu waliopata hasara kwa kuwa ni Serikali yenyewe ndiyo iliyotoa dawa hizo? Naomba Serikali inieleze.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili swali alilouliza Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, halijibiki kwa sababu hatuambii ni wapi wala lini? Nashukuru. *(Kicheko)*

Na. 107

**Kilimo cha Umwagiliaji kwa Kutumia Maji ya Kuvuna**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza: -

Kwa kuwa suala la kutimiza lengo la Kitaifa kuwa Sekta ya Kilimo itoe mchango mkubwa katika kufanikisha mageuzi katika uchumi wa Taifa kuwa imara na wa kisasa ifikapo mwaka 2025: -

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha programu na miradi ya kuvuna maji ya mvua kwa kuchimba mabwawa madogo madogo na miundombinu itakayowezesha maji yafikishwe mashambani kwa matumizi ya kilimo cha kumwagilia maji hususan kwenye Wilaya za Ukame kama Mikoa ya Singida na Dodoma?

(b) Je, Serikali inaweza kulitaarifu Bunge hili kuwa, kwa kipindi cha 1995 - 2001 ni mabwawa mangapi yamekwisha kamilishwa pamoja na miundombunu ya kufikisha maji mashambani kwa kilimo cha kumwagilia?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha Tume ya Taifa ya Kuvuna Maji ya Mvua kwa Kilimo cha Umwagiliaji *(National Rain Water Harvest and Irrigation Commission)* ambayo itapewa jukumu la kupanga na kuratibu kikamilifu mikakati muhimu *(Irrigation Strategic Planning)?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Kwa miaka mingi Serikali imekuwa ikitilia mkazo uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo kwa ajili ya kumwagilia mashamba. Yapo makubwa mengi ya ukubwa mbalimbali yaliyojengwa miaka iliyopita na ambayo yanaendelea kutumika hadi sasa. Mabwawa hayo ni pamoja na yale ya Hombolo, Chikopelo na Buigiri katika Wilaya ya Dodoma Vijijini, Chibumagwa katika Wilaya ya Manyoni, Nang'onyi katika Wilaya ya Singida Vijijini, Mwaisenge, Kisese na Mrijochini katika Wilaya ya Kondoa na kadhalika.

(b) (i) Kati ya mwaka 1994 na 1997, Serikali kwa kutumia mkopo wa *IFAD,* ilitekeleza Mradi wa Kuendeleza Wakulima wa Wadogo Wadogo katika maeneo ya ukame *(Smallholder Development Project for Marginal Areas).* Chini ya mradi huo Serikali ilijenga vibanio katika skimu 18 katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Kati ya skimu hizo tano ziko Mkoa wa Singida na nne ziko katika Mkoa wa Dodoma.

(ii) Kati ya mwaka wa 1996 na 2002 Serikali ilitekeleza *Mara Farmer's Initiative Project (MARAFIP)* kwa mkopo wa *IFAD.* Chini ya mradi huo mabwawa madogo sita yalijengwa mawili mawili katika Wilaya za Bunda, Musoma Vijijini na Tarime.

(iii) Kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza wakulima wadogo wadogo kati ya mwaka wa 1990 na 1997, *IFAD* ilikubali kuipa Serikali mkopo kwa ajili ya kugharamaia Program Husishi Jamii ya

Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme).* Utekelezaji wa Programu hiyo ulianza mwaka wa 2000 na unatarajiwa kumalizika mwaka wa 2006. Chini ya programu hiyo, ambayo itahusisha Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Manyara, mabwawa madogo manane yatajengwa na ujenzi wa mabwawa matatu kati ya hayo umeshaanza na vibanio 22 vitajengwa na 14 vimeshaanza kujenga.

Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kujenga na kukarabati mabwawa kumi na moja katika Mikoa ya Dodoma (moja), Tabora (mawili), Mara (manne), Tanga (moja) na mabwawa mawili yatajengwa kwenye Vijiji vya Tyme - Masage na Kironda - Datali, Wilayani Iramba.

(c) Kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha Tume ya Taifa ya Kuvuna Maji ya Mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji peke yake. Uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji maji mashambani ni sehemu ndogo tu ya utaratibu wa umwagiliaji maji mashambani.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa janga la njaa ambalo limeikumba Taifa letu limesababishwa na upungufu wa mvua mwaka huu na pia na sera isiyozingatia kutotekeleza kilimo cha kisasa. Je, Serikali imejifunza nini kutokana na tukio hilo la njaa na sasa ina mikakati gani na tahadhari gani pamoja na kuelekeza nguvu zake zote katika kuwawezesha wakulima wa nchi hii kuendesha kilimo cha kisasa kwa kuwajengea miundombinu ya kuvuna maji ya mvua? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa zoezi linaloendelea sasa la kuomba omba misaada ya chakula cha njaa ambayo imelikumba Taifa hili inaonekana kama ni sera ya kudumu na ni sera mbadala kwa kilimo cha kisasa cha umwagiliaji. Je, Serikali haioni kuwa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la njaa ni kuliingiza Taifa katika kilimo cha kisasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, janga ni janga, hata ungejiandaa vipi janga likitokea limetokea. Sisi Kiserikali bila janga tulijiandaa vilivyo kwa kuandaa Mpango kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani ambao tuliupata kutoka Mikoani na tumeuunganisha, kuna buku nene hivi na nikianza kulisoma hapa nitapoteza wakati wa Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aridhike kuwa tuna mkakati wa kutekeleza mpango wa umwagiliaji maji ambao utahusisha Mikoa yote na Wilaya zote kulingana na ule mpango kabambe ulioandaliwa na Serikali.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mpango kabambe wa umwagiliaji katika nchi hii na kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa familia moja moja ndiyo inaunga Jamhuri hii kwa sababu familia moja ndiyo raia wa Tanzania.

(a) Je, Serikali haioni kwamba mpango wa uvunaji maji kwa familia moja moja unaweza kusaidia katika kuvuna maji na kumwagilia kwa familia moja?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za kuchimba visima virefu ili familia moja moja iweze kupata maji na kumwagilia na kuweza kupata mavuno ya kutosheleza familia moja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunapenda kusisitiza uvunaji wa maji kwa kila familia, lakini hata hivyo Kitaifa tumeagiza tutumie mabonde yaliyopo sasa hivi katika kulima mazao ambayo yanaweza kuiva katika muda mfupi na hasa maeneo kama Kagera anakotoka Mheshimiwa Mbunge, kuna mito mingi kweli na mabonde mengi sana. Tuondoke majumbani twende mabondeni tukalime na hiyo ndiyo njia pekee ya kupambana na njaa vilivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 108

**Misamaha ya Ushuru wa Migodi**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo kwa ukwepaji mkubwa wa ushuru (unaofikia shilingi bilioni 50 kwa mwaka) kutokana na misamaha ya kodi kwa migodi hewa inayoshamiri nchini na kwa kuwa ili ukwepaji huo ufanyike na kufanikiwa lazima wahusike *TRA,* wenye migodi pamoja na wenye vituo vya mafuta: -

(a) Je, ni Kampuni ngapi zimepewa misamaha hiyo ya kodi na ni kiasi gani cha mafuta kilichukuliwa kwa kipindi cha 2001 hadi sasa? (Idadi kwa kila Kampuni/mgodi)

(b) Je, Serikali kuanzia Julai 2002 hadi sasa imefanya marejesho kiasi gani *(amount)* kwa kila mgodi?

(c) Je, Serikali baada ya kugundua wizi, ubadhirifu na ufisadi huo mkubwa imechukua hatua gani kwa Wafanyakazi wa *TRA,* wamiliki wenye migodi iliyohusika na ufisadi huo na Kampuni za mafuta zilizohusika na ufisadi huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Wankanga Marwa; Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu imeshuhudia ukwepaji mkubwa wa kodi na ushuru katika Sekta ya Mafuta ya Petroli katika siku za hivi karibuni. Hali hii inathibitishwa na takwimu za matumizi ya mafuta nchini katika miaka ya hivi karibuni ikilinganishwa na hali ya ukuaji wa uchumi. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imefanikiwa kugundua ukwepaji kwa wafanyabiashara katika Sekta hii. Hata hivyo, kiasi halisi cha hasara iliyotokana na ukwepaji huo hakijulikani na hivyo yaliyopo ni makadirio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini ni mtumiaji mkubwa wa mafuta ya petroli, dizeli na mengineyo hasa kwa ajili ya kuzalisha umeme katika migodi ambayo haijaunganishwa katika gridi ya Taifa na kwa ajili ya kusafirisha udongo wenye madini hadi kwenye mitambo ya usafishaji. Mafuta yanayotumika katika migodi ya madini yamesamehewa ushuru kwa mujibu wa sheria na hivyo si sahihi kusema kodi hiyo haikusanywi kutokana na ukwepaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

(a) Kulingana na takwimu zilizopo, kati ya Januari 2001 na Juni 2003 kulikuwa na Makampuni 35 yaliyokuwa yanajishughulisha na uchimbaji wa madini nchini na kiasi cha lita 206,965,011 za mafuta zilisamehewa ushuru kwa kipindi hicho.

(b) Kwa kipindi cha Julai 2002 hadi sasa, Serikali imefanya marejesho ya ushuru wa kiasi cha shilingi 11,953,120,267/=.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ukwepaji mkubwa wa kodi kwenye mafuta umebainika katika misamaha ya kodi ambapo watumiaji walikiuka taratibu za misamaha kwa kuingiza mafuta ya misamaha kwenye soko la ndani. Aidha, *TRA* imechukua hatua mbalimbali kila ilipogundua ukwepaji. Hatua hizo ni pamoja na kufunga vituo vya mafuta vilivyothibitishwa kuuza mafuta yasiyolipiwa kodi, kutaifisha magari yaliyobeba mafuta ya magendo pamoja na hatua nyingine za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kugundua ukwepaji wa kodi kwenye mafuta ya petroli, Serikali imechukua hatua kadhaa za kiutawala kuanzia mwezi Julai mwaka huu wa 2003 na hatua hizo zilitangazwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha ya Bajeti ya mwaka 2003/2004. Hatua hizi zimeziba mianya ya ukwepaji kwa kiasi kwamba makusanyo ya kodi kutokana na mafuta ya petroli yameongezeka kwa Shilingi bilioni 6 kwa mwezi kuanzia Julai 2003. Nia ya Serikali ni kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi.

Kwa upande wake, *TRA* imeendelea na utaratibu wake wa kubadilisha mara kwa mara watumishi wanaoshughulikia bidhaa za mafuta, ili kupunguza uwezekano wa kuzoeana na wakwepa kodi. Pia, *TRA* iko makini sana kutovumilia wafanyakazi wake kujihusisha na vitendo vya rushwa. Hatua kali huchukuliwa mara moja hali hii ikigundulika.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa sababu wapo wamiliki wa migodi ambao wanapata mgao wa mafuta zaidi ya mahitaji yao na kiasi kile cha ziada huyauza kwenye soko na hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Je, Waziri anaweza kuniambia sasa kwamba ataifanyia kazi taarifa aliyopewa ya kuhusu ukwepaji huo ambao unamhusisha mmiliki mmoja wa mgodi ambao mgao wake mkubwa anaopata baadhi ya mafuta yale anauza kwa watu wenye vituo vya mafuta Jijini Dar es Salaam? *(Makofi)*

(b) Kwa sababu sasa biashara hii ya ukwepaji wa ushuru wa mafuta imeshamiri sana kwenye maeneo mengi ya nchi yetu hasa maeneo ya ziwa na kadhalika. Je, Waziri anaweza kunithibitishia kwamba sasa Serikali inachukua hatua kuhakikisha kwamba ile *fuel delivery* inafanywa kwa mita kwenye maeneo yote ambako mafuta yanashushwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa anayosema Mheshimiwa Mbunge kwamba nimepewa, ni tatizo ambalo lilijitokeza ambapo mafuta yalikamatwa na hayakuwa yamelipiwa kodi na *TRA* na Wizara ya Fedha tulifuatilia suala hili na *TRA* walikwenda mpaka kwa mmiliki wa mgodi huo na ikafanya *audit on the ground* na kugundua upungufu.

Lakini ilituthibitishe kwamba mwenye mgodi huo tayari alikuwa na ushahidi wa kuuza dhahabu nje na alikuwa na ushahidi mwingine. Lakini ripoti ya *auditor* ipo *TRA* na kama Mheshimiwa Mbunge atahitaji ipo. *TRA* ilichukua hatua ya kufuatilia kwa makini na waliohusika na kununua mafuta hayo walifungiwa kituo na magari yalitaifishwa, lakini baada ya kulipa kodi pamoja na adhabu magari yake yalirudishwa na kituo chake kilifunguliwa.

Kwa hiyo, Serikali iko makini na inafuatilia kwa karibu sana. Napenda nitumie nafasi hii kuwaonya wafanyabiashara pamoja na wenye migodi ambao wanatumia fursa iliyotolewa na Serikali kwa kusamehe kodi kwa migodi kutumia mwanya huo kupeleka mafuta ambayo yamesamehewa kodi kwenye soko la ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Serikali imechukua hatua mbalimbali kubana mianya ya ukwepaji wa kodi kama nilivyoeleza. Hatua hizo ni pamoja na kufunga *flow meters* bandari ambazo zitafungwa hivi karibuni. *Flow meter* itafungwa bandarini kuona ni kiasi gani cha mafuta yanayoingia nchini na pia tumeweka utaratibu maalum wa uingizaji wa mafuta unaosimamiwa na mamlaka ya mapato kwenye mipaka ya Kenya na Tanzania. Pia bidhaa za mafuta zinazoingizwa kwa ajili ya nchi zingine transit zitasafirishwa hadi kwenye maghala ya mafuta yaliyopo mpakani, kodi zote za mafuta hayo zitalipwa wakati wa uingizwaji na mwagizaji atarejeshewa kodi hizo baada ya

kuthibitisha kwamba mafuta hayo yamesafirishwa nchi za nje. Kama mafuta hayo hayatasafirishwa ndani ya siku 15 kodi zote zitapaswa kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba *TRA* inabaina matatizo ya ukwepaji kodi, lakini kila inapobaini inaziba mianya kuhakikisha kwamba ukwepaji huo hauendelei. Kama nilivyosema zoezi hili limeokoa shilingi bilioni 6 kila mwezi zimeongezeka kwenye kodi zinazolipwa na mafuta. Hiyo ni ishara kwamba mianya inazidi kuzibwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi nzuri za dhati za Serikali mpaka hivi sasa vituo vya mafuta vya Dar es Salaam, bei yake ni ghali lakini jinsi unavyokwenda *up country* bei inapungua. Je, hizi ni sababu gani zinazosababisha hiyo na hasa vituo vingine inafika mpaka shilingi 600? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (DR. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu biashara ya mafuta ya *petrol* na dizeli imekuwa huria kwa hiyo, mwingizaji wa mafuta hatujui ameyapata kule kwa bei gani japokuwa kodi zetu zinakadiriwa kulingana na *International price* iliyoko kwa wakati ule lakini yeye ameyapata kwa bei gani au ana kisima chake akiuza kwa bei ya chini sisi hatufuatilii. Lakini kama nilivyosema huko nyuma kulikuwa na ukwepaji mkubwa wa kodi ndiyo maana mafuta yale yalikuwa yanauzwa kwa bei rahisi. Sasa hivi mianya imezibwa na kama bei hizo zinaendelea kuwa chini basi Mheshimiwa Mbunge atupe takwimu hizo ili tuweze kufuatilia na kubaini kama kuna tatizo la ukwepaji kodi. *(Makofi)*

Na. 109

**Kupitishwa kwa Bajeti ya kila Wizara**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza: -

Kwa kuwa kuna utaratibu kwamba Bunge hupitisha Bajeti za kila Wizara na Wizara hizo kutumia fedha zinazoombwa katika mipango yake ya kazi kwa mwaka mzima kwa maendeleo ya jamii: -

(a) Je, ni Wizara ngapi ambazo zimeshapewa fedha zote zilizoombwa kwa Bajeti mbili zilizopita?

(b) Je, ni Wizara ngapi ambazo hazipati fedha walizoomba na kupitishwa na Bunge?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutoa fedha za serikali ni wa *Cash Budget* ambao hutegemea mapato ya Serikali kwa mwezi au kwa kipindi husika. Sekta zinazopewa kipaumbele ambazo ni maji, elimu, afya, kilimo na barabara, hupewa fedha zake kwa miezi mitatu mitatu wakati Wizara nyingine hupata mgao wake kila mwezi. Aidha, inapotokea kwamba kuna mahitaji maalum uhamisho wa fedha hufanyika kukidhi mahitaji hayo hasa kutoka mafungu ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2000/2001 jumla ya shilingi 713,045,402,491/= zilikuwa zimetengwa kuendesha shughuli za Wizara, Asasi, Mikoa na Halmashauri za Wilaya na Miji. Kati ya kiasi hicho jumla ya shilingi 700,851,412,680/= au asilimia 98.3 zilitolewa. Fedha zote za Bajeti za sekta za huduma za kijamii, miuondombinu, Halmashauri, sekta za uzalishaji, vyombo vya ulinzi na usalama zilitolewa.

Kwa mwaka 2001/2002, kiasi cha shilingi 1,046,510,887,100/= kilitengwa kugharamia shughuli za Serikali na jumla ya shilingi 914,977,789,224/= au asilimia 87.4 zilizotolewa na kutumika ambapo pia fedha zote za sekta za huduma za jamii, miiundombinu, Halmashauri, sekta za uzalishaji na vyombo vya usalama zilitolewa kikamilifu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa za utoaji wa fedha, hakuna Wizara au Asasi, Mkoa au Halmashauri isiyopewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Fedha kidogo ambayo asilimia 13 ambayo haikutolewa kwa mwaka 2001/2002 ni vifaa ambavyo havikupokelewa kutoka kwa wahisani katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Nishati na Madini pia Mikoa ya Morogoro, Lindi, Mwanza na Kagera. Vifaa ambavyo havikupokelewa mwaka husika huendelea kuletwa mwaka unaofuata.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika Wizara zilizopewa kipaumbele ni kilimo, afya, maji na elimu na kwa kuwa Serikali ilifuta kodi za maendeleo kwa Halmashauri na kusema itafidia kwa *top up* pamoja na kuzipa pesa hizo. Je, Waziri haoni kuwa ucheleweshaji wa kutokuiwekea kipaumbele Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mikoa kwenye kilimo, maji na elimu inachangia kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi sekta zinazopewa kipaumbele na kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni maji, elimu, afya kilimo na barabara. Sasa fedha hizi hupitishwa kwenye Halmashauri moja kwa moja na zinatangazwa kwenye magazeti katika sekta ya elimu, maji nakadhalika. Kwa mfano fedha za *PEDEP, MMEM* zinapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri na hizi zinatangazwa kwenye magazeti.

Kwa hiyo, hizi kodi zilizofutwa ni kwa ajili ya *top up* ya Bajeti za Halmashauri fedha ambazo zilikuwa zinakusanywa na Halmashauri. Lakini fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kipaumbele zinakwenda moja kwa moja na hizo haziko kwenye utaratibu wa ku-*top up* kutokana na kodi ambazo zimefutwa. Kwa hiyo, Serikali inakipa kipaumbele katika sekta hizo na *top up* zinaendelea na Serikali imeshaanza kupeleka *top up* hizi kwenye Halmashauri zote nchini. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa muuliza swali la msingi na la nyongeza amezungumzia fedha za maendeleo ambazo Halmashauri za Wilaya zilikuwa zinajitengea katika Bajeti zao kabla ya Serikali haijafuta kodi.

Je, kwa kuwa Halmashauri zinamaliza mwaka wa fedha Desemba na kwa sasa tuko mwezi Novemba, Serikali imeshatuma fedha kiasi gani za maendeleo katika ku-*top up* zile ambazo zimo kwenye Halmashauri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Bajeti za Halmashauri zinaisha mwezi Desemba, lakini kuna utaratibu ambao unaandaliwa wa kuoanisha *(synchronize)* Bajeti za Halmashauri na Bajeti ya Serikali Kuu ili zote zianze mwezi Juni. Kuna zoezi ambalo linaendelea sasa kwenye Halmashauri limepelekwa agizo kwamba Halmashauri ziandae mini budget kwa ajili ya kipindi cha mpaka Juni ili itayarishwe *budget* nyingine kwa ajili ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, hili tatizo sidhani kama lipo kwa sababu taratibu zote zinaendelea na fedha ambazo zilikuwa zimepangwa kwenye Bajeti ya maendeleo kwenye Serikali Kuu kama *subventions* au *top up* kwenye Halmashauri zitaendelea kutolewa mpaka mwezi Juni.

Na. 110

**Ujenzi wa Bara Hifadhi ya Selous**

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO (k.n.y. MHE. BAKARI M. MBONDE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Uongozi wa Mradi wa Hifadhi ya Selous umekubali kusaidia ujenzi wa barabara inayounganisha Vijiji vya Mloka (Wilaya ya Rufiji) na Vikumbulu (Wilaya ya Kisarawe) ili kurahisha mawasiliano kati ya Wilaya hizo mbili na kusaidia ulinzi wa Hifadhi hiyo.

Je, ujenzi wa barabara hiyo utakamilika lini na utagharimu fedha kiasi gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII)**alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kurahisisha mawasiliano ya wananchi kati ya Wilaya ya Rufiji na Kisarawe kwa vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Selous, Wizara yangu kupitia Idara ya Wanyapori, Pori la Akiba la Selous ilijenga barabara yenye urefu wa kilometa 60 kwa gharama ya shilingi 50,000,000/= kuanzia Kijiji cha Vikumbulu Wilaya ya Kisarawe hadi kijiji cha Mtanza Wilaya ya Rufiji. Ujenzi huo ulifanyika kuanzia mwaka 1999 hadi 2000 kwa kung'oa miti na kuinua tuta kwa greda. Uwezo wa Wizara yangu kifedha ulikomea kwenye kiasi hicho cha fedha zilizotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke wazi kuwa ujenzi wa barabara, hasa katika maeneo yanayozunguka Mapori ya Akiba, siyo jukumu la msingi la Wizara yangu. Hivyo ujenzi wa barabara tajwa ni mojawapo ya michango ya Wizara yangu katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa jamii na hivyo kuwapunguzia wananchi kero na kupunguza kiwango cha umaskini miongoni mwao, kipaumbele kikielekezwa zaidi kwa vijiji vinavyopakana na mapori ya akiba na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali na Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Ili barabara hii iweze kupitika majira yote, kunahitajika makaravati kwenye vijito na sehemu korofi maeneo ya Lambo la Msanga. Aidha, kunahitajika kumwaga changarawe sehemu zenye udongo wa mfinyanzi kwa umbali unaokadiriwa kufikia kilometa 10 za maeneo ya Lambo la Msanga.

Kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, Wizara yangu kupitia uongozi wa Pori la Akiba la Selous, inawasiliana na Mkoa wa Pwani ili kuiomba *TANROADS* Mkoa iweze kuchangia gharama za kukamilisha matengenezo ya barabara hiyo na kuiwezesha barabara nzima kupitika katika majira yote ya mwaka.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba nimuulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kati ya mwaka 1999/2000 Wizara kupitia Mradi wa Selous imeweza kutumia milioni kati ya 45,000,000 mpaka 50,000,000 kwa kutengeneza barabara. Kwa jitihada hizo wananchi wa Vijiji vya Mloka na Vikumbulu sasa angalau wamepata nafasi. Je, yuko tayari kupokea shukrani za wananchi wa Kisarawe na Rufiji kwa jitihada hizo? *(Makofi)*

(b) Kwa vile kwa maelewana baina ya mradi wa Selous na Halmashauri ya Kisarawe, tayari Mwandisi wa Kisarawe ameshafanya usanifu wa kuiboresha barabara hiyo katika kiwango hicho alichokuwa akizungumzia Mheshimiwa Waziri. Je, sasa Wizara iko tayari kuweka nguvu zake zaidi ili kusudi kazi iliyokwishaanza ya kutaka kuiboresha barabara hii iweze kukamilishwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Napokea shukrani kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe.

La pili inawezekana ni kweli kazi hii kulikuwa na makubaliano lakini kimsingi tumejua barabara hii ili iwe endelevu lazima tutafute watu wenye misuli mikubwa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifikiri tuwaombe wenzetu wa *TANROAD* na mazungumzo yanaendelea vizuri ili waweze kutupokea kuendelea na hii barabara, lakini endapo itapandishwa hadhi na kuwa katika hali yao kwa sababu hata tukifanya kwa mwaka wa kwanza tunajua baada ya mvua huwa barabara hii inaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitaendelea kufuatilia hayo makubaliano ya Mheshimiwa Mbunge na Mhifadhi wa Selous ili kuona kama uwezekano huo wa ombi la ziada alilolitoa leo kama linaweza likatekelezeka.

Na. 111

**Barabara Iendayo Sokoine**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine ni Taasisi muhimu kwa Taifa letu inayotutolea watalaam na viongozi wa baadaye na kwa kuwa barabara hiyo itokayo mjini kuelekea hapo chuoni ambayo zamani ilikuwa ya Mkoa *(Old Iringa Road):-*

(a) Je, Serikali itairejesha kwenye hadhi yake ikiwa Barabara ya Mkoa?

(b) Kwa kutumia Mfuko wa Barabara, je, Serikali inaweza kuisaidia Halmashauri ya Manispaa kuijenga kwa kiwango cha lami ili hadhi ya Chuo chetu ilindwe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara iendayo Sokoine kilikuwa chini ya barabara ya Mkoa kabla ya kufanyika matengenezo makubwa mwaka 1972 ambapo ulijengwa mchepuko *(re-alignment)* kupitia maeneo ya Chamwino, Mindu hadi Sangasanga. Kwa sasa hivi, barabara yenye urefu wa kilometa 1.55 iko chini ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Hata hivyo zoezi la kupanga upya madaraja kwa barabara zote nchini, ikiwemo hii ya kutoka Morogoro Mjini hadi Chuo Kikuu cha Sokoine itafanyika mara baada ya kukamilika kwa mapitio ya Sheria ya Barabara *(Highway Ordinance)* yanayoendelea hivi sasa. Zoezi za kupanga madaraja ya barabara zote nchini litakapokamilika ndipo itakapofahamika endapo barabara hii inakidhi vigezo vilivyokubalika na kuwa chini ya barabara za Mkoa au iendelee kuwa chini ya Manispaa kama ilivyo sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tayari imefanyiwa ukarabati *(rehabilitation)* kwa kiwango cha lami chini ya Mpango wa *Urban Sector Rehabilitation Project(USRP),* uliofadhiliwa na *IDA.* Kazi zote zilizopangwa kwa mujibu wa Mkataba zimekamilika na barabara imekwisha funguliwa kwa matumizi.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali:-

Kwanza niishukuru Serikali kwa kuchelewesha kujibu swali hili ili kuvuta muda wa kuitengeneza barabara hii, naamini kwamba kama uaskari miavuli hapa imekamilika nawashukuru sana. Lakini pamoja na shukrani hizo ningependa kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara hii ni muhimu kwa Taifa ukizingatia kuwa licha ya kuwepo taasisi hii ya Elimu ya Juu pia inaendelea hadi Shirika la Mzinga ambalo lina kiwanda pekee nchini ambacho tulitegemee upekee kwa taifa wa bidhaa zinazotengenezwa pale. Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kumalizia kipande kile kisichozidi km 2 kwa kiwango cha lami ili kiwanda hiki kiweze kupata heshima yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba barabara hii ni muhimu na ni kweli kwamba inaendelea mpaka kwenye Kiwanda cha Shirika la Mzinga lakini naye vile vile anafahamu hali yetu ya kifedha jinsi ilivyo, lakini tuvute muda ili kama barabara hii itapanda daraja na kuwa ya mkoa basi tutaitengeneza mpaka huko. *(Makofi)*

Na. 112

**Ujenzi wa Barabara Nchini**

**MHE. SULEIMAN AHAMED SADIQ (k.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefikia maamuzi ya kuzifanyia matengenezo na kujenga barabara kwa nguvu zetu wenyewe na kwa msaada wa wafadhili.

Je, ni barabara za kilometa ngapi zimetengenezwa kwa kiwango cha lami kwa nchi nzima na ni kilomita ngapi za barabara zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na ni kilometa ngapi zinakusudiwa kujengwa na zile kilometa zitakazobakia zinatarajiwa kujengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Jimbo la Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kipaumbele katika ukarabati na matengenezo ya barabara kwa nchi nzima kwa sababu ni sehemu muhimu ya miundombinu inayochangia kwa kiasi kikubwa kuboresha na kuimarisha uchumi wa Taifa na hivyo kupunguza umaskini. Jumla ya kilomita 5,000 zimejengwa kwa kiwango cha lami, kilomita 24,400 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na zaidi ya kilomita 5,300 zinakusudiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zilizosalia zitajengwa kufikia kiwango cha lami kadri Serikali, itakavyopata uwezo wa kifedha kutekeleza miradi hiyo chini ya lengo la kuunganisha kwa barabara za lami Makao Makuu ya Mikoa yote na nchi jirani. Aidha, ujenzi wa barabara mpya za changarawe utaendelea kutekelezwa kulingana na mahitaji ya njia mpya za usafirishaji kama vile kwenye Mikoa na Wilaya mpya.

**MHE. SULEIMAN AHMED SADIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili.

(a) Kwa kuwa barabara ni ukombozi katika uchumi na kwa kuwa wananchi wengi wa vijijini hali zao zinazidi kuwa duni kila siku kutokana na hali za barabara na kwa kuwa barabara ya kutoka Korogwe - Handeni - Turiani - Mvomelo hadi Dumila ilikuwa ndiyo barabara ilikuwa inapitika katika miaka ya nyuma na katika hotuba ya Waziri wa

Ujenzi mwaka huu, Naibu Waziri alitoa taarifa kwamba barabara hii iko katika hatua za awali.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

(b) Kwa kuwa ziko barabara za mkoa ambako ziko chini ya *TANROAD* na ambazo hazijatengenezwa kwa zaidi ya miaka 10 ikiwemo barabara ya Mvomelo, Ndole, Kibati. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mbunge wa Mvomelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu wakati wa Bajeti nakumbuka nilisema kwamba barabara ya Korogwe hadi Dumila ilikuwa inafanyiwa *feasibility study* ili ikiwezekana iwe barabara mbadala badala ya ile ya kupita Morogoro - Mikumi. Hilo bado linafanyika na *feasibility study* haichukui muda mfupi kiasi hicho. Tutakapokamilika tutachukua hatua zinazofuata.

Barabara ya Mvomelo hadi Kibati iko chini ya *TANROAD* na itatengenezwa kufuatana na kipato cha Serikali. Lakini kwa kuwa na yeye ni Mjumbe wa Bodi ya Mkoa nafikiri watapanga kikamilifu kutumia fedha hizo za mkoa zinazokwenda ili kutengeneza barabara hiyo. *(Makofi)*

Na. 113

**Elimu ya Watu Wazima**

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa shabaha ya Elimu ya Watu Wazima ilikuwa kuwawezesha wananchi kusoma na kuandika kwa lengo la kuandaa wananchi kupata taaluma zinazohitajika kujifunza pamoja na mambo mengine mbinu bora za ufugaji na kilimo na kwa kuwa lengo hilo halikutekelezwa kutokana na kukosekana kwa vitabu vya kufundishia, upungufu wa walimu na wakaguzi, kuvunjika moyo kwa walimu na wakaguzi, usafiri wa walimu/wakaguzi na wawekezaji.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kwa kushirikisha Wizara ya Elimu na Utamaduni na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Elimu hiyo bado ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu kutafsiri kwa vitendo mbinu mpya za elimu ya ugani kuwawezesha kuwa wabunifu na kuinua maendeleo ya uchumi wa kilimo na ufugaji?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah Mbunge wa Kilosa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kwa miaka mingi baada ya Uhuru shabaha muhimu ya Elimu ya Watu Wazima ilikuwa kuwawezesha wananchi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa lengo la kuwandaa wananchi kupata taaluma mbalimbali ikiwa ni pamoja na mbinu bora za ufugaji na kilimo.

Serikali ilianzisha katika Wizara yangu kurugenzi maalumu ya Elimu ya Watu Wazima na iliunda kitengo cha Elimu Watu Wazima katika kila ofisi ya elimu ya wilaya kwa lengo la kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu hiyo. Aidha, kila Wilaya hapa nchini inaye Afisa Elimu kilimo na ufugaji mwenye jukumu la kuhakikisha utoaji wa elimu ya kilimo na ufugaji bora kwa wananchi kupitia Elimu ya Watu Wazima kwa kushirikiana na watalaam wa sekta hizo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba utoaji wa Elimu ya Watu Wazima kwa sasa unakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na upungufu wa walimu. Wizara yangu inachukua hatua mbalimbali za kuimarisha mafunzo ya elimu ya watu wazima hapa nchini ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa elimu ya watu wazima kupitia programu ya Mpango wa Uwiano Kata ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii *(MUKEJA).* Programu hii inalenga kuwashirikisha wananchi katika kuibua matatizo yao, kujadili utatuzi wake, kupanga, kutekeleza na kutathmini programu mbalimbali za kujiletea maendeleo.

(ii) Kubadilisha mtindo au mbinu na njia za ufundishaji kwa kuanzisha mbinu mpya ya *RIFLEKTI* yaani mbinu shirikishi katika kujifunza.

(iii) Kuoanisha stadi za kisomo na miradi midogo midogo ya uzalishaji mali katika madarasa ya watu wazima (kilimo, ufugaji, ufundi na sayansikimu). Miradi hii itakuwa vivutio (motisha) kwa wananchi ili kuinua kipato chao na uchumi wa taifa kwa jumla.

(iv) Kuwashirikisha wananchi wanaoshiriki mafunzo pamoja na wataalamu wengine vijijini katika uandishi wa vitabu vya kusoma.

Na. 114

**Ujenzi wa Uzio Shule ya Sekondari Mwenge**

**MHE. JUMANNE H. NGULI** alijibu:-

Kwa kuwa shule ya Sekondari ya Mwenge sasa iko katikati ya Mji na kwa kuwa shule hiyo zamani ilikuwa na uzio wa waya na minyara ambayo sasa uzio huo ulishaharibiwa na wanafunzi watoro na watu wahalifu kiasi cha kuhatarisha usalama wa wanafunzi na mali za shule na kwa kuwa shule hiyo ilishaomba kupatiwa fedha kwa ajili ya kuwekewa uzio imara.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha hiyo ili shule iweke uzio na hivyo kulinda wanafunzi na mali na kukomesha watu wanaopita katikati ya shule?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uzio wa Shule ya Sekondari ya Mwenge umeharibika. Uharibifu huo haukuletwa na wanafunzi watoro au watu wahalifu peke yao, bali pia na mifugo iliyopo mjini hapo. Wizara imeshaanza kulishughulikia suala hilo kwa kutengeneza makadirio ya uzio huo wa urefu wa mita 2,700. Ujenzi wa uzio unakadiriwa kugharimu shilingi 23,000,000/=. Hadi sasa Wizara yangu imeshatuma shuleni hapa shilingi 5,000,000/= kwa kuanza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeshatoa maelekezo kwa Mkuu wa shule kuwadhibiti wanafunzi waliopo na kuwachukulia hatua za kinidhamu wanafunzi watoro na wale watakaobainika kuhujumu kwa makusudi mali ya umma. Katika suala hili, namwomba Mheshimiwa Mbunge katika nafasi azungumze na wananchi namna watakavyosaidiana na uongozi wa shule, kulinda mali ya umma iliyopo shuleni pamoja na uzio unaojengwa ili usiharibiwe tena na watu waharibifu pamoja na mifugo yao.

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa sasa hivi wanafunzi wanalazimika kupeana zamu ya kulinda mchana eneo lao ili wasije wakaibiwa wakati wakiwa madarasani. Ni wazi kwamba wakati wanapokuwa wanalinda wanakosa masomo kwa wakati huo.

(a) Je, Wizara inaweza kuongeza walinzi wa mchana ili wanafunzi hawa wasiendelee kupoteza masomo yao? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa *system* yote ya vyoo vya ndani imeharibika mpaka sasa hivi na *sewerage* ambayo ilikuwepo pia imeharibika na kwa hiyo wanafunzi hulazimika kwenda kujisaidia nje ya vyoo ambavyo ndiyo vimetengenezwa usiku ambayo ni hatari kwa sababu ya kutokuwa na uzio.

Je, Serikali pia inaweza ikatengeneza *system* yote ya vyoo hivi vya ndani ili wanafunzi wawe na amani ya kujisaidia ndani bila kupoteza muda huo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Jumanne Nguli, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru kwa kunitaarifa hali halisi ya hapo shuleni isiyoridhisha. Sasa kwa maswali yake mawili napenda kumjibu kama ifuatavyo:-

Hili la kwanza kwamba wanafunzi wanakosa masomo kwa sababu ya kufanya zamu za ulinzi. Nakubaliana naye kwamba jambo hilo sio zuri, lazima tuweke kila jitihada kwamba wanafunzi hawakosi kupata masomo darasani bila sababu za kutosha. Kwa hiyo, tutaangalia uwezekano wa kurekebisha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu wanafunzi kutumia vyoo vya nje kwa sababu vya ndani vimeharibika; napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari ambao Wizara yangu inaukamilisha na tunatarajia uanze mapema iwezekanavyo mwaka kesho, utakuwepo ujenzi wa shule mpya lakini pia ukarabati wa shule zetu nyingi ambazo ziko katika hali mbaya sana ikiwemo hii anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie kwamba itakuwemo katika mpango huu ambao tunatarajia uanze mwaka kesho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na leo maswali yamekwisha. Pamoja na *speed* isiyokuwa ya kawaida, lakini tumemaliza *actually*.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo kadhaa. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake wakutane Chumba Na.428 ghorofa ya nne saa 4.30 leo Asubuhi kupitia Muswada wa *National Microfinance Bank*. Pia Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo Mkutano leo saa 5.00 Chumba Na.231 ghorofa ya pili.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala, Mheshimiwa Athumani Janguo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake ya Katiba na Sheria wakutane saa 7.00 leo mchana kwenye Ukumbi Na.227 ghorofa ya pili. Kikao hiki ni saa 7.00.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kikao saa 5.00 leo asubuhi, Chumba Na. 227 na Mwenyekiti amewaomba wote wahudhurie wana jambo la dharura la kuilishughulikia..

Sasa Matangazo ya vikao vya Vyama vya Hiari. Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanaotoka Zanzibar, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane. Yeye alisema mara moja baada ya kikao cha Bunge. Mara moja baada ya Kikao cha Bunge, siyo mara moja baada ya maswali, maana yake saa 7.00.

Pia, Mwenyekiti wa Chama cha Hesabu za Watu na Maendeleo, Mheshimiwa Paul Kimiti anawatangazia Wajumbe wa Chama hicho kwamba kutakuwa na Mkutano kuanzia saa 7.00 baada ya kikao hiki, lakini watajadili masuala ya warsha na semina baada ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kimiti anataka kufafanua.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani. Nilitaka niombe Wajumbe wote wa Chama cha Idadi ya Watu na Maendeleo ya kwamba tumeandaa Semina ya siku tatu ambayo itaanza tarehe 20 mpaka tarehe 22. Tunaomba wale ambao watakuwa na nafasi wajiandikishe Chumba Na.37, tuko hapa. Wengine wanaweza kuwa hawana nafasi, nataka nijue ni wangapi. Malipo yatalipwa kwa siku hizo tatu. Ni taarifa tu.

**WABUNGE FULANI:** Hapa hapa?

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Hapa hapa Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mkikutana mtapanga ni wapi, ili tusikwamishe shughuli yetu. Baada ya matangazo hayo, sina tangazo lingine. Sasa tunaendelea. Katibu agenda inayofuata.

## KAULI ZA MAWAZIRI

## KUHUSU FIDIA YA GHARAMA YA USAFIRISHAJI WA MBOLEA KATIKA MIKOA YA NYANDA ZA JUU KUSINI

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kutoa kauli ya Serikali hapa Bungeni kuhusu fidia ya sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika msimu wa kilimo wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha alipowasilisha hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2003/04 mbele ya Bunge lako Tukufu katika Kikao cha tatu cha Mkutano wa 12 kilichofanyika tarehe 12 Juni, 2003, alieleza azma ya Serikali ya kutoa ruzuku kwa mbolea kwa Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa zao la mahindi.

Katika hotuba yangu ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2003/2004 niliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 30 Juni, 2003, nilijulisha Bunge lako Tukufu kwamba na ninaomba kunukuu: “Katika mwaka wa 2003/2004 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kufidia gharama za usafirishaji wa pembejeo muhimu hasa mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.”

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu wa Serikali kutoa ruzuku kwa usafirishaji wa mbolea ulitokana na mambo makuu matatu.

La kwanza, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hupata mvua za uhakika kila mwaka hata katika miaka ambayo nchi hupata mvua zisizokuwa za kuridhisha.

Pili, ardhi ya Mikoa hiyo ina upungufu mkubwa wa madini na uzalishaji wa mazao katika maeneo yaliyo mengi katika Mikoa hiyo unawezekana tu kwa kuongeza virutubisho kwenye udongo kwa kutumia mbolea za chumvichumvi.

Tatu, katika mwaka 2002/2003, katika maeneo mengi ya nchi mvua zilinyesha chini ya viwango vya kawaida na kwa mtawanyiko mbaya na maeneo mengi ya nchi yalipata ukame uliosababisha kushuka kwa uzashilishaji wa mazao ya chakula na mazao kukauka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Taifa linakabiliwa na upungufu wa chakula na kuna uwezekano mkubwa wa hali mbaya ya hewa kuendelea katika mwaka wa 2003/2004. Lengo la kutoa ruzuku ya mbolea kwa Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini, ni kuwezesha Mikoa hiyo kuzalisha chakula kwa wingi ili ijitosheleze kikamilifu na kuwa na ziada itakayotumika kulisha maeneo yatakayokabiliwa na upungufu wa chakula.

Baada ya Serikali kujitoa katika uagizaji na usambazaji wa mbolea na kuruhusu Makampuni binafsi kufanya kazi hiyo kuanzia mwaka 1992, bei za mbolea zimekuwa zikipanda mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mbeya, bei ya mbolea aina ya *DAP* ilipanda kutoka shilingi 13,500/= msimu wa 2001/2002 hadi shilingi 18,000/= kwa mfuko mmoja wa kilo 50 katika msimu wa 2002/03. Mfuko huo unauzwa kwa shilingi 20,000/= katika msimu huu.

Kutokana na upandaji wa bei, matumizi ya mbolea yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano katika Mkoa wa Rukwa, matumizi ya mbolea aina ya *Urea* yaliteremka kutoka tani 746 katika mwaka 2000 hadi tani 269 tu katika mwaka 2001. Mwaka wa 2002 matumizi ya mbolea hiyo yalipanda kidogo hadi tani 295.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutenga shilingi milioni 500 kwenye Bajeti yake ya mwaka 2003/2004 kwa ajili ya kutoa ruzuku kwenye usafirishaji wa mbolea, ilitambua kwamba hatua hiyo peke yake haingetosha kuwahakikishia wakulima wa Nyanda za Juu Kusini upatikanaji wa mbolea kwa wingi na kwa bei nafuu.

Mnamo mwezi wa Julai, 2003, Serikali iliunda Kamati ya Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha ambapo alikuwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo na Chakula, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mipango na Ubinafsishaji na Ofisi ya Waziri Mkuu kuweka utaratibu wa kutumia fedha zilizotengwa kufidia gharama za usafirishaji wa mbolea na kubuni utaratibu utakaohakikisha kwamba mbolea inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushauri wa Kamati wa Makatibu Wakuu, Serikali imeiwezesha Kampuni ya Mbolea ya Tanzania inayoitwa *TFC* kwa kifupi kuagiza mbolea moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa mbolea hizo kwa kuwapatia shilingi 3,500,000,000/=. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kwamba tunapata mbolea kwa wingi na kwa bei nafuu ambazo zitawafanya wauzaji wengine wa mbolea washindwe kupandisha bei za mbolea kiholela. Hadi tarehe 31 Oktoba, 2003 tani

5000 za *Urea,* tani 2,750 za *Can* na tani 500 za *NPK 201010,* ilikwishakupokelewa na kuanza kusambazwa.

Mwaka huu tunakusudia kutilia mkazo matumizi ya mbolea ya *Minjingu Rock Phosphate* ambayo inapatikana kwa wingi humu humu nchini na *TFC* wamekwishanunua tani 500 za mbolea hiyo. Mbolea hizo zinaendelea kusambazwa kwenye Vituo vya Makambako, Njombe, Songea, Mbeya na Sumbawanga. Kwa taarifa tu, Serikali imeamua kutokubinafsisha Kampuni ya Mbolea ili ibaki kuwa chombo cha wakulima cha kusimamia mbolea. *(Makofi)*

Serikali iliridhika pia kwamba kiasi cha shilingi milioni 500 kilichotengwa hakingetosha kupunguza bei ya mbolea kwa Mkulima kwa kiwango cha kuridhisha. Ili kuhakikisha kwamba mkulima anapata mbolea kwa bei nafuu inayoainishwa kuwa kati ya shilingi 10,000/= na shilingi 14,000/= kwa mfuko wa kilo 50, Serikali imetenga nyongeza ya shilingi 1,500,000,000/= na kufanya fedha zote zilizotengwa kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kuwa shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matumizi ya mbolea katika Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini kati ya mwaka 1985 na 2002 unaonesha kwamba kwa wastani Mikoa hiyo hutumia tani 59,426 za aina mbalimbali za mbolea kwa mazao ya chakula. Mgawanyo wa mbolea hizo Kimkoa ni kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Iringa hutumia tani 20,713, Ruvuma tani 17,481, Mbeya tani 18,225 na Rukwa tani 3,007.

Mheshimiwa Naibu Spika, uagizaji na usambazaji wa mbolea kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini unafanywa na Makampuni kumi. Hadi tarehe 10 Novemba, 2003 kiasi cha mbolea ambacho kilikwishapatikana na kusambazwa Mikoani kilikuwa ni tani 32,525 sawa na asilimia 55.4 ya mahitaji ya mbolea ya Nyanda za Juu za Kusini. Mgawanyo wa mbolea hiyo Kimkoa ni kama ifuatavyo:-

Iringa wamekwishapata tani 13,062 sawa na asilimia 63 ya mbolea wanayohitaji, Ruvuma tani 4,830 sawa na asilimia 27.6; Mbeya tani 12,682 sawa na asilimia 69.6 na Rukwa tani 2,351 sawa na asilimia 78.2 ya mahitaji yao ya mbolea. Hadi sasa Mikoa hiyo imekwishapata asilimia 55.4 ya mbolea wanayohitaji.

Mbolea iliyoko Dar es Salaam kwenye maghala ya Makampuni yanayoagiza mbolea kutoka nje ya nchi ni tani 20,920. Nayo pia imegawanyika kama ifuatavyo:-

*HA* kuna tani 66. Hatupendi sana matumizi ya *HA* kwa sababu inaharibu udongo, *Can* tani 3,543, *Urea* tani 15,919; *TSP* tani 1,241 na *DAP* tani 151. Jumla ni tani 20,920.

Makampuni yanayoagiza mbolea kutoka nje yameahidi kuagiza tani 79,000 kwa matumizi ya nchi nzima. Hii siyo kwa matumizi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini peke yake, ni kwa matumizi ya nchi nzima. Tani 66,014 zikiwa ni kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula. Aina hizi za mbolea zinagawanyika kama ifuatavyo:-

*HA* tani 10,000, *Can* tani 12,000, *Urea* tani 41,014, *TSP* tani 2000 na *DAP* tani 1000 kufanya tani 66,014. Mbolea hiyo inatarajiwa kuwasili nchini kuanzia mwezi huu hadi mwezi wa tatu mwaka 2004. Sehemu ya mbolea hiyo itajazia pengo la tani 26,500 ya mahitaji ya mbolea ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matumaini mazuri ya upatikanaji wa mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, inatarajiwa kwamba kutakuwepo na upungufu wa mbolea za kupandia. Mahitaji ya *DAP* kwa Mikoa hiyo ni tani 3,834, lakini inatarajiwa kwamba tani 1,903 tu ndiyo itakayopatikana na kuacha pengo la tani 1,931. Pengo hilo linaweza kujazwa na *Minjingu Rock Phosphate* ambayo inapatikana kwa wingi humu nchini. Tatizo tu ni kwamba wakulima hawana mazoea ya kutumia *Minjingu Rock Phosphate* na wengi hawana imani na aina hiyo ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa unaonesha kwamba shilingi bilioni mbili zilizotengwa na Serikali zitawezesha kupunguzwa kwa gharama za usafirishaji wa mbolea kutoka Dar es Salaam hadi Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa asilimia 82. Kiasi cha fedha hizo, kitatumiwa pia kupunguza bei ya mbolea ya *DAP* kutoka shilingi 15,802,090/= kwa mfuko wa kilo 50 hadi shilingi 14,000/=.

Utaratibu huu utawezesha mbolea kuuzwa kwa bei ya shilingi 10,000/= hadi shilingi 14,000/= kwa mfuko wa kilo 50 katika Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea katika Mikoa kutegemeana na aina ya mbolea. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba katika Mikoa yote na katika Vituo vya kupokelea mbolea, mbolea haitazidi shilingi 14,000/=. Mbolea ya aina moja itakuwa na bei sawa kwenye Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea kwenye Mikoa ambako ni Makambako kwa Mkoa wa Iringa na Makao Makuu ya Mikoa ya Ruvuma yanayoitwa Songea, Mbeya na Rukwa ambayo Makao Makuu yake yako Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea yoyote ambayo itasafirishwa kutoka Dar es Salaam hadi kwenye Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea kwenye Mikoa itapewa ruzuku kwa viwango vinavyohusika. Kwa maana nyingine mbolea inayokwenda Rukwa itapewa ruzuku kubwa zaidi kuliko mbolea inayokwenda Iringa. Ndiyo maana ya viwango vinavyohusika.

Mbolea ambayo ilikwishapokelewa Mikoani kabla ya utaratibu huu kuanza, itakaguliwa na Maofisa watakaoteuliwa na Mikoa kwa ajili hiyo nayo pia itapewa ruzuku kwa viwango vinavyohusika. Wote watakaopewa fidia ya sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea wataingia katika mikataba ya kisheria na Serikali, kwamba watauza mbolea iliyopata fidia kwa bei ya makubaliano ambayo itakuwa kati ya shilingi 10,000/= na shilingi 14,000/= tu kutegemeana na aina ya mbolea.

Orodha ya Makampuni yanayosambaza mbolea yaliyoingia kwenye mikataba na Serikali pamoja na nakala za mikataba hiyo itasambazwa kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu

wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya ili wahusike kikamilifu katika kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo.

Kutakuwepo na Kamati za Usimamizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kamati ya Mkoa itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

Mkuu wa Mkoa atakuwa Mwenyekiti, Afisa Tawala atakuwa Mjumbe, Wakuu wa Wilaya zilizoko katika Mkoa, Mshauri wa Kilimo wa Sekretarieti ya Mkoa atakuwa Katibu, Mshauri wa Biashara katika Sekretarieti, Wakurugenzi wa Halmashauri zilizoko katika Wilaya.

Kazi kubwa za Kamati hii itakuwa ni kuhakiki mbolea iliyopo Mikoani, kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Usafirishaji na Uuzaji wa mbolea, kuratibu na kutoa taarifa Wizarani kuhusu Makampuni yaliyofikisha mbolea na kiasi cha mbolea kilichofikishwa katika Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea. Kuratibu na kufuatilia mahitaji ya upatikanaji wa mbolea.

Katika Wilaya kutakuwepo na Kamati itakayokuwa na Mkuu wa Wilaya kama Mwenyekiti wake, Mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya, Afisa Kilimo wa Wilaya, Afisa Biashara na Waheshimiwa Wabunge, tunawaomba wakubali kujiunga na Kamati hiyo.

Kamati ya Wilaya itakutana mara moja kila wiki na kazi zake zitakuwa ni kuratibu usambazaji na uuzaji wa mbolea katika maeneo yote na kuhakikisha kwamba bei za mbolea kwa mkulima haziwi juu sana zikilinganishwa na bei za mbolea katika Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea. Tunatarajia kwamba Kamati hizi zitatusaidia kuhakikisha kwamba mbolea inamfikia mkulima kwa ile bei inayokusudiwa kwa kuhakikisha kwamba watu hawachukui mbolea kwenye vile Vituo na kwenda kulangua, kuratibu mawakala wa mbolea katika Wilaya na kutoa taarifa katika ngazi ya Mkoa juu ya hali ya mbolea katika Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wanapata mbolea kwa bei nafuu, zina lengo la kuwaongezea wakulima hao uhakika wa chakula na mapato, lakini muhimu zaidi zina lengo la kuhakikisha kwamba Mikoa hiyo inazalisha chakula kwa wingi kwa ajili ya kulisha maeneo yatakayokuwa na upungufu wa chakula katika mwaka wa 2003/2004 na 2004/2005. Wananchi wote wanakumbushwa wito wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyotoa tarehe 30 Machi, 2003 alipowataka wananchi watumie chakula kwa uangalifu, wajiwekee akiba na watumie fursa zote walizonazo za kuzalisha chakula cha nyongeza ili kujihakikishia upatikanaji wa chakula. Inabidi tujiandae kupambana na ukame na njaa, iwapo mvua za mwaka 2003/2004 zitakuwa mbaya kama zilivyokuwa mwaka 2002/2003. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na janga kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali siku zote inawathamini sana wakulima na inafanya yote yaliyo ndani ya uwezo

wake ili kutafuta njia za kuongeza uzalishaji na hivyo kuwaongezea kipato. Kama ilivyotenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa msimu huu wa 2003/2004, Serikali itaendelea kutafuta njia za kuwasaidia wakulima katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 10 Novemba, 2003 Mawaziri wa Fedha, Viwanda na Biashara na Kilimo na Chakula walikutana na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa hiyo kwa kufuatilia suala la upatikanaji wa mbolea kwa uadilifu mkubwa sana. Ahsanteni sana. Nawahakikishia kwamba makubaliano yote tuliyofikia, ikianza na utoaji wa tamko hili, yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe kauli ya Serikali rasmi kwamba bei ya mbolea kwenye Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini itakuwa kati ya shilingi 10,000/= na shilingi 14,000/= kutegemeana na aina ya mbolea. Bei ya mbolea ya aina moja itakuwa sawa kwa Vituo vyote Vikuu vya kupokelea mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kwamba utaratibu wa kutoa ruzuku ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea hadi kwenye Vituo Vikuu vya kupokelea mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, inaanza mara moja. Kwamba mbolea iliyokwishafikishwa Mikoani itapewa ruzuku kwa viwango vinavyohusika baada ya kuhakikishwa na uongozi wa Mkoa.

Wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wanashauriwa kujinunulia mahitaji yao ya Pembejeo na hususan mbolea mapema wakati barabara bado zinapitika wasisubiri mpaka mvua zikaanza kunyesha kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Kwa nia njema tu, kwa kuwa kanuni Na.39(2) na (1) kiko kimya kuhusu Mbunge kupata maelekezo zaidi kuhusu Kauli ya Mawaziri, je, unaweza ukaniruhusu nipate ufafanuzi kwa kutumia busara zako?

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu tuna mengi ya kufanya na kauli imetolewa na unaweza tu kupata ufafanuzi kutoka kwake, nafikiri tuendelee ili shughuli zetu zisikwame kwa sababu tuna shughuli nyingi sana. Katibu, *agenda* inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uvuvi wa Mwaka 2003
***(The Fisheries Bill, 2003)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana walibaki wachangiaji watatu wa Muswada wa Sheria ambao unaendelea. Wachangiaji hao ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Sasa namwita Mheshimiwa Ruth Msafiri.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu. Inaonesha kwamba Serikali imejizatiti katika hatua zote za kuendelea kutekeleza sera zake kwa lengo la kupunguza kero au kuondoa kero kabisa pale ambapo inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inafuta sheria ya mwaka 1970 na inakusudia kuweka mazingira endelevu ambayo yataweza kuweka hali bora kwa wavuvi na samaki na hata mazao yake mengine. Sheria hii inalenga kusimamia raslimali za uvuvi na kuweka viwango vya ubora wa mazao ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nilikuwa naomba nieleze kidogo pale kwenye ibara ya nne, sehemu ya tano. Hapa Mkurugenzi amepewa nafasi ya kushughulikia mambo mbalimbali yanayotokea kwenye eneo lake, lakini kipengele kidogo cha tano, kama pale yule mtu ambaye amepewa uamuzi na Mkurugenzi hakuridhika anaambiwa kwamba kwa muda wa siku 30 anaweza kuwa amepeleka rufani yake kwa Waziri. Lakini sikuona Waziri amepewa muda gani kuwa ameshughulikia jambo hilo na kumpa uamuzi yule ambaye atakuwa amelalamika.

Kwa hiyo, ningeomba suala hilo likaongezwa hapo, kwamba muda uwepo.

La pili, nimeona kwamba Mkurugenzi huyu amepewa majukumu mengi sana kwa sheria hii, lakini sikuona kama amepewa msaidizi. Licha ya wale Maofisa mbalimbali watakaoteuliwa na kuwa kwenye maeneo mbalimbali yanayohusika na masuala yote ya uvuvi, lakini hana mtu mwingine anayemsaidia.

Kwa hiyo, ningeshauri akawepo Naibu Mkurugenzi ili kazi hizi ziweze kufanyika kwa wakati wote, kwa sababu wakati ni mali. Itakuwa ni taabu kama Mkurugenzi hayupo, yale maswali yake mengine hakuna mtu ambaye anaweza kuyashughulikia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Muswada huu kama ambavyo Kamati iliuchambua, Kamati ilitueleza kwamba yenyewe iliona Muswada huu unalenga kuboresha shughuli na maisha ya wavuvi wadogo wadogo na hasa kulenga kuwaondolea umasikini.

Mimi katika kujaribu kuangalia Muswada huu, nimeona pengine kuna mambo ambayo katika kuhakikisha kweli mvuvi anasaidiwa, basi ni vizuri na mambo haya yakazingatiwa, ni pamoja na ibara ya 30(a) na (b). Pale kwenye sehemu ya (b) mimi

sikuridhika vizuri ninavyoona kile kipengele kinavyosomwa pale, kwamba mojawapo ya huu mfuko unaokwenda kuundwa kwa ajili ya kuendeleza uvuvi, (b) inasema: *"Promote and assist in the development of community management units by giving grants and assisting groups of persons wishing to form fisheries conservation and protection groups."*

Mimi nilipokuwa nikiangalia nimeona kama haikuzingatia ipasavyo kumweka wazi mvuvi wa samaki naye kuona kwamba eneo hili litamsaidia kwa kiwango gani. Nimeona zaidi hapa inakusudia kutunza pengine mazalia ya samaki na kuyalinda yale makundi ambayo yatakuwa yanashughulikia mazingira kama ya *BM Unit* na mengine. Lakini nimeona kama hapa mvuvi mwenyewe hakupata nafasi ipasavyo.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwenye lile eneo kwamba ili kuweza kumwezesha huyu mvuvi na mwenyewe kuinua mtaji wake, kumwezesha mvuvi naye kuwa na zana za kuendesha uvuvi ipasavyo, lakini zaidi kumpa mazingira yatakayomwezesha huyu mvuvi ambaye ni mvuvi mdogo ambaye kwa kiwango ambacho kabla sheria haijakuwepo, sheria ambayo inafutwa sasa ilikuwa haikuweka mazingira ipasavyo ya kumfanya mvuvi mdogo naye aweze kushiriki ipasavyo katika shughuli ya uvuvi, badala yake alifanya zaidi kazi zilizoonekana ni za upagazi ambazo yeye inatakiwa akafanye kazi kwa kibarua alipwe kwa kibarua kwa kazi aliyoifanya.

Sasa kwa kuweza kuyabadili mazingira haya, mvuvi naye akawa mdau, ni wakati muafaka sasa wa eneo hili kwamba kuwepo na kipengele pale kiongezwe, kiseme waziwazi kwamba mfuko huu utatoa mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo walioungana pamoja na kusajiliwa kwa lengo la kuendeleza uvuvi.

Mimi naamini kwamba itamsaidia mvuvi mdogo kuweza kuwa na nguvu ya kwenda kuomba pesa katika mfuko huu na vile vile wavuvi wataweza kupata nguvu ya kuungana ili waweze kufanya kazi ipasavyo ya uvuvi, lakini vile vile wapate nguvu ya kujitetea dhidi ya wavuvi wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao maeneo yetu ni pamoja na wavuvi wengi tunapambana na tatizo kubwa la migogoro mikubwa inayoendelea katika maeneo ya uvuvi hasa katika visiwa miongoni mwa wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo. Wavuvi wadogo mara nyingi sana wanapoteza maisha yao, wanapoteza zana zao, wanaishi maisha ya tabu sana na kwa kuwa ndani ya ziwa hakuna amani kabisa. Hii ni kutokana kwamba hawana uwezo wa kifedha wala zana kuweza kujitetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa kazi nzuri hiyo imefanyika mvuvi mdogo mdogo naye atapata tatizo la soko. Kwa sababu wavuvi wetu katika maeneo ambayo wanaishi hakuna masoko, walizoea kuvua kwa sehemu ndogo na wananchi ndiyo walikuwa walaji na hapakuwa na viwanda, sasa baada ya kwamba wavuvi wakubwa wamekuwepo viwanda vipo lakini vyote vipo maeneo ya Mwanza.

Kwa hiyo, yule mvuvi anayevua Gozba ambapo ni karibu masaa 12 ili aweze kufika Makao Makuu ya Wilaya ya Muleba, anayevua Kerebe, anayevua Iroba, Bumbile

na maeneo mengine inampasa akae na samaki wake sio chini ya masaa 10 kabla hajaweza kufika Mwanza palipo na viwanda. Wenzangu wa kule Ukerewe nako wana matatizo yanayofanana na ya kwangu. Kwa sababu maeneo yale nayo hayana viwanda, viwanda vyote vimekaa eneo la Mwanza, jambo hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linaleta matatizo makubwa sana na hali ya mwenzetu huyu mvuvi mdogo kuweza kujikomboa inakuwa ndoto. Kwa ajili ya kuweza kumpa nafasi ya kujikomboa ni vizuri pia katika maeneo yanayovuliwa samaki kukawa na viwanda ili kuweza kuwatunza wale samaki mara wanapovuliwa kwa kuwafanyia taratibu za kuwahifadhi ili wasiharibike lakini pia waweze kupata nafasi ya kuweza kuendelea na uvuvi.

Halafu katika Ziwa Victoria katika eneo langu la Muleba Kaskazini, kuna utaratibu ambao naona wavuvi wakubwa wananunua samaki katikati ya Ziwa. Nafikiri Sheria hairuhusu. Utaratibu unataka lazima wavuvi wote wapeleke samaki wao katika nchi kavu, halafu samaki waweze kununuliwa kule na pia kuna taratibu zingine ambazo zinaendelea pale zinazotawaliwa na Serikali za Mitaa, zikiwepo Shuru za Mialo kwa wale ambao ni wavuvi wakubwa wanatakiwa kulipia. Lakini wanapokuwa katikati ya Ziwa, siyo rahisi. Lakini pia inaweza kuhatarisha maisha ya mvuvi ambaye anakwenda kuuza samaki wake katikati ya Ziwa. Kwa hiyo, nashauri kwamba hili suala ziangaliwe ili wananchi wale ambao wanashughulika na uvuvi waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naamini kwamba Sheria hii sasa itakwenda kuijali lishe ya mwananchi wa kawaida. Baada ya viwanda kuwa vimeanzishwa samaki wote wanapelekwa viwandani. Kwa Sheria hii sasa, itakwenda kusaidia kwamba samaki gani auzwe na samaki gani abaki. Kwa hiyo, kwenye sheria ndogo ndogo hili jambo liangaliwe. Kwa sababu kwa sasa hivi samaki wote wanapelekwa kwenye viwanda.

Kwa hiyo, wananchi wangu wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa sasa hivi afya zimeanza kuzorota kwa sababu hawana mahali pa kupata kitoweo. Kitoweo chao ambacho wamekizoea katika miaka yote ni samaki, kama siyo samaki ni dagaa. Sasa hivi dagaa wanauzwa mbali, samaki wanauzwa kwenye viwanda na mvuvi mdogo haruhusiwi kuvua samaki anayezidi kilo moja wala kuonekana naye.

Kwa hiyo, haya mazingira ninayosema sasa wananchi wanaozunguka ziwa wanaanza kushambuliwa na tatizo kubwa la utapia mlo, akinamama wajawazito, watoto wachanga, wazee na watu wazima ambao wanahitaji lishe. Vijana ambao wanahitaji kupata lishe ipasavyo waweze kuchangia pato la Taifa ipasavyo wanakuwa hawawezi kupata kitoweo ipasavyo. Suala hili na lenyewe lingeangaliwa pamoja na biashara lakini lazima kuwe na kiasi ambacho kinauzwa katika maeneo ambayo wale wananchi wengine ambao wanazunguka katika lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo lingine ambalo hapa limeelezwa nalo ni la kuhusu ulinzi, kwamba kutakuwa na vyombo vitakavyopelekwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani. Nilikuwa naomba watu hao wateuliwe kwa makini sana. Lakini pia

Sheria yenyewe nilipoisoma sikuona kwamba imeweka muda kwamba hawa watu watakuwa katika kazi hiyo kwa muda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazoea yenyewe yana matatizo. Kwa sababu hili ni suala la kamata kamata, una leseni, hauna leseni, wewe umetokea wapi. Suala hilo kama mtu atakaa katika eneo moja akazoea yale mazingira na wale watu, ni suala ambalo na lenyewe litaleta matatizo. Kuwe na muda wawepo pale kwa muda, kisha wabadilishwe. Lengo ni kwamba kusiwe na mazoea ambayo yanaweza yakaleta udhaifu wa kazi.

Lingine ambalo naomba liangaliwe ni lile linalohusu kwamba vyombo vyote vya uvuvi vinavyokuwa katika ziwa ama bahari vitakuwa vinasajiliwa na pia hapatakuwa na mtu anayeruhusiwa kuuza ama kuvua ama kuuza samaki bila kuwa na kibali au leseni.

Nilikuwa naomba suala hili liangaliwe kwa makini lisije likageuka likawa kero. Kwa sababu sheria inaweza ikatamkwa vizuri lakini wale watekelezaji wakawa wasisimamie ipasavyo. Kwa hiyo, badala yake sasa ikageuka ikawa ni kero kwa maana kwamba wanaweza wakawabana sana hawa wavuvi wadogo wadogo ambao wanalengwa wasaidiwe na sheria hii ikawa badala ya kusaidiwa inakuwa ni matatizo.

Naomba sana kama itawezekana kwa pendekezo hili la kuongeza kile kipengele kule kwenye Ibara ya 30 naomba uwekwe msamaha kwa wavuvi wadogo wadogo wanaokaa pamoja wakashirikiana wakaunda umoja wao. Nao wapewe msamaha ule wa miaka mitano kuweza kufanya kazi ya uvuvi bila kuwa wametozwa pesa zozote, wasajili tu vyombo vyao lakini waruhusiwe kufanya uvuvi kwa miaka mitano baada ya hapo waweze kuendelea na hizi shughuli mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri atakuwa anasimamia kuzitolea maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono sana utaratibu wa kuwashughulikia ambao ni wahujumu wa uchumi ikiwemo meli zinazokuja kuvua bila kibali. Katika Ziwa Victoria kuna meli nyingi sana zinazosumbua wavuvi pale katika Ziwa Victoria zinazotoka nchi za jirani. Vile vile tunaungana sisi Watanzania, Waganda na Wakenya. Lakini meli ambazo hazieleweki zinatoka wapi huwa zinavamia lile Ziwa.

Sasa inasemekana kwamba eneo letu la Tanzania ndiyo ambalo bado lina samaki wengi, hasa katika Visiwa hivyo vya Goziba, Kerebe na Makibwa.

Kwa hiyo, ningeshauri sana suala zima la kuhakikisha kwamba walinzi wetu wanapewa zana zinazofaa na wanakuwa kundi la kutosha. Kwa sababu hawa wavamizi wanakuwa wamejiandaa. Vinginevyo watu wetu watakuwa wanavamiwa wanaumizwa katikati ya ziwa ama wanauliwa bila sisi kufahamu. Kwa hiyo, wawe pia na namna ya kuwasiliana na wenzao walioko nchi kavu kuweza kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo.

Lipo lingine ambalo ni tatizo, hawa watu ambao wanaishi katika maeneo haya hawana ulinzi wa kutosha. Mimi katika vifaa vyangu ambavyo ninavyo, takriban 19 hakuna polisi, likitokea tatizo lolote lazima usafiri karibu masaa 10 kwenda kutoa taarifa

na waje kupokea msaada inawezekana ikachukua siku mbili, tatu hata wakati mwingine inachukua wiki.

Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba kuwe na *Police Post* zinazoweza kusaidia ili wananchi waweze kutoa taarifa pale anapopata tatizo, na kushughulikiwa haraka badala ya kuendelea katika tatizo hili kwa kipindi kirefu na badala yake ikaleta kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalopenda kuzungumzia ni elimu. Sheria hii baada kutolewa isiwekwe kwa Hakimu ikangoja kuhukumu wale wanaotenda makosa. Naomba elimu ya kutosha ya sheria hii ipelekwe kwa wananchi waifahamu. Wananchi ndio watasaidia Serikali ili kuweza kulinda zile zana zote ambazo hazifai na kubaini wanaotumia sumu, baruti au mabomu katika uvuvi ambao ni haramu. Wananchi wakishakuwa wanafahamu watasaidia sana Serikali.

Lakini vile vile wavuvi wasingoje kukamatwa kwa sababu wametenda kosa. Wale ambao wote watakuwa wameelimishwa na kufahamu sasa kwamba sehemu ya watu waliopata elimu ni kubwa naamini kabisa wataweza kubadilika wakawa ni wavuvi bora na wakasaidiana na Serikali yetu. Lakini kubwa la msingi ni kuhakikisha wavuvi wanapewa nyenzo na pesa za kuwasaidia wapate mitaji ya kuwasaidia ili waweze kushiriki ipasavyo katika kuboresha uchumi wetu. Samaki wanachangia Pato kubwa la nchi yetu ambalo ukweli wenyewe kama wavuvi wadogo wakishirikishwa ipasavyo Pato hili litakua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada wa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003.

La pili, nipende kutoa salaam za rambirambi kwa wafiwa wote wa ajali mbaya ya gari iliyotokea kule Mkoani Arusha na Kilimanjaro, watu wapatao 26. Hii hasara kubwa sana kwa Taife letu. Natoa pia pole nyingi kwa majeruhi wote wa ajali hii na kumwomba Mwenyezi Mungu aweze kuwapatia marehemu wote pumziko la milele na kuwapoza majeruhi wote wa ajali hii kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nipende kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kututayarishia Muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya raslimali za majini na uchumi wa raslimali za majini katika nchi yetu. Nawapongeza sana kwa kutuletea Muswada huu ambao utaweza kuwasaidia wananchi wetu waweze kuundokana na umaskini wa kipato kwa kuwapatia watu ajira katika eneo la uvuvi na kuwapatia watu chakula kwa njia ya lishe.

Pia niwapongeze kwa kutuletea Muswada huu ambao utatusaidia kuhifadhi raslimali za uvuvi katika maji Kitaifa na Kimataifa na pia kuhifadhi na kulinda mazingira

ya dunia ya samaki katika mabwawa, maziwa na bahari. Nawapongeza sana kwa kutuletea Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu sasa ni kuhusu maudhui ya Muswada huu. Mengi yamesemwa na sisi ambao tunachangia mwishoni mwishoni kiukweli tunakuwa na machache ya kuweza kuchangia katika Muswada. Lakini mimi nimekuwa na maeneo mawili ambayo ningependa kuyachangia katika Muswada huu.

La kwanza ni kuhusu sehemu ya *development of the fishing industry,* maendeleo ya viwanda vya uvuvi katika nchi yetu. Ile sehemu Ibara ya 9(a), (b) na (c) kwanza ili kuweza kuboresha eneo hilo ni muhimu sana tukawaelimisha wafugaji wa samaki. Tumekuwa na mazoea makubwa kwamba ukifika mtoni unapata samaki, kwenye ziwa unapata, kwenye bwawa unapata. Lakini watu wetu bado hawajaweza kuelimishwa na kupewa utaalam wa kuweza kufuga samaki.

Kuna maeneo ambayo hakuna bahari, hakuna mito, halafu hakuna maziwa. Lakini wanaweza wakafuga samaki kama maji yako. Kwa hiyo, watu wangeelimishwa ili huu utaalam uweze kutapakaa nchi nzima sehemu ambapo watu wanaweza kuvuna maji ya mvua na kufuga samaki. Kwa hiyo, ningefikiri, kwa kuwa na hii Sheria tuweze kuelekeza nguvu za Serikali katika yale maendeleo ya uvuvi ili kuwekeza katika hili eneo kwa sababu imetengwa fedha maalum kwa ajili ya hayo maendeleo.

La pili, ni kuendeleza mabwawa yaliyopo. Tulikuwa na mabwawa ya samaki, tulikuwa na maziwa, mengi yana hali mbaya. Ukifika kule Ziwa Victoria kuna matatizo. Ukienda katika bwawa la samaki kama la Nyumba ya Mungu kuna matatizo. Sasa itakuwa ni wakati mzuri sasa hivi kuweza kuendeleza hayo mabwawa. Mengi tokea yamejengwa mpaka sasa hivi hayajapata huduma. Kwa sababu ya sheria hii kuweka nafasi ya mfuko wa kuweza kutoa hiyo huduma ningeomba sana Mheshimiwa Waziri akaangalie kwa makini jinsi atakavyoweza kuendeleza na pia kufufua mabwawa ambayo mengi yake yatakuwa aidha yamekufa na yanahitaji kufufuliwa au kukarabatiwa.

Kwa mfano, kule kwetu kuna Bwawa hili la Nyumba ya Mungu, lina matatizo ya *silt,* lina matatizo ya upungufu wa maji. Hili bwawa linapata maji kutoka Mto Pangani na Mto Kikuletwa na kwa sababu mazingira ya Mto Pangani yanaharibiwa sana na mazingira ya huo Mto Kikuletwa.

Kwa hiyo, hili Bwawa la Nyumba ya Mungu mara nyingi linakuwa halina kina cha maji ya kutosha. Kwa hiyo, uvuvi wa samaki unakuwa hafifu. Uzalishaji wa samaki kule kwetu umeshuka mno maana yake ni kwamba wavuvi wameathirika.Kwa hiyo, lile bwawa lingeangaliwa kwa njia hiyo ya kukarabatiwa na vile vile kulinda mazingira ya mito hiyo niliyoitaja ili kuweza kuboresha kina cha maji si kwa ajili tu ya kuzalisha umeme. Lakini pamoja na mahitaji ya uvuvi kwa ajili ya samaki. Kuna mabwawa mengine ambayo yamekufa kabisa.

Kwa mfano, tuna Bwawa la Chato, mara nyingi naliongelea hapa, lile bwawa lilikuwa linazalisha samaki wengi sana pamoja na bwawa la Dindira.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri baada ya sheria hii kutoka na kuwa na huu mfuko hayo mabwawa yaweze kufufuliwa. Tuna Ziwa la Jipe na Ziwa la Chala. Haya ni maziwa madogo madogo. Lakini yamekuwa yakichangia uchumi mkubwa wa maeneo yetu kwa ajira ya uvuvi.

Kwa hiyo, tungeomba na haya yaangaliwe na namshukuru Waziri kwa sababu ameshawahi kupanga ziara akatembelea Ziwa Jipe na akaona ni jinsi gani atakavyosaidia. Nina imani baada ya kufika Ziwa Jipe, malengo yatakuwa yamewekwa ya kuboresha hili Ziwa na bila shaka uchumi wa watu pale utakuwa umeweza kukua.

Sehemu zingine ambazo zinahitaji mabwawa. Kwa sababu sasa hivi dunia inaanza kupata matatizo ya upungufu wa maji na huwezi ukaongea habari ya samaki bila maji. Ukitaka kupata samaki lazima uongee maji, maana maisha ya samaki ni ndani ya maji. Sasa vyanzo vya maji vinapungua sana duniani kote na wataalam wanatuambia kwamba hivi vyanzo vinapungua kwa kasi kubwa sana kiasi kwamba kama hatua za makusudi hazitachukuliwa hata maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu yatakuwa shida, licha ya hayo ya samaki.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Wizara iwe makini sana kuanza kufikiria kuanzisha miradi ya kuvuna maji ya mvua, hasa sehemu ambazo ina raslimali ya milima kama kule kwetu. Milima inaweka kingo nzuri za kuweza kuhifadhia maji ya mvua na kama hakuna *seepage* yale maji yakaweza kukaa katika msimu mmoja wa mvua mpaka mwingine na kwa njia hiyo wakapanda samaki. Samaki ambao watasaidia kwa chakula, kuondokana na umaskini wa chakula pamoja na umaskini wa ajira.

Kuna nchi ambayo imefaidi sana kwa kuvuna maji ya mvua kama kule Zimbabwe, mji wa Bulawayo wanavuna maji ya mvua, wana mabwawa makubwa mengi, wamevuna maji ya mvua na wanaendesha utalii na uvuvi katika hayo mabwawa na wanaendesha pia kilimo na misitu kuzunguka hayo mabwawa.

Kwa hiyo, mazingira yanakuwa yanahifadhiwa vizuri. Vyanzo vya maji vinahifadhiwa vizuri kwa kuweza kuvuna maji ya mvua. Kwa hiyo, nafikiri katika eneo hilo Mheshimiwa Waziri aangalie sana kuhakikisha kwamba sehemu ambazo uwezekano wa kuvuna maji ya mvua kwa kutumia *topography* ya asili ya nchi yetu zitumike vizuri.

Sehemu ya pili ya Muswada huu ambao ningependa kuchangia ni katika *management* na *control* ya *fishing industry.* Uharibifu wa mazingira utatufikisha kubaya. Kwa hiyo, tunapoongelea suala hili la kukuza viwanda vyetu vya samaki, vile vile tuangalie uharibifu wa mazingira. Huu uharibifu wa mazingira unapunguza maji kama kule kwetu ambavyo nimeeleza ambavyo tumeathirika, vina vya maji vimepungua katika bwawa la Nyumba ya Mungu na mabwawa mengine kama Kalemawe.

Tunaomba vile vyanzo vya maji vilindwe kama hakuna Sheria inayoweza ku-*address* mazingira haya ya vyanzo vya maji, Sheria itafutwe na iboreshwe ili kuhakikisha kwamba vina vya maji vinalindwa.

Sehemu nyingine ni kuhusu *silt* (tope), mabwawa mengi, maziwa mengi yamekuwa na matope kiasi ambacho yanahitaji kufanyiwa huduma. Lingine ni kuhusu wavuvi wetu kukosa mitaji. Sasa kwa sababu tumekuwa na huu mfuko nina imani wavuvi watapatiwa mitaji. Lakini nafikiri kuwapatia mitaji peke yake haitoshi. Itakuwa muhimu sana kuanza kuwaelimisha, kuwapatia elimu na teknolojia ya kuwawezesha kufanya kazi yao ya uvuvi kwa maslahi mazuri na tija kubwa. Kitu hiki kingefanyika kitaweza kupandisha pato lao lakini wakipewa tu mitaji watafikia mahali ambapo mitaji hiyo haitalipa.

Siku hizi hakuna mitaji inatolewa kama sadaka Kanisani au Msikitini, fedha nyingi zinatolewa kwa njia ya mikopo midogo midogo au mikubwa mikubwa. Sasa kabla ya kutoa hiyo mikopo wapewe elimu nzuri na wapewe elimu ya ufundi kuhusu kazi yao wanayofanya kwa sababu kazi ya uvuvi ni kazi ya ufundi, wasiifanye kienyeji ili isije ikawa wanakwenda kuvua kuanzia asubuhi mpaka jioni na kurudi tupu.

Sehemu nyingine ya kuwasaidia wavuvi hawa ni kuhusu *storage.* Samaki wakishavuliwa hawawezi kukaa muda mrefu sana na *storage* kwetu imekuwa shida sana katika nchi yetu. Utakuta sehemu nyingi samaki wamevunwa halafu wameharibika na wametupwa. Sasa kama *storage* itafanyika na vile vile kusindika samaki, wakati mwingine tunasema kwamba kuna njaa, lakini pale ambapo samaki wanavunwa lazima wasindikwe, wakahifadhiwe, wakaweze kutumika wakati ambapo labda mavuno ya samaki ni kidogo. Wavuvi wetu hawa wafundishwe njia za kuhifadhi samaki waweze kukaa kipindi kimoja hadi kingine na kuweza kupelekwa maeneo ambayo labda hakuna samaki.

Lingine ni kuhusu masoko. Wavuvi wakati mwingine wanabaki na mavuno yao ya samaki yakaharibika kwa kukosa soko. Kwa hiyo, tungeomba vile vile Wizara ikaangalia kwamba hawa wavuvi wanasaidiwa katika kupatiwa masoko kwa kushirikiana na Wizara ambayo itakuwa inahusika.

Sasa baada ya kusema hayo, niombe tena Wizara iweze kuwasaidia watu wetu kwa sababu wavuvi wetu wako mmoja mmoja na ni dhaifu. Ili kuwapa nguvu lazima kuwaunganisha katika vyama vya ushirika. Ushirika mdogo mdogo kuwawezesha kuunganisha nguvu zao ili kuweza kuendesha biashara yao na uzalishaji wao wa samaki kwa nguvu zaidi. Wakiwa mmoja mmoja hawatafaulu lakini wakiwa wanashirikiana kwa vikundi vya watu watano watano, wavuvi sita sita au kumi basi wakipata na misaada ya fedha wataweza kufaulu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa napenda nichukue nafasi ya mwisho tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kutuletea Muswada huu na naunga hoja Muswada wa Sheria hii ya Uvuvi wa mwaka 2003 asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia Muswada huu wa *Fisheries Act* mwaka 2003.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji pamoja na Wataalam Waandamizi wa Wizara yake kwa kututayarishia Muswada huu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kuwasilisha Muswada huu kwa uzuri sana na kuufanya tuuelewe kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baada ya wenzangu kuongea na kwa kuwa mimi ni msemaji wa mwisho nitalenga zaidi matatizo ya uvuvi katika Jimbo langu la uchaguzi. Katika jimbo langu la uchaguzi kuna Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo namshukuru sana Mheshimiwa John Singo kwa kulielezea matatizo yake na mimi nitazingatia zaidi uvivu haramu ambao unaendelea katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu nimelileta hapa Bungeni mara nyingi na naishukuru sana Serikali kwa hatua ambazo imechukua za awali katika kupambana na uvuvi haramu katika bwawa hilo.

Napenda hasa hasa nimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa hilo, Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Wakuu wa Polisi wa Mikoa hiyo kwa kazi nzuri ambayo walifanya katika hatua ya kwanza ya kudhibiti uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Wananchi wa Wilaya za Mwanga, Simanjiro na Moshi wamefurahia matokeo ya kudhibiti uvuvi haramu hasa wa kutumia Makokoro, Vimila na Chandarua katika bwawa hilo. Lakini bado wako wakorofi wachache na ambao sasa wanasema kwamba nguvu za Serikali ni nguvu za soda. Kwa sababu baada ya operesheni ile kufanyika wamerudi tena wanavua na makokoro, vimila na chandarua katika vijiji vya Kagongo, Nyabinda na vijiji vingi kule Simanjiro bila kudhibitiwa tena kama ilivyofanyika kwenye operesheni.

Kwa hiyo, ningependa Serikali itoe tamko rasmi hapa, kwamba kuzuia uvuvi haramu katika bwawa hilo Serikali haina nguvu ya soda na kwamba Serikali ina dhamira thabiti kabisa za kukomesha uvuvi haramu katika Bwawa hilo.

Katika maeneo ambako baada ya operesheni wananchi wamezingatia maelekezo ya Serikali na baada ya miezi mitatu tu ya kufanya operesheni hiyo, samaki tena wamerudi, wanakuwa wakubwa kama walivyokuwa zamani na biashara nzuri ya samaki sasa inawezekana.

Kwa hiyo, ingekuwa vizuri Serikali ikatoa rasmi tamko la kuwaeleza wananchi kwamba inapofanya operesheni hii haifanyi udhibiti wa uvuvi haramu kama soda inavyofunguliwa na nguvu halafu nguvu ile iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niupongeze Muswada huu kwa kuelezea katika sehemu ya 17 (g) kwamba inapendekeza kufunga uvuvi katika maeneo fulani fulani katika sehemu za mwaka ili kuhakikisha kwamba *populations* za samaki zinarudia katika hali yake. Ningependa nitoe pendekezo hapa rasmi kabisa kwamba kufunga uvuvi katika maziwa hasa *inland water bodies* iwe ni kitu cha kudumu katika wakati au katika msimu samaki wanazaliana. Huu ni utaratibu ambao unafanywa katika nchi mbalimbali na ni utaratibu ambao unahakikisha kwamba *ecosystems,* zinarudi katika hali yake na zinaweza kuwa *managed in perpetuity* yaani vinaweza kuendelezwa, zinaweza kuwa endelevu. Bila kufunga uvuvi wakati samaki wanapozaliana hakuna uhakika wowote wa kuhakikisha kwamba samaki watakuwepo wakati wote na sisi tutaweza kuwapa vizazi vijavyo maliasili ambazo tumepewa na baba zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu katika hili ni kuwa Wizara iangalie wafanyakazi hawa wanaosimamia mabwawa na maziwa haya madogo madogo ya ndani, kama Bwawa la Nyumba ya Mungu, Maofisa wa Uvuvi walioko Bwawa la Nyumba ya Mungu, wote wamekaa pale zaidi ya miaka 20, wanasimamia pale zaidi ya miaka 20. Kwa hiyo, hata hao Maofisa Uvuvi nao wana makokoro, nao wana vimila.

Kwa hiyo, wamekuwa wanavijiji kabisa na wavuvi haramu wao wenyewe. Kwa hiyo, hawawezi kabisa kusimamia uvuvi haramu. Serikali iangalie utaratibu wa kubadilisha maofisa hawa waende katika maeneo mengine watuletee wafanyakazi wengine badala ya kuwageuza wafanyakazi wawe wanavijiji na wawe wanatumia ziwa hilo kama eneo lao la kufanya rushwa na wenyewe wajiingize katika uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, katika hili ningependekeza tuanze mjadala wa Kitaifa wa jinsi gani sasa tutumie maji. Kwa sasa kipaumbele cha kwanza cha kutumia maji ni kuzalisha umeme lakini maji ndiyo hayo hayo tuna kunywa, maji ndiyo hayo hayo tunahitaji kwa ajili ya umwagiliaji na pia maji ndiyo hayo hayo tunahitaji kwa matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa tuanze kufikiria kuzalisha umeme kutoka kwenye makaa ya mawe, kutoka kwenye gesi, kutoka kwenye *sources* kama *geothermal,* kutoka kwenye *solar* na kutoka kwenye mafuta ili maji yabaki ni ya kunywa, kutuzalishia samaki na ya kumwagilia mashamba. Kama hatukuweza kubadilisha mfumo mzima wa jinsi gani tunafikiria kutumia maji yetu haya yaliyoko Tanzania, kwa wakati ujao tutafika mahali tutashindwa tufanye nini maana tutakosa samaki, tutakosa maji ya umwagiliaji na hata maji ya kunywa tutakosa.

Kwa hiyo, ni vema tuanze kufikiria sasa kuzalisha umeme kwa njia ambazo ni za uhakika zaidi na Mwenyezi Mungu ametupa makaa ya mawe mengi, ametupa gesi nyingi, tunalo bonde la ufa kubwa sana ambapo chini yake kuna *geothermal sources* kubwa sana na kubwa zaidi labda ya nchi zote za Kiafrika ambayo tungeweza kuzalisha umeme mwingi na wa kutosha. Nchi jirani ya Kenya tayari inazalisha robo ya umeme wake kutoka kwenye *geothermal sources* ambazo ziko kwenye bonde la ufa. Kwa hiyo, tungefikiria sasa badala ya kungoja mpaka kesho na kesho kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunaelewa kwamba kutegemea maji kuzalisha umeme, tunajiingiza kwenye utaratibu wa migao kwa sababu pindi inapotokea kiangazi kirefu basi maji hayatoshi na umeme hautoshi. Kwa hiyo, wakati umefika sasa tuondokane kabisa na mambo ya kufikiria kwamba tunaweza kuzalisha umeme kutokana na maji peke yake. Hata ikibidi kwa nini tusifikirie kuzalisha umeme kutokana na *nuclear energy?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kuongelea kidogo kuhusu Ziwa la Jipe. Napenda ninapoongelea juu ya Ziwa la Jipe, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuzingatia tatizo kubwa lililoko kule la magugu yanayoliua Ziwa la Jipe.

Napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa kulitembelea Ziwa la Jipe. Napenda pia niishukuru Kamati ya Bunge ya Afrika ya Mashariki iliyoongozwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, kwa kulitembelea Ziwa la Jipe kuangalia matatizo ya magugu yaliyoko katika eneo lile. Naomba juhudi ambazo zimeanzwa na Ofisi ya Makamu Rais, Mazingira, ziongezwe ili tatizo la magugu katika Ziwa la Jipe liweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya tisa ya Muswada huu kuna pendekezo (k) pale linalosema ya kwamba Mkurugenzi atafanya *regional and international collaboration in the sustainable utilization, management and conservation of resources in shared water bodies.*

Napenda niliambie Bunge lako Tukufu kwamba wenzetu wa jirani wamefunga Mto Chala unaotokea Mlima Kilimanjaro katika Wilaya ya Rombo na kuingia Ziwa la Jipe kupitia Ziwa ndogo la Chala, wakaufunga mto huo na kuupeleka kwenye mashamba. Kwa hiyo, mto huo sasa hauingii katika Ziwa la Jipe na kwa sababu hiyo Ziwa la Jipe linakauka. Kwa sababu kuna makubaliano ya Kimataifa kwamba huwezi kuzuia mto ambao unatumika na nchi nyingine, ukautumia wewe mwenyewe, ninaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, iwasiliane na jirani zetu wa Kenya ili kuhakikisha ya kwamba Mto Chala unaingia katika Ziwa la Jipe na kwamba suala hili linatatuliwa mapema iwezekanavyo kabla Ziwa la Jipe halijakauka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninapenda nikuhakikishie ya kwamba na mimi ninaunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhimitisha mjadala wa hoja katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia katika Muswada ama kwa kusema humu Bungeni au kwa maandishi. Nawashukuru sana kwa sababu wote wameunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kama ilivyo kawaida yetu nianze kuwatambua kwa kuwataja kwa majina. Nitaanza na wale waliochangia kwa kusema humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumtambua Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na namshukuru sana kwa kuunga mkono hoja hii kwa sababu nadhani tulipoanza mfumo huu wa Vyama Vingi vya Siasa pengine pale mwanzoni tulikuwa tunadhani na baadhi yetu walikuwa wanafikiri ukiwa upande wa Upinzani basi ni kupinga kila kitu, wala sio lengo la mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Kwa hiyo, napenda kumpongeza sana kwa hili kwa sababu huku ndiko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi niwashukuru Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, hawa walipata nafasi ya kuzungumza humu ukumbini. Kama kuna niliyemsahau katika hili lakini bila shaka tutakuwa tumeorodhesha kile alichokichangia na tutautumia mchango wake katika kutekeleza Sheria hii pindi Waheshimiwa Wabunge watakapopitisha Muswada na kuwa Sheria ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwatambue na kuwashukuru waliochangia kwa maandishi nikianza na Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Remidius Kissasssi, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Esha Stima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari Waheshimiwa Wabunge wametoa michango muhimu sana na Wizara itahakikisha kuwa michango yao inazingatiwa katika utekelezaji wa Muswada wa Sheria. Mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge yatazingatiwa katika kanuni za utekelezaji wa Sheria ambazo Sheria ikiishapitishwa inampa mamlaka Mheshimiwa Waziri kutunga kanuni ili kutekeleza kwa makini na ufanisi matokeo ya Muswada huu ambao ndiyo Sheria ya Uvuvi. Nilitaka niseme hivyo kwa utangulizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakiri kwamba upo muda lakini siku zote muda hautoshi, Waingereza wanasema, *time is a scarce commodity.* Kwa hiyo, kwa kweli naomba nitangulie kwa kusema ya kwamba haitawezekana kuzungumzia kila ambalo Mheshimiwa Mbunge amechangia katika hoja ya Muswada huu lakini yapo maeneo

ambayo unaweza ukasema ingawa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamechangia na kwa muda tofauti lakini unakuta kimsingi maeneo haya yanashabihiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze na eneo moja ambalo nadhani ni la msingi na kwa sababu katika Muswada huu eneo hili ni jipya. Upya wake unaweza ukaupata katika hotuba na ninaomba Waheshimiwa Wabunge ambao si Wajumbe wala wanachama wa Chama cha Mapinduzi wasijisikie vibaya, ninaporejea kwenye msingi wa Muswada huu ambao ni ile Ilani ya Chama cha Mapinduzi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2000 pale ambapo Chama kilielekeza kwamba hiyo Serikali itakayopatikana baada ya wananchi kukipa Chama ridhaa, sasa hiyo Serikali kwa manufaa ya Watanzania wote ifanye nini? Ilani ilielekeza kama ifuatavyo:-

Nitapenda ninukuu: "Kama ambavyo wengi wenu mnafahamu Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000 inatamka wazi kwamba katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2005 Serikali za CCM zitaendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna kwa busara raslimali za maliasili kwa manufaa ya Taifa letu. Suala la uvuvi ni suala la kuvuna raslimali ya majini na ni kwa manufaa ya Taifa letu, manufaa yanayotokana na uvuvi kama ilivyo katika madhumuni ya Muswada huu, huwezi ukasema inaelekea kukidhi mahitaji na matakwa ya chama fulani cha siasa, unaweza ukalisema hilo kama labda ni siasa lakini ukweli hauko nawe kwa sababu tunalenga maslahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa moja ambalo limo katika Muswada huu na ni jipya na limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kadhaa katika wale waliochangia ningependa nianze nalo, ni lile lililo katika Ibara au kifungu cha 29, pale inapozungumziwa juu ya Mfuko wa kuendeleza uvuvi na matumizi ya fedha katika Mfuko huu. Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamesema inavyosomeka na hasa ukienda pale kwenye ukurasa wa 32 walio na nakala ya Muswada, ukaenda ukurasa wa 33 sehemu ya (b), Waheshimiwa Wabunge kadhaa kama Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Ruth Msafiri, wamesema, hivi huyu mvuvi mdogo mdogo, *fisher man or fisher woman* pamoja na kwamba jambo hili ni jipya na ni jema lakini suala ambalo tunalizungumzia wakati wote la mikopo na nini, limezingatiwa vipi ili umvushe huyu mvuvi mdogo mdogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukisoma pale (b) inaposema: *"The objects and purposes of the Fund are (b) To promote and assist in the development of community management units by giving grants and assisting groups or persons wishing to form fisheries conservation and protection groups."*

Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wamesema twende zaidi tuseme, unapolenga hapa baadaye basi kwa sababu katika taaluma ya Sheria huwezi ukaweka kila kitu katika Sheria na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri anapewa mamlaka ya kutunga kanuni, litakalozingatiwa hapa katika kanuni kwa sababu ni kweli tunaona ya kwamba ni takwa la jamii na Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kwa nguvu, kwa kiingereza wanasema, *felt need,* katika kanuni nina hakika eneo hili litaendelezwa na suala la mikopo ili kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo liweze kuzingatiwa katika utekelezaji.

Kwa hiyo, ningependa niliseme hili na pengine niongezee jambo lingine ambalo limesemwa katika eneo hili kwamba ni kweli ni jambo jema unapozungumzia kuwawezesha wananchi na kuelekeza mikopo kwao lakini tusiimbe tu suala la mikopo ila lazima pia na elimu, mikopo ile itumike vipi ili mikopo ile na shughuli nzima iweze kuwa endelevu.

Kwa hiyo, mimi nilitaka nilisema hili kwa sababu ni jipya lakini pia limeongezewa ubora, limeboreshwa na michango ya Waheshimiwa Wabunge na ninaamini katika kanuni za kutekeleza Sheria hii litazingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nije kwenye eneo ambalo katika ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ambalo kwa kweli ni kwa niaba ya Kamati nzima, Kamati ambayo kwa bahati nzuri Wizara hii inafanya kazi kwa karibu sana na Wajumbe wa Kamati hii ikiwa ni pamoja na kupeana elimu.

Nashukuru kwamba hata sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunafanya kazi kwa karibu sana na Kamati hii ya Maliasili na Mazingira na limekwishatolewa hata pendekezo kwamba katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunajishughulisha pia na masuala ya Muungano na pengine ni vizuri hata jina la Kamati likaonyesha kwamba linajihusisha na masuala ya Muungano. Nilitaka niseme tu kwa muhtasari kwamba mapendekezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, haya ni miongoni mwa yale ambayo yatafanyiwa kazi katika kufanikisha utekelezaji wa Sheria itakayotokana na Muswada huu.

Kama nilivyosema muda mchache uliopita, Wizara yangu kwa maana ya Waziri ninayemwakilisha hapa, Wizara ya Maliasili na Utalii, inafanya kazi kwa karibu sana na Kamati hii na ushauri wao daima huzingatiwa katika kutekeleza majukumu na wajibu wetu. Kwa hiyo, ningependa niseme tu kwamba yale mapendekezo ambayo yamelenga kuboresha Muswada na utekelezaji wa Sheria itakayotokana na Muswada huu, yatazingatiwa katika utekelezaji ili kuifanya Sheria iwe bora na itutumikie Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nijaribu kuona ni maeneo gani ambayo kila mmoja kwa kifupi sana alikuwa ameyazungumzia. Kwa mfano, Mheshimiwa Hashim Saggaf, katika mchango wake kidogo alikuwa amezungumzia suala ambalo linahusiana na uvuvi katika bahari kuu, *deep sea.*

Naomba niseme tu ya kwamba Muswada ulio mbele yetu unajihusisha na uvuvi katika maeneo yanayoitwa *inland waters* na si uvuvi katika bahari kuu. Mheshimiwa mmoja katika kuchangia alisema, hii raslimali ya majini haijui mipaka na si ya maji katika *inland waters* au *deep sea* lakini pia hata kama mna mipaka ya nchi na nchi, raslimali ya majini haijui mipaka, hiyo mipaka tunaitambua sisi katika kuendesha mambo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni vizuri tunapokuwa tunazungumzia Miswada ili tujielekeze ipasavyo, tusichanganye Muswada wa uvuvi katika bahari kuu na Muswada katika uvuvi wa maeneo haya ambayo ni maeneo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, ni kweli kuna ushauri aliokuwa ameutoa, ule unaohusu uvuvi katika bahari kuu kwa namna fulani ilikuwa kidogo ni nje ya Muswada ulio mbele yetu lakini ushauri wake nina hakika katika kuzingatia na kutekeleza Sheria ya uvuvi katika bahari kuu, utazingatiwa pia maana ni suala la kuboresha kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko moja ambalo alilisema na pengine labda *with a light touch* kwamba Waheshimiwa Mawaziri wote wanakaa *Oysterbay,* sasa yale mabomu yanapolipuka kwa wale wanaovua kwa kutumia mabomu, wanasikia kwa kuwa wako kule *Oysterbay* karibu na bahari. Vema, lakini naamini si Waheshimiwa Mawaziri wote, bahati nzuri mimi nimezaliwa Kijijini na ninapenda mazingira ya Kijijini, binafsi nakaa sehemu inayoitwa Kimara Temboni na kunafanana na Kijijini kwangu kuliko *Oysterbay.* Kwa hiyo, nilitaka nilisema hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna moja alilolisema Mheshimiwa Hashim Saggaf, kuhusu suala la *International Maritime Organization,* Shirika la Umoja wa Mataifa la masuala ya bahari, akaihusisha na Muswada huu unaosema Sheria hii itatumika Tanzania Bara na si Tanzania Zanzibar. Ni kweli Sheria inasema hivyo lakini ninalotaka kulisema hapa ni kwamba, Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na katika masuala ya Kimataifa na manufaa yanayotokana na uanachama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mashirika haya ya Kimataifa, Zanzibar ina sehemu yake kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, ingawa Sheria hii au Muswada huu hauhusiki na Sheria haitatumika Zanzibar kwa sababu dhahiri suala la uvuvi si suala la Muungano lakini manufaa yanayotokana na uanachama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika *International Maritime Organization* kwa vyovyote vile Zanzibar haiwezi ikawekwa pembeni. Nilitaka nilisema hilo.

Pngine niruhusu kwamba nikiwa katika eneo hili niliunganishe na kitu kimoja ambacho ni jambo la msingi katika suala la kutunga Sheria, tunatunga Sheria kwa mujibu wa katiba ya nchi. Sasa ukiisoma Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nina nakala hapa mbele yangu, kwa idhini yako Mheshimiwa Naibu Spika naomba niisome, Ibara ya 64(2) inasema hivi: “Mamlaka yote ya kutunga Sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano” na suala la uvuvi si suala la Muungano, “yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.”

Ibara ndogo ya tatu inasema: “Endapo Sheria yoyote, sasa hii inazungumzia upande wa Baraza la Wawakilishi lakini niizungumzie inayohusu Bunge la Jamhuri ya Muungano, endapo Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, Sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka.”

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Bunge lako Tukufu haliwezi likasema liitungie Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Sheria ambayo haihusiani na masuala ya Muungano kama suala hili tunapozungumzia suala la uvuvi. Kwa hiyo, katika yale yaliyokuwa yamesemwa nilitaka tu turejee katika msingi wa katiba ya kwamba tunafanya hivyo kwa kutekeleza katiba ya nchi yetu na si kwa sababu nyingine yoyote. Ndiyo maana sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunajali sana na kuzingatia ushirikiano katika masuala ambayo yana maslahi kwa watu wetu wote kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hata kama hayahusiani na wala si masuala ya Muungano ndiyo maana unakuta kwa kiswahili cha Zanzibar ni kwamba, tuna mashirikiano katika maeneo haya ambayo si ya Muungano kwa sababu tunajua yana manufaa kwa watu wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura ametoa mchango mzuri sana na hasa suala la Muswada kujielekeza katika mambo mazuri tu mapya kwa mfano Muswada huu umetambua, unaposema juu ya suala la kufuata Sheria na unazungumzia uwazi. Kunapokuwa na *conflict of interest,* mgongano wa maslahi, ni vizuri ikatamkwa hivyo na Sheria ikalisema wazi wazi kwamba inapotokea hivyo, lengo ni kwamba ukiona kuna mgongano wa maslahi jiweke pembeni, alichouliza tu ni kwamba, sasa kama anayehusika hatafanya hivyo tunafanyaje? Ndiyo tunaanza, tukigundua ya kwamba lipo tatizo hilo tutakwenda hatua zaidi. Lakini nilidhani ni mwanzo mzuri na tunatarajia watumishi wawe waadilifu na kufuata misingi ya utumishi kwa umma na sio kujitumikia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna eneo lile katika kifungu cha nane, sehemu ya kwanza, pale inapohusu *best endeavors* kwamba katika kufanya maamuzi basi atumie lile ambalo kibinadamu umechukua kila tahadhari, hakuna upendeleo wala hakuna uwoga, ndiyo ninavyoielewa kwa maana ya *best endeavors* kwamba pamoja na ubinadamu wetu lakini mahali pa kazi unajitahidi kutimiza wajibu wako ukiweka pembeni maeneo ya upendeleo na masuala mengine haya yasiyofaa kama rushwa na vitu vya namna hiyo.

Kwa hiyo, najua alisema kwa sababu sisi wengine katika maeneo fulani fulani tunaitwa *learned friends or learned brothers* kwamba pengine tulitolee ufafanuzi. Ile *best endeavors* ni kwamba unafanya linalowezekana ukitambua ya kwamba sisi ni binadamu na hayuko binadamu mkamilifu isipokuwa pia makosa ya makusudi ili upindishe linalotakiwa, yanakuwa yameepukwa ndiyo maana ya *best endeavors.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumzia maslahi ya watumishi kwamba ni vizuri kwa sababu Sheria hii inalenga katika kusimamia raslimali muhimu sana na kuna Mheshimiwa Mbunge amelisema vizuri sana kwamba raslimali hii ni moja kati ya raslimali zinazotusaidia katika mapambano dhidi ya umaskini, sasa watumishi katika eneo hili ni muhimu pia tuseme wapo lakini lazima ujiulize hawa watumishi wapo namna gani kwa maana ya kwamba maslahi yao, vitendea kazi na mishahara ili kusudi kama sisi wengine tunaomwomba Mwenyezi Mungu siku za Jumapili, Wakristo, iko sala moja tunamwomba Mwenyezi Mungu kwamba, usitutie katika vishawishi, sasa wewe watumishi hawa wanaotusaidia katika eneo hili mojawapo muhimu katika kupambana na

umaskini, kwa nini mishahara yao unaiweka kwa jinsi ambavyo unawatia katika vishawishi? Nadhani ndiyo alikuwa anatukumbusha hapa. Namshukuru sana kwa mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu kwa walengwa nalo limezungumziwa na wachangiaji kwa kweli wengi kati ya wale niliowataja. Naomba niseme tu kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa watakumbuka Ofisi ya Makamu wa Rais imewahi kuwashirikisha katika uzinduzi wa mkakati wa utekelezaji wa kitu kinachoitwa *Cost and Marine Environment Management Project* ambapo tunashirikisha Serikali za Mitaa na wavuvi wadogo wadogo katika maeneo yote haya.

Katika Ofisi ya Makamu wa Rais, suala zima hili la Hifadhi ya Mazingira ya Bahari na Pwani, tunalifanya kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba, katika nchi yetu robo ya idadi ya Watanzania wote wanakaa katika maeneo haya, unaweza kuita maeneo ya Bahari na Pwani na shughuli zao mtu mmoja mmoja kujitafutia riziki au vikundi kujitafutia maendeleo hutegemea raslimali zilizoko katika maeneo haya. Hivi sasa tunajaribu hata kusema tafsiri ya *coastal and marine* isibakie kwenye Bahari tu lakini hata Maziwa na Mito mikubwa ihusishwe kwa sababu tunacholenga ni ile raslimali ya kusaidia wananchi wetu kupambana na umaskini. Wazo hili tumelifikisha kwa wale tunaoshirikiana nao katika sehemu ya Benki ya Dunia wanaoshughulika na suala la *Coastal And Marine Environment Management* na inaelekea tutafanikiwa kujenga hoja hiyo kwa sababu lengo letu kuu ni kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi ule ambao tuliwashirikisha baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Mbunge wa Mafia, sikumbuki kama Mheshimiwa Mbunge wa Pangani alibahatika kuhudhuria, lakini pia tulikuwa na Waheshimiwa Wabunge kutoka Lindi na Mtwara. Mradi ule kwa suala la elimu umepiga hatua kwa sababu wavuvi wamefika mahali ambapo wanasema anayevua kwa kutumia sumu au baruti ni adui wa wavuvi walio wengi kwa sababu anaharibu mazalio ya samaki na anaharibu raslimali yenyewe. Ukienda upande wa Ziwa Victoria kule suala hili limeeleweka vizuri zaidi kwa mradi ule wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, kile kilichofafanuliwa katika Muswada, *Beach Management Unit,* vikundi hivi wamefika mahali mvuvi akivua kwa kutumia sumu au baruti, akifikisha samaki katika eneo lile *(landing site),* ambalo katika Ziwa Victoria linajulikana zaidi kama mwalo, huyu mvuvi akifikisha samaki mwaloni basi kajipeleka Polisi anakamatwa na vikundi vile na wanachomwambia ni kwamba, unachokifanya wewe unaharibu raslimali yetu lakini pia unavuruga uchumi wa nchi kwa sababu hatuwezi kuendelea kuuza minofu ya samaki nchi za nje kwa sababu inafika mahali wanasema samaki wote wanavuliwa kwa mtindo wa ovyo ovyo, kwa kutumia sumu na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, hili ambalo nilikuwa nataka nilihusishe na suala zima la elimu kwa walengwa, kwa kweli kuna mahali tumepiga hatua na naomba kwa Muswada huu ambao unaanzisha na Mfuko, tuliendeleze vizuri zaidi na tuweze kuwa watumishi bora wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri niyaseme haya na nimpongeze sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa sababu kwa kule anakotoka suala la uvuvi na raslimali ya samaki neno la Kiingereza *livelihood,* nina hakika analielewa vizuri zaidi

kwa sababu bila raslimali ya samaki, sidhani kama maisha ya mwana Ukerewe atayaona yana maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kama Muswada unavyosema na niruhusu nisome sehemu ile ya *objects* kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu nadhani unapata ile *scheme* ya Muswada vizuri zaidi pale inaposema: *"The object of this Bill is to enact legislation pertaining to the sustainable development"*, uendelezaji endelevu, *protection* (kulinda), *conservation* (kuhifadhi) *aquaculture*, suala la ufugaji wa samaki, hapa maneno yaliyotumika ni ya Kilatini *aqua* kwa Kilatini ni maji, *cultura* ni desturi sasa desturi ya majini ni kuvua samaki na hata kilimo cha mwani nadhani unaweza kusema ile ni *maricultura*, *mari* ni bahari sasa kilimo cha baharini ni *mari-culture* kwa Kiingereza lakini Kilatini ungesema *maricultura.* Halafu kuna *aquaculture development,* kuna Mheshimiwa Mbunge alilihusisha na suala la utalii lakini kama mtakavyoona, Muswada unasema itafika mahali shughuli za uvuvi zifungwe kwa kipindi.

Napenda kuwashukuru wasanii sijui ni kundi gani liliimba wimbo mmoja wa taarabu unaosema: “Kama mvuvi wa pweza tutaonana mwambani”. Ni kwamba, kuna vipindi lazima usitishe shughuli za kuvua ili uwaruhusu samaki kuzaliana na kama inavyofanyika kuna kipindi katika uwindaji wa kitalii tunasema wawindaji wa kitalii wasiende kuwinda. Sasa unapozungumzia juu ya vipindi hivi kama samaki wanahitajika, *aquaculture,* ufugaji wa samaki katika shamba lako utajua wewe wale samaki watavunwa lini, hutahusika na kipindi hiki ambacho uvuvi wa samaki utakuwa umesitishwa. Ndio lengo la *aquaculture.* Inawezekana ikawa ni sehemu ya utalii lakini nadhani zaidi ni hiyo kulenga kupata maeneo mengi zaidi ya kupata samaki. Yale madhumuni bado yanaendelea kwamba kuna *regulation and control of fish, fish products and aquatic flora and its products.* Sasa hapa unaona kwamba, sheria hii imepiga hatua ingawa tunafuta ile sheria ya mwaka 1970, tumepiga hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala limezungumzwa juu ya usalama wa wavuvi katika maeneo yetu ya uvuvi na hasa katika maziwa yetu na najua hili kwa sababu katika Mkoa wangu kule Kigoma, suala la usalama kwa wavuvi ni tatizo kubwa sana, masuala ya ujambazi ziwani unaweza kusema yamefika mahali hata ukatumia neno kukithiri. Lakini kitu kimoja ambacho kinatia matumaini ni kwamba, sisi katika uongozi wa Mkoa wa Kigoma, hawa ambao wamekuja kuweka mitambo yao ya simu za mkononi tuliwaambia wafunge mitambo yao ili kuwezesha masafa yale ya simu za mkononi kwa wavuvi wale wanaokuwa kule ziwani, likitokea tatizo waweze kuwa na mawasiliano na Jeshi letu la Polisi ikibidi Jeshi la Ulinzi kwamba liko tatizo la majambazi kule Ziwani ili kama ile boti inayokwenda kasi ya kupambana na masuala ya ujambazi ziwani waweze kupewa nguvu. Kwa maana hiyo, unaona mchango wa mawasiliano katika maendeleo katika nyanja zote za uchumi wetu. Hili nilidhani nalo tuliseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo moja ambalo wachangiaji wamesema kwamba, unapovua samaki ingefaa kuwe na viwanda vya kusindika samaki. Nakubali lengo la msingi ni hilo lakini siku hizi tunazungumzia uchumi wa soko na uchumi huria. Sina hakika suala la kusema kiwanda cha kusindika samaki kiwe wapi, huwezi kulitolea uamuzi kwa maana ya kusema lazima kiwe sehemu fulani. Niseme tu kama si

kuchekesha, mimi nisingechukia kama kiwanda cha kusindika samaki wangekiweka Kibondo, lakini nani atagharamia ujenzi wa kiwanda cha Samaki Kibondo na hao samaki wanaotoka Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, kwa nini ufanye uamuzi ambao kwa vyovyote vile misingi ya uchumi itakuambia aah nafikiri hapa hujalenga sawasawa? Kwa hiyo, hili ingawa limetoka lakini pamoja na nia njema kabisa ya Serikali, suala la viwanda vya kusindika samaki vijengwe wapi, sidhani huko tunakokwenda katika misingi ya uchumi wa soko tunaweza kusema tuna kauli kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kwa yale aliyoyasema katika mchango wake. Liko suala moja ambalo ameligusia ambalo wakati mwingine tunalisahau, alizungumzia juu ya suala la umuhimu wa maabara. Ni kweli suala la utafiti ni la kudumu katika mambo yote tunayoyafanya na niseme tu katika mradi ambao unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika Ziwa Victoria, maabara ya kujihakikishia ubora wa maji na ubora wa minofu ya samaki iko katika mradi ule. Kwa hiyo, alichokisema Mheshimiwa Kazi ni kitu ambacho anakisema kwa ufanisi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika lile nililoligusia katika vikundi vya *Beach Management Units,* liko moja ambalo ni la msingi sana na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dr. Limbu, analifahamu vizuri sana kwa sehemu ya Kayenze. Wana *Beach Management Unit* pale ambayo ni Wakala wa Halmashauri, sasa sina hakika kama iko Magu au imesogezwa Jiji la Mwanza, lakini lile nililolisema napenda niongezee kusema kwamba, ilifika mahali kwa siku kikundi kile walikuwa wanakusanya si chini ya shilingi milioni 15. Kwa vyovyote vile katika kupambana na umaskini unaona kwamba, hapa wamepiga hatua. *(Makofi)*

Labda nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, kwa mchango wake ambao ulikuwa *to the point* na mfupi kuliko michango mingine yote. Yeye alikuwa anasema mnazungumzia juu ya nyavu zenye matundu ya inchi tatu, sasa wananchi wamemtuma Serikali tumwambie unavuaje dagaa kwa wavu wa nchi tatu na aliliweka vizuri sana, mnajua namna yake ya kuchangia. Akazungumzia pia suala la sheria kutafsiriwa kwa Kiswahili kusudi watu walio wengi waweze kunufaika, ni suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba, kwa wale watakaobahatika kusoma *document* ya *NEPAD, New African Partnership for Development,* suala linaloitwa *cultural diversity,* umuhimu wa thamani ya mila na desturi zetu katika jamii ulivyo na thamani katika jamii na nchi za Afrika utaukuta hapa huhitaji wavu wa nchi tatu kuvua dagaa, wananchi wanajua wafanye nini waweze kuvua dagaa. Kwa maana hiyo alichokuwa anakisema Mheshimiwa Namkulala ni kwamba, tuwasikilize wananchi huwezi ukavua dagaa kwa ndoana au kwa wavu wa nchi tatu, hutapata dagaa lakini wananchi wanajua wafanye nini na maana yake tuwasikilize. Wakati mmoja nilikuwa nasoma kitabu kimoja, yupo Mwanasiasa mmoja wa India alikuwa anasema hivi: *"Where democracy is concerned people are Gods lets go to our Gods". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia niseme mawili, matatu, naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga. Nianze na lile alilosema kuhusu Serikali inavyotekeleza shughuli zake na hasa katika kupambana na uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, Serikali inakubaliana na msemo wa nguvu ya soda, hata kidogo Serikali haifanyi mambo yake katika kuwatumikia wananchi kama nguvu ya soda, haitawezekana. Serikali ina nia thabiti na kwa kweli wale ambao nakumbuka nilipata nafasi ya kuzungumza nao tarehe 27 Januari, 2003 na walituambia dhahiri kwamba waharibifu wa mazingira waliosababisha samaki wakubwa kupotea ni miongoni mwa wale wakazi wa maeneo yale yale. Sasa ambacho napenda kusema ni kwamba, kama hawaamini kwamba Serikali haiendeshi mambo yake kama nguvu ya soda, labda waanze kujiuliza nini kimetokea mpaka hivi sasa kwa *operation* ile iliyofanyika na hatutaki iwe *operation,* tunapenda kuwaarifu kwamba, kazi ile itakuwa ya kudumu na kama wanasikia misemo ya mijini waanze kujiuliza kati yao na Serikali kwa utaratibu wa kudumu, nani zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe, ile safari tuliyoifanya kwenda Ziwa Jipe ilikuwa ni ya kuthibitisha kwamba, Serikali yetu inawajali watu wake. Tumekwenda pale na tumejionea jinsi magugu maji yalivyokwishavamia eneo zaidi ya nusu ya Ziwa Jipe kwa upande wa Tanzania na jinsi wavuvi na wafugaji hawa tunaowazungumzia wanaofikia 8,000, walivyoathirika hadi wakalazimika kuhama sehemu ile na kwenda sehemu nyingine.

Tulifanya vile kama nilivyowahi kusema Bagamoyo, sio kwa sababu tunapohifadhi mazingira au tunaposhughulikia suala lolote linalohusiana na mazingira, tunafanya matambiko, hapana tunafanya vile kwa sababu kuna raslimali inayowapatia wananchi wetu riziki na vikundi kujitafutia maendeleo.

Kwa maana hiyo, sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa niaba ya Watanzania wote, tutaendelea kutekeleza yale yaliyo ndani ya uwezo wetu kama tunavyosema katika dua kila siku, kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Uvuvi wa Mwaka 2003**
***(The Fisheries Bill, 2003)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tulionao na kwa sababu Kanuni zinaturuhusu, Katibu atakuwa anataja sehemu nzima kama mtu una tatizo na sehemu hiyo basi utasimama ili uweze kuhoji, Katibu endelea.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana katika Kifungu cha 9(1)(k)(iv): *"consulting with neighboring states before deviating water causes or introducing non...)"*, yaani ku-*insert* maneno *"deviating water causes"* ili sheria hii ihusu pia kuweka mazingira ya mwenendo wa mabwawa na mito ambayo inashirikisha zaidi ya nchi moja, ifanikishe nchi zote.

**MWENYEKITI:** Kwetu sisi hapa hatujapata mabadiliko hayo kwa maandishi lakini kama Waziri anaona halina matatizo kwake basi anaweza akajibu *amendment* hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na namshukuru Profesa Maghembe, kwa hili analolisema. Kusema kweli kile anachokisema kinalenga wale majirani zetu na sio sisi wenyewe na ndio maana sisi tumesema tufanye mawasiliano na kushauriana na wengine. Nina hakika ambacho anakisema Mheshimiwa Profesa Maghembe hapa ni kwamba, nchi nyingine hawajali hili kwa sababu linakuja kutupa madhara sisi. Sasa sio rahisi Bunge lako tukatunga sheria kwa wengine lakini hii ni tahadhari kwamba, tutakapokuwa tunawasiliana na nchi jirani, tulisisitize hili ambalo

tumeliweka katika Muswada huu kwa nia njema kwamba na wao kama tunavyosema wale tunaosali Jumapili, usimtendee mwenzako usichopenda kutendewa wewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29

**MHE. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niko katika Sehemu hii ya Saba, kifungu cha 30(b). Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi mzuri alioutoa baada ya mchango wangu wa jana, lakini bado nina tatizo ambalo nadhani ni la kisheria. Ukisoma hicho kifungu cha 30(b) kinasema: *"Promote and assist in the development of community management units by giving grants and assisting groups of persons wishing to form fisheries conservation and protection groups."* Hoja hii ya ku-*promote* hizi *groups* za *conservation and protection* ni sawa, *issue* yangu ilikuwa kwamba, katika Mfuko huu mzima hapa ndipo ambapo ingeongezwa *"in the participation of the fishing activities"* kwa sababu hawa hawajawa *direct supported to do sustainable fishing.* Sasa hili ndilo lilikuwa tatizo langu, *you can protect, you can conserve but they are not empowered to fish sustainable*. Sasa hili ndio nilitaka *commitment* kama Waziri anasema kwenye kanuni itatafutwa uwezekano wa kuwezesha wavuvi hawa wadogo wadogo waweze kuvua na kwa sababu hoja kubwa ilikuwa ni kwamba kama ukitaka kufanya uvuvi endelevu gharama zake ni kubwa kwa watu ambao wanaishi kwa dola moja kwa siku.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuonyesha msisitizo. Eneo hili katika Muswada na katika mtazamo wa shughuli nzima ya uvuvi kwa wavuvi wetu wadogo wadogo ni mpya na kama nilivyosema na yeye anakiri kwamba, inawezekana tuna tatizo la kisheria, nimkubalie kwamba, kama nilivyosema wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, bila shaka kanuni zitakazotolewa na Mheshimiwa Waziri, kwa kulenga kuitafsiri sheria hii kwa vitendo na kwa kuzingatia maslahi ya walengwa bila shaka hivi vikundi havitakuwa na maana kama havitajishughulisha na uvuvi lakini vile vile kwa sababu tumeanzisha Mfuko itakuwa na maana zaidi na kwa kweli itakuwa ni kupambana na

umaskini kwa vitendo na kwa ufanisi kama vikundi hivi vitawezeshwa. Kwa hiyo, natarajia kanuni zitalenga kutekeleza hilo. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani mimi ni mjumbe wa Kamati, sasa sio kama nataka kuleta marekebisho, isipokuwa nataka kusema kwamba, katika kifungu hicho hicho cha 30(j) kinasema: *"Promote acquaculture activities and restocking of natural water bodies".* Sasa hivi kuna zao lingine ambalo lipo Baharini ambalo kwa kiwango kikubwa na wananchi wa ukanda mzima wa Pwani wanaanza kulifuatilia na kulitia mkazo. Naomba kama kutakuwa na uwezekano kuongezwe (m) ku-*promote mare-culture*, ukulima wa mwani. Wakulima wa mwani nao wawekwe katika sheria hii ili waweze kutambulika na waweze kupata msaada katika Mfuko huu ambao utasaidia jamii nzima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia. Ukiangalia sehemu ile ya Kifungu 30(l) kinasema: *"Promote such other activities of a like nature to those set out in this section as will advance the purposes of this Act".* Kama nilivyosema wakati mwingine katika utaratibu wa kutunga sheria husemi kila kitu unaweka msingi na hapo baadaye kama nilivyosema mnakuta mna kitu wanaita *felt need* katika kanuni kwa sababu msingi unakuruhusu unaliweka katika suala la utekelezaji. Kwa hiyo, nina hakika kama halipo mahali pengine katika Muswada huu lakini sehemu ile inamruhusu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatunga kanuni na suala la kilimo cha mwani liweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 38

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 58
Kifungu cha 59

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kusaidiwa pengine sielewi, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie. Katika ile 4, pale juu anasema: *"List of offences that may be compounded permitting others to use unregistered vessel for fishing."*

Sasa hapo mimi ninavyoelewa, mwenye uwezo wa kutoa ruhusa ya kuvua au kutumia vyombo majini ni Mkurugenzi mwenyewe. Sisi wengine watu wa pembeni tunachoweza ni kumshawishi tu mtu kufanya makosa, lakini siwezi kutoa ruhusa ikaitwa ni ruhusa.

Sasa hii *permission* inatolewa na Mkurugenzi, nilikuwa nafikiri hapa je, isingefaa kusema kwamba, *using unregisteredvessels for fishing* kwa maana ya kwamba, hii *permission* inatolewa na Mkurugenzi mwenyewe? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ya nne ya jedwali, ambayo inaturudisha kwenye kile kifungu kilichompa mamlaka Mkurugenzi na Afisa yeyote aliyeidhinishwa, kutolazimika kupeleka kila kosa au tuhuma ya kosa Mahakamani na badala yake kulishughulikia kiutawala, sasa ninachosema hapa kama mtu atakutwa na kosa la kuruhusu mwingine kutumia chombo cha uvuvi ambacho hakijasajiliwa, sasa kosa hilo kwa orodha hii iliyoko hapa, Mkurugenzi anaruhusiwa kushughulikia kosa hilo kiutawala.

Ndicho kinachosemwa hapa na pengine msingi wake ni kwamba, kama ni matumizi ya chombo ambacho hakijasajiliwa na hakuna madhara mengineyo yote ya mazingira na nini, nadhani ndicho kinacholenga na linaweza kutokea kosa la namna hii.

Kwa mfano, tunapozungumzia vile vikundi vya *Beach Management Units* au vile vikundi alivyokuwa anavizungumzia Mheshimiwa Balozi Mongella, ikawa imetokea katika kikundi wameruhusu chombo cha uvuvi ambacho hakijasajiliwa kikawa kinavua lakini kwa misingi ambayo inakubalika kwa chombo kilichosajiliwa, sasa hapa ndiyo Mkurugenzi anaruhusiwa kushughulika na kosa hilo la kuruhusu tu kiutawala kuliko kupelekana Mahakamani, kwa sababu madhara hayapo ila kosa ni kwamba hakijasajiliwa. Hayo ndiyo maelezo.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Uvuvi wa Mwaka 2003**
***(The Fisheries Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu likikaa kama Kamati ya Bunge Zima, limepitia Muswada wa Sheria ya Serikali unaoitwa Muswada wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 *(The Fisheries Bill, 2003),* pamoja na marekebisho yaliyofanywa na kuupitisha. Naomba kutoa taarifa kwamba, sasa Muswada huo ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuongeza Muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(The Presidential Parastatal Sector Reform Commission)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tume si chombo cha kudumu, ni chombo ambacho kimeridhiwa kutekeleza Sera ya Taifa ya ubinafsishaji. Kwa mara ya mwisho mwaka 1999, Bunge hili Tukufu liliridhia kuongeza muda wa Tume kwa miaka minne hadi 31 Desemba, 2003.

Aidha, ilitamkwa kwa Azimio la Bunge, muda huo unaweza kuongezwa endapo shughuli za kurekebisha, kubinafsisha mashirika hazitakuwa zimekamilika kwa utaratibu wa Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa ya utendaji wa Tume katika kipindi hicho cha miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali inawasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu, Azimio la kuongeza muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(The Presidential Parastatal Sector Reform Commission).* Azimio hili limekwishapitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge chini ya Uenyekiti wake Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Chunya. Tunaishukuru sana Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji imetoa taarifa ya utendaji wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kwa kipindi cha mwaka 2000 hadi 2003. Ukurasa wa 6 - 8 unaelezea tathmini ya utendaji wa Tume wakati ukurasa wa 9-10 unaonyesha mafanikio ya ubinafsishaji. Ukurasa wa 11 - 13 unaonyesha matatizo yaliyojitokeza katika zoezi zima la ubinafsishaji katika kipindi tajwa, pamoja na taratibu za ufumbuzi wa matatizo hayo. Ukurasa 13 - 14 unaonyesha kazi iliyoko mbele ya Tume kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utendaji inaonyesha kuwa bado mashirika 77 hayajabinafsishwa, lakini la muhimu zaidi ni yale mashirika ya huduma na miundombinu. Ubinafsishaji wa mashirika hayo, pamoja na *NMB,* unahitaji uangalifu mkubwa sana ukihusisha pande zote za Serikali na Bunge kwa ujumla wake. Sababu kubwa ni kuwa hii ni miundombinu inayomgusa kila mwananchi nchini kwetu. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa, ubinafsishaji wa maeneo haya unakuwa wa makini na tija. Uzoefu katika nchi nyingine duniani unaonyesha kuwa ubinafsishaji wa huduma za miundombinu unachukua muda na kwa hiyo basi, kasi ya ubinafishaji wa mashirika haya utazingatia hali hii ili kuepukana na matatizo yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuuliza kwa nini muda unaoombwa kuongezwa ni miaka minne na siyo muda wote mwingine. Mantiki ya muda huu ni kutokana na uzoefu tulioupata hapo nyuma. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, viwanda 90 na mali nyingine 215 vimebinafsishwa. Hii inatupa wastani wa takriban viwanda 23 kwa mwaka na mali nyingine takriban 54, hii ni kazi kubwa. Muda wa miaka minne utafanya Tume kuendelea na zoezi la utekelezaji wa sera hii muhimu kwa uangalifu bila ya haraka isiyo ya lazima. Aidha, muda huu utatoa nafasi ya kutatua baadhi ya matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo litapewa umuhimu mkubwa ni lile la kuimarisha zaidi ufuatiliaji wa utekelezaji wa makubaliano ya kuendesha viwanda vilivyobinafsishwa, pamoja na matakwa yaliyofikiwa katika Mikataba baina ya Serikali na wawekezaji. Hadi sasa jukumu hili la ufuatiliaji limeachiwa Wizara husika. Mkazo mkubwa kwa sasa ni kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji katika Wizara husika. Hapa niipongeze sana Kamati za Fedha na Uchumi na ile ya Uwekezaji na Biashara, kwa ufuatiliaji wa karibu sana wa mashirika yaliyobinafsishwa hata kusaidia kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika maeneo yaliyobinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine linalozungumziwa ni lile la usiri wa Mikataba. Napenda niseme kimsingi Mikataba hii siyo siri kwa sababu utayarishaji wake unahusisha wadau wengi kwa mfano, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia ngazi mbalimbali hadi kufikia maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Hata hivyo, ni utaratibu wa Kimataifa kuwa si jambo la busara kuweka wazi mpango wa mtaji na uwekezaji pamoja na mpango wa kazi wa wawekezaji kadhaa wanaowania kununua mali husika kwa njia ya ushindani. Hii si kwa Tanzania bali ni utaratibu wa dunia nzima. Tutaendelea na jitihada za kuelimishana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo litaangaliwa zaidi ni dhana inayojitokeza kuwa Tume ni chombo kisichojali wananchi hasa linapokuja eneo la ulipaji wa mafao ya wafanyakazi. Ukweli ni kuwa Serikali imekwishalipa mafao yote ya kisheria kwa wale wafanyakazi walioachishwa kazi. Tatizo linalojitokeza ni pale wafanyakazi wanapodai mafao ya ziada kama mkono wa dhahabu katika mashirika yaliyofilisika au kufanya kazi bila faida. Kwa mashirika ya aina hii, mafao ya aina hiyo ni tabu kupatikana bila kutumia kodi za wananchi. Aidha, tatizo la mafao ya pensheni linajitokeza sana kwa vile mashirika hayakuwa yakiwasilisha makato ya michango husika kwenye vyombo husika. Katika hali hii, Serikali inajikuta ina shinikizo ambalo linatokana na uzembe uliofanywa na *management* za mashirika husika. Kwa mantiki hii, hata wafanyakazi wanapozingira Ofisi za Tume kudai mafao ya aina hiyo, ni taratibu ambazo zinapeleka azma hizo mahali pasipohusika. Tume haitunzi hazina. Hata hivyo Serikali inaangalia taratibu kadhaa za ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kijacho, Tume itaendelea kutoa semina, elimu, hamasa na taarifa mbalimbali kuhusu madhumuni, mafanikio na matatizo ya ubinafsishaji kwa wananchi ili waelewe sera hii ya ubinafsishaji. Kwa bahati mbaya hivi karibuni kumetokea upotoshaji wa makusudi kabisa wa kukejeli sera hii nzuri ya CCM. Ubinafsishaji umeongeza ajira ya moja kwa moja na ile itokanayo na kuongezeka kwa uzalishaji katika mashirika yaliyobinafsishwa. Ubinafsishaji umesaidia kukuza uchumi wetu. Ubinafsishaji umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza mapato ya Serikali kwa njia ya kodi na gawio kutoka viwanda vilivyobinafsishwa na kufufuliwa. Ubinafsishaji umeongeza upatikanaji wa bidhaa muhimu katika uchumi wetu. Wananchi wanapoelezwa haya vizuri wanayaelewa bila ya matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa Tume utaendelea kugharamiwa na fedha za Benki ya Dunia. Serikali ilipata mkopo kutoka Benki ya Dunia wa dola za Kimarekani 26.6 milioni na hadi sasa zimetumika dola 11.4 milioni. Bunge hili halitakuwa na jukumu la kutafuta fedha za uendeshaji wa chombo hiki. Yapo mawazo ya kurekebisha Sheria ya *Specification,* ambayo inaonekana inaipa nguvu Tume juu ya viwanda vinavyokuwa *specified*. Utaratibu huu ni kinga kubwa na muhimu kwa mali ya Serikali. Hata hivyo, Serikali inauchukua ushauri huu ili iufanyie kazi. Kwa hatua za sasa, kanuni za Bunge haziruhusu kufanya marekebisho kwenye Sheria ya *Public Corporation Act, 1992* hata kama hoja hiyo ingekubalika na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Tume itaendelea kutoa taarifa zake mara kwa mara ili Serikali na Bunge ifanye tathmini ya kujua maendeleo ya sera ya ubinafsishaji. Hii itasaidia vile vile kutafuta ufumbuzi wa pamoja wa matatizo hasa tunapoelekea kipindi cha ubinafsishaji wa mashirika ya umma na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi Serikali ilivyotekeleza sera ya ubinafsishaji ambayo ni asilimia mbili tu ya urekebishaji uchumi, miundombinu na huduma za jamii, tunazo changamoto mbili: Kwanza, ni jinsi gani mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na ubinafsishaji yatakuwa endelevu, tukiangalia ukurasa wa 10 na kiambatanisho (d) cha taarifa na yanayostahmili mabadiliko ya sasa ya uchumi.

Pili, ni jinsi gani kwa mashirika yaliyobaki tutaendelea kutoa upendeleo maalum kwa Watanzania kama hapo nyuma. Ni vema Watanzania wakatwaa fursa hizi si kwa kisiasa tu bali kwa mantiki ya tija, uchumi na ufanisi. Hata hivyo, tunajaribu kuelimishana kuwa sera ya ubinafsishaji lengo na madhumuni yake si kwa Serikali kuuza mashirika hayo ili ipate fedha, bali lengo kuu ni mashirika hayo yafufuliwe na kukarabatiwa ili yachangie katika ujenzi wa uchumi wetu, ambao hivi sasa Tanzania ni nchi ya kwanza katika kukuza uchumi katika nchi za Afrika Mashariki na ni nchi ya tatu katika nchi za *SADC* katika kukuza uchumi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwasilishe Azimio la kuongeza muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(The Presidential Parastatal Sector Reform Commission).*

KWA KUWA Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma iliyoundwa mwaka 1993 chini ya Sheria ya Umma ya Mwaka 1992 kama ilivyofanyiwa mabadiliko kwa Sheria Namba 16 ya Mwaka 1993 *(The Public Corporations (Amendment) Act, 1993)* kwa nia na madhumuni ya kutekeleza sera ya ubinafsishaji, yaani kurekebisha na kubinafsisha mashirika ya umma yapatayo 400;

NA KWA KUWA madhumuni ya kundwa kwa Tume hii haikutarajiwa kwamba Tume hiyo itakuwa ya kudumu na hivyo muda wa uhai wake umekuwa unawekwa na Bunge kulingana na majukumu ambayo hayajatekelezwa kama ilivyokusudiwa;

NA KWA KUWA wakati wa kurekebisha Sheria ya Mashirika ya Umma mwaka 1999, majukumu ya Tume yalipanuliwa kupitia Sheria Na. 17 ya Mwaka 1999 na kujumuisha usimamizi wa uanzishwaji wa Mamlaka na Udhibiti;

NA KWA KUWA katika marekebisho yaliyofanyika mwaka 1999, Bunge liliongeza muda wa Tume kwa kipindi cha miaka minne kuanzia tarehe 1 Januari, 2000 hadi tarehe 31 Desemba, 2003 na kwamba muda huo unaweza kuongezwa kwa Azimio la Bunge endapo Serikali itawasilisha mapendekezo Bungeni pamoja na taarifa ya utendaji wa Tume katika kipindi hicho;

NA KWA KUWA Serikali imewasilisha taarifa ya utendaji wa Tume inayoonyesha kuwa licha ya Tume kufanya kazi kwa ufanisi mzuri katika kipindi cha miaka minne iliyopita, bado mashirika sabini na saba (77) hayajarekebishwa au hayajabinafsishwa;

NA KWA KUWA taratibu za kuanzisha mamlaka za udhibiti ikiwa ni pamoja na utungaji wa sheria zinazoanzisha mamlaka hizo bado zinaendelea na ziko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji;

NA KWA KUWA utekelezaji wa majukumu ya kazi za Tume bado unaendelea na Taarifa ya utendaji inaonyesha kuwa kulingana na majukumu na kazi zilizobaki, muda wa miaka minne unahitajika ili Tume iweze kukamilisha majukumu na kazi hizo;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa Kifungu Na. 21(3) cha Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992, kama kilivyofanyiwa mabadiliko, ambacho kinalipa Bunge madaraka ya kupokea taarifa na kupitisha Azimio la Kuongeza Muda wa Tume, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu linaazimia kuwa muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma uongezwe kwa kipindi kingine cha miaka minne kuanzia tarehe 1 Januari, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ambayo imepitia Azimilio hili, nitoe tu maelezo kidogo. Kwa mujibu wa kanuni ya 49A kanuni ndogo (c) msemaji anayewasilisha maoni kwa mujibu wa kanuni ya 43(5)(b) na (c), ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika thelathini, hii ni kwa Mwenyekiti ambaye atawasilisha.

Sasa nakusudia kufanya jambo ambalo pengine hatujalizoea sana, nitampa muda kwa sasa hivi aweze kusema kama atakuwa hajamaliza ataendelea jioni. Hii ni kwa sababu kazi tuliyo nayo ni kubwa sana na tuna siku mbili tu, tuna leo na kesho, walioomba kuchangia hii ni wanane ambao maana yake ni saa mbili, saa mbili za jioni maana yake ni hao wanane, hivyo bado hata Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hiyo mtaona tuna matatizo namna ya ku-*manage* muda. Kwa hiyo, nitamruhusu aseme kama atakuwa hajamaliza nitampa nafasi jioni aendelee.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (k.n.y. MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni Na. 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Kuongeza Muda wa Uhai wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, ambao muda wake wa sasa utakoma ifikapo 30 Desemba, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge ambao siyo wajumbe wa Kamati, kwa kuhudhuria kikao cha Kamati kilichojadili Azimio na kuweza kulitolea maoni. Aidha, Kamati inampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kuwasilisha mbele ya Kamati maudhui na makusudio ya Azimio yaliyolenga katika kuiongezea Tume muda wa miaka minne ili iweze kuendelea kutekeleza kazi yake ya kurekebisha mashirika ya umma ambayo bado haijakamilisha ubinafsishaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kazi ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma bado haijakamilika ambapo kwa mujibu wa taarifa ya utendaji wa *PSRC* ya

kuishia Desemba, 2003 imebainisha kazi itakayofanywa katika kipindi kijacho cha Tume ni kushughulikia ubinafsishaji wa mashirika makubwa na nyeti kama vile *TANESCO, TRC, TAZARA, THA, BIMA, TTCL* na *NMB,* pamoja na kukamilisha ubinafsishaji wa mashirika na makampuni ambayo ubinafsishaji wake upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utangulizi huo hapo juu, napenda kulielezea Bunge lako Tukufu kuwa, Waheshimiwa Wabunge wote walijadili kwa kina Azimio hilo na kulitolea maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa pamoja na kuleta Azimio la kuomba *PSRC* kuongezewa muda, ni vema pia ingeonyeshwa taarifa ya kina ya tathmini ya zoezi la ubinafsishaji na programu nzima ya jinsi Tume itakavyoitekeleza kazi yake baada ya kuongezewa muda;

(ii) Kutokana na kazi kubwa itakayofanyika ya kubinafsisha mashirika makubwa na nyeti, Kamati ilipatwa na wasiwasi iwapo muda wa miaka minne kama kweli utatosha kukamilisha zoezi la kubinafsisha mashirika yaliyobakia na hivyo wengi wa Waheshimiwa Wabunge walishauri ikiwezekana muda wa kuongezewa uwe zaidi ya miaka minne. Lakini kwa ajili ya udhibiti wa Bunge kipindi hicho kilibaki miaka minne;

(iii) Kamati imebaini kuwa katika kipindi chote cha utendaji wa *PSRC,* kumejitokeza matatizo mengi ikiwa baadhi yake ni pamoja na wawekezaji kutoheshimu Mikataba, mashirika mengine kuwa *specified* kwa muda mrefu, kuwepo kwa migogoro ya wafanyakazi, ufuatiliaji hafifu wa wawekezaji na ni nani anayehusika kufanya kazi ya ufuatiliaji, baadhi ya viwanda kufungwa au kutumika kwa kazi ambayo haikukusudiwa, pia baadhi ya wawekezaji kutolipa gharama ya mauzo kama ilivyo katika Mikataba;

(iv) Kamati imebaini pia kuwepo kwa hisia kuwa *PSRC* imeelemewa na majukumu iliyonayo na kwamba ipo haja ya kuanzisha chombo kingine chenye nguvu za kisheria kitakachokuwa kinatathmini kazi za Tume na kutolea maoni Bungeni. Aidha, ili kuondokana na matatizo yaliyojitokeza na ambayo yamesababisha ubinafsishaji wa baadhi ya mashirika, viwanda na makampuni, ni vema sheria ya uwezeshaji ikaangaliwa upya;

(v) Kamati ilipatwa pia na wasiwasi juu ya migongano ya kiutendaji kati ya mamlaka za udhibiti na Serikali ambapo mamlaka hizi zinakuwa na nguvu zaidi ya kisheria kuliko hata Wizara husika pale inapofikia kutekeleza kazi zake kama Kimahakama; na

(vi) Kuna kesi nyingi mno Mahakamani na nyingi ya kesi hizo haziishi kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina Kamati ilipitisha Azimio na kuagiza:-

(a) Tathmini ya mara kwa mara ya zoezi la ubinafsishaji iwe inafanyika.

(b) Wizara mama zihusike katika kufuatilia kisheria utekelezaji wa wawekezaji.

(c) Takwimu sahihi za mashirika yaliyopo katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji zionyeshwe katika taarifa za utendaji za Tume.

(d) Serikali iwe makini na siyo kubinafsisha mashirika yaliyobakia kwa haraka haraka hususan yale ambayo ni makubwa na nyeti. Tukifanya makosa hasara itakuwa kubwa na gharama kwa Taifa itakuwa kubwa sana.

(e) Elimu zaidi itolewe kwa ujumla juu ya zoezi la ubinafsishaji.

(f) Kwa kushirikiana na Wizara husika, kuendelea kufuatilia kesi zilizopo Mahakamani zinazohusiana na ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru tena Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wasaidizi wake, Mwenyekiti Mtendaji wa *PSRC,* Ndugu John Rubambe na wasaidizi wake, kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake katika muda uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti kwa kuokoa muda. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tutampa nafasi jioni. Kwa hiyo, kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS - MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuongeza muda wa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kama lilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri katika kipindi cha Bunge cha asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 43(5)(c) cha Kanuni za Bunge, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Azimio la Kuongeza muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kama lilivyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Kambi ya Upinzani kwa kuwawakilisha Watanzania walio wengi ambao wameshakerwa mno na utendaji usioridhisha wa *PSRC* ikiwa ni pamoja na kuwataabisha wafanyakazi walio wengi

walioondolewa kazini katika Mashirika na Viwanda mbalimbali na wasipate mafao yao, tunapata kigugumizi na kuwa wazito kulikubali moja kwa moja Azimio lililoletwa mbele ya Bunge hili Tukufu. Sio siri kwamba, *PSRC* imeshindwa kulifanya lile ambalo Watanzania walio wengi walilitegemea kutokea kama mafanikio ya huo unaoitwa Ubinafsishaji badala yake wameambulia ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri *PSRC* na Serikali pindi wanapozungumzia suala la mafao au mkono wa kheri kwa watumishi wanaoachishwa kazi, kutegemea faida iliyotengenezwa na Viwanda au Mashirika, ni bora wakarejea huko nyuma ambapo Viwanda na Mashirika yetu vilikotoka. Mkono mrefu wa Serikali uliokuwa umeingizwa ndani ya Viwanda na Mashirika haya uliyaweka hoi bin taabani. Mashirika haya na Viwanda vilibebeshwa mzigo wa kugharamia hata mambo ambayo yalikuwa nje ya shughuli zao. Chama wakati huo kilikuwa kimekamata hatamu zote za nchi. Ufanisi wa *management* ya *TANESCO* ya wakati ule hauwezi kuufananisha na sasa hivi na *management* ya *Net Group Solution,* ambayo sisi wenyewe tumeipa meno na jeuri ya kulikatia hata Jeshi umeme au nchi kama Zanzibar pindi wanapochelewa kulipia madai ya umeme. Sera ya Ubinafsishaji ambayo kimsingi Kambi ya Upinzani haiipingi, lakini namna inavyosimamiwa na kuendeshwa na *PSRC* ndiyo jambo linalotutia mashaka na kupinga Azimio la kuwaongezea muda wote huo wa miaka minne, maana ndani ya muda mrefu wa jinsi hiyo Watanzania wanaweza kumalizwa kabisa kama siyo kufutika katika kuumiliki na kuutawala uchumi wa nchi yao, endapo mambo ya msingi ya kuirekebisha *PSRC* yatakuwa hayajafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania bila kutambua nini kilichokuwa kinawajia mbele yao, waliingizwa mjini na huenda wakaendelea kuingizwa mjini na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 1995, ambayo pamoja na mambo mengine kifungu namba 7(1) kinaeleza kwamba: "Mashirika ambayo ni ya msingi na nyeti yaani Bandari, Reli, Posta, Simu, Mabenki ya Umma na Nishati kwa maendeleo ya Taifa, yanaendelea kumilikiwa na dola. Wananchi wanaweza kununua sehemu ya hisa katika Mashirika hayo ambayo pia yanaweza kuingia ubia na makampuni binafsi mradi tu uwiano wa hisa unalifanya Shirika kuendelea kuwa la dola."

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ambayo imetokea na inayoendelea kutokea ni kinyume kabisa na hayo waliyoahidiwa Watanzania kutokana na Mikataba ambayo Serikali imeingia na hao wanaoitwa wabia, wanunuzi, wakodishaji, wawezeshaji na majina mengine ya kupigana chenga. Hiyo inayoitwa dola imepoteza mamlaka na uwezo wa kuyasimamia na kuyatolea maamuzi Mashirika haya na maamuzi yamebakia kwa wawekezaji na wanunuzi toka nje. Hizo zinazoitwa hisa za Watanzania zimebakia kilemba cha kukoka cha kuwafanya Watanzania wajione kama vile wamepata kumbe wamepatikana. *Privatization Trust Fund* chombo ambacho kilipaswa kusaidia na kuhakikisha Watanzania wanawezeshwa na wanapata uwezo wa kununua na kumiliki hisa ndani ya Mashirika yaliyobinafsishwa, kimeshindwa kufanya kazi hiyo na Watanzania wameishia kunawa tu. Mashirika makubwa na yenye kutengeneza faida nzuri, yamechukuliwa na wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri kwamba, madhumuni ya kuundwa kwa Tume hii mwaka 1993 haikutarajiwa kuwa ya kudumu, mwelekeo na hoja inayotaka kujengwa na kuendelezwa hapa ni kutaka kuipa *PSRC* kibarua cha kudumu au wakati wote kujenga mazingira ya kutokamilisha kazi wanazopaswa kuzikamilisha. Kwa kuwa kuendelea kuwepo *PSRC* ni kuwahakikishia wahusika mkate wa kila siku, ni bora Bunge likaelezwa ukweli na likaombwa kuiunda *PSRC* kama chombo cha kuwepo siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumwoa mke kwa mkataba wa kumwondoa kwa vitisho vya kila baada ya miaka mitatu au miaka minne ni kumjengea mtazamo wa kukaa mkao wa kuondoka na kumfanya apange mkakati wa kukukomba na kukuacha mtupu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kelele ambazo zimekuwa zikipigwa ndani na nje ya Bunge kuhusu *PSRC* ni nyingi mno. Serikali kabla ya kuleta Azimio hili, ilipaswa kuleta *Comprehensive Report*, inayoonyesha uhakiki wa uendeshaji wa *PSRC* na mikakati ambayo imetayarishwa kuhakikisha kasoro ambazo zimekuwa zikijitokeza zitatatuliwa vipi au ni kwa namna gani hazitajirudia. Taarifa ya utendaji iliyoletwa sambamba na Azimio hili ni ya kufunika kombe ili mwanaharamu apite. *(Makofi)*

Tusiwaone Watanzania wako kimya tukafikiria hawaelewi au hawafuatilii nini kinachoendelea na hususan kuangalia hatma ya kile ambacho huko nyuma walielezwa kwamba, Serikali inakopa na kuanzisha Viwanda na Mashirika kwa manufaa yao au kwa manufaa ya umma. Ni vizuri Watanzania wakaelezwa kwa uwazi kwamba, inakuwaje kile ambacho waliwekeza kwa kufunga mikanda na Serikali yao dola za Kimarekani bilioni 9.5 kati ya mwaka 1968 hadi 1995, hivi sasa vitu hivyo vinabinafsishwa na kuuzwa kwa dola za Kimarekani milioni 500 na kati ya hizo zilizolipwa hadi tarehe 30 Juni, 2003 ni dola 278. Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kwamba, hata hizo dola milioni 222 huenda tukawa tumeingizwa mjini hasa tukiangalia *style* ya *PSRC* ya ufuatiliaji madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli watu ambao wameshindwa kukusanya pesa zetu hizo ndogo walizotuingiza mikataba inayoitwa ya siri, tukubali kwa haraka haraka tu kuwaongezea muda bila kuwawekea kibano kitakachowafanya wawajibike ipasavyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la *PSRC* ni kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji katika shughuli wanazozisimamia. Kwa mfano, Kiwanda cha *Polytex* kilichopata mwekezaji mwaka 1998 kwa dola za Kimarekani milioni 8, mwekezaji huyo alizungushwa na mwaka 2001 *tender* ilitolewa upya kwa mwekezaji aliyepatikana kwa dola za Kimarekani milioni 5. Hata hivyo, kiwanda hicho kilikuja kutolewa mwaka 2002 kwa dola za Kimarekani milioni 3 tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kama hiyo na nyingine nyingi zinazofanana na hiyo, zinazua harufu kubwa ya rushwa na Serikali lazima itoe maelezo ya kina kabla hatujaongeza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoteli ya Kilimanjaro utaratibu wa *tender* haukutumika na badala yake Ubalozi wa Saudi Arabia chini ya mfumo wa *"fast truck"* ulitumika. Kama hii inawezekana kwa nini tuwe na chombo wakati tuna Idara za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo Watanzania inabidi walielewe dhidi ya takwimu chungu nzima zinazowasilishwa kujengea hoja ya kuonyesha mafanikio yaliyopatikana ni sawa na mtu aliyezoea kulima kwa jembe la mkono siku anapopewa jembe la kukokotwa na ng'ombe (maksai), anaweza akaamini kwamba, hiyo ndiyo njia nyepesi na bora kuliko zote zilizoko duniani. Siku ya kuona trekta au *combined harvesteor* vikichakaza ardhi, ukiacha mtu huyo ashangae vilevile atafikiri ni uchawi unatembea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *PSRC* kama itaendelea kwa sura na mfumo uliopo, ni wazi itakuwa ni mzigo na sababu ya kero kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la usiri mkubwa wa mikataba inayofanyika litatuua kama sio kutumaliza kabisa. Jambo hili la kuendelea kuifanya mikataba iwe ya siri au kuzungumziwa ndani ya Baraza la Mawaziri tu kama lilivyozungumzwa hapa Bungeni na upande wa Serikali na hata huko nje ya Bunge, ni jambo ambalo Kambi ya Upinzani haikubaliani nalo. Kuna hatari ya suala hili la usiri kuendelea kuwafanya baadhi ya watu wachache wawe wananufaika na huo ubinafsishaji na Watanzania tulio wengi tuendelee kuwa wapiga debe na wapitisha Maazimio na Miswada ya Ubinafsishaji. Jambo linalotakiwa hapa na ambalo lingetangulia kabla ya kutushawishi kupitisha Azimio la Kuongeza muda, lingekuwa ni kutazama upya na kurekebisha maeneo ambayo yanapigiwa kelele na hasa suala la mikataba na namna ya kuondoa usiri unaoizunguka mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunaingia kipindi cha kubinafsisha na kukodisha *utilities,* shughuli ambayo Kambi ya Upinzani inaona inapaswa iangaliwe kwa umakini. Kuna hisa ambazo zinabaki bila kubinafsishwa hizi zinalindwa vipi kwa maslahi yetu Watanzania? Kwa namna ambavyo tumekuwa tunapelekwa, kumekuwa na utofauti kati ya kile kinachokuwemo kwenye sheria au sheria kwa kiasi kikubwa inakuwa finyu na hasa ukilinganisha na kile kinachokuwemo kwenye mikataba ya ubinafsishaji inayotengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kama Serikali imeng'ang'ania kuleta Azimio hili ili lipitishwe basi liambatane na sharti ya kuleta marekebisho ya sheria itakayohakikisha mikataba yote inawekwa wazi na kuletwa Bungeni kabla ya kusainiwa na pia sheria mahsusi inayowahakikishia Watanzania kuendelea kumiliki na kuwa na sauti ndani ya vyombo vinavyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani inatoa wito kwa Serikali kujenga utaratibu na tabia ya kulipa Bunge nafasi ya kuisimamia ipasavyo kama inavyotamkwa ndani ya Katiba yetu. Suala la *PSRC* halikupaswa kuwa jambo la

kuletwa kiharaka haraka namna hii wakati ilikuwa inaeleweka wazi kwamba, muda wa *PSRC* unaelekea ukingoni. Majukumu wanayoyafanya *PSRC* yanagusa sehemu kubwa ya hatma ya uchumi wa Taifa letu na maisha ya kila siku ya Watanzania walio wengi. Tusifanye mchezo na maisha ya watu. Bunge lilipaswa kupewa muda wa kutosha kulijadili suala la *PSRC.* Kutokana na kwamba kwa mujibu wa Sheria , *mandate* ya *PSRC* inakwisha Desemba na Serikali imeleta kwa makusudi Azimio hili dakika za majeruhi.

Kambi ya Upinzani inapendekeza *PSRC* ipewe mwaka mmoja na baada ya hapo kuletwe ripoti kamili Bungeni ambayo itajadiliwa kwa kina na Waheshimiwa Wabunge kwa minajiri itakayowezesha Serikali kuleta marekebisho ya sheria yatakayoziba mapungufu ambayo yamekuwa yakijitokeza ndani ya utendaji wa *PSRC*. Kwa misingi hiyo, Kambi ya Upinzani inaomba Bunge hili Tukufu, lipokee na kukubali mapendekezo ya marekebisho ya Azimio hili kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa, chini ya Kanuni za Bunge Namba 47(1) na (c) kwamba: Kwanza, inapendekezwa kuwa kabla ya kifungu kinachoanza na maneno KWA HIYO BASI ..... ukurasa wa tatu viingizwe vifungu vingine viwili vifuatavyo:-

NA KWA KUWA kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kuhusu jinsi na namna mikataba ya kubinafsisha Mashirika ya Umma inavyozua utata na pengine kulisasbabishia Taifa hasara;

NA KWA KUWA Waheshimiwa Wabunge huwa hawaioni mikataba hiyo yenye utata na hasara kwa Taifa kabla ama baada ya kusainiwa;

Pia katika kifungu cha mwisho kinachoanza na KWA HIYO BASI ..... baada ya tarakimu 2004. Inapendekezwa "nukta" iondolewe na iwekwe nukta mkato (;) na kuongeza maneno yafuatayo: "Na Tume kupitia Serikali iwe inawasilisha Bungeni mikataba ya kubinafsisha Mashirika ya Umma yote yaliyobaki kabla ya makubaliano ya mwisho na mwekezaji."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wakubwa kwenye hoja hii wamemalizika. Ninao wachangiaji wanane kwa hoja hii na pengine kwa sababu msemaji aliyemaliza sasa hivi amegusia mabadiliko ya hoja yaliyoletwa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, ningependa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Katibu ameyapokea na saini kama inavyotakiwa na Kanuni imepokelewa, sasa nadhani imeshagawanywa huko mliko. Kwa hiyo, kama ataona wakati umefika nitamruhusu ili aweze kutoa mapendekezo hayo.

Sasa namwita mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa William Shellukindo atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kidogo kuhusu Azimio la Kuongeza muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilianza kazi yake bila uzoefu wowote kwa hiyo imejifunzia kazini na katika hali hii kumetokea mambo mawili. Kuna baadhi ya maeneo Tume imefanya kazi vizuri na baadhi ya maeneo Tume imefanya kazi ambayo imezua matatizo au kumetokea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, katika baadhi ya Mashirika yaliyobinafsishwa, waliouziwa Mashirika hayo hawakutekeleza mikataba ipasavyo kwa maana ya kulipa. Kuna vipindi vya kulipa kwa hiyo kuna baadhi hawakuvizingatia vipindi hivyo, kwa hiyo hapo ni dosari moja ambayo imejitokeza na inaonekana katika taarifa ya Tume.

Vilevile kwa upande mwingine katika baadhi ya Mashirika ambayo yamebinafsishwa, yale majukumu yaliyokuwa yanafanywa na Mashirika hayo kwa wale ambao wameuziwa Mashirika hayo hasa Viwanda hawakutekeleza majukumu yaliyotakiwa yaendelezwe hayo, kwa mfano, baadhi ambao wameuziwa viwanda, kwa mfano, Kiwanda cha Magunia na Kiwanda cha Ngozi, hawakutekeleza vizuri yale ambayo walikubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha waziwazi kwamba, zoezi lolote la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma haliwezi kufanyika haraka haraka kama tulivyotazamia. Kwa hiyo, hii ni moja ya mambo ambayo nadhani inabidi yatazamwe. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu katika ubinafsishaji kuna matatizo ya mabadiliko ya hali ya uchumi ambayo yamefanya baadhi ya malengo yaliyowekwa yasiweze kutekelezwa. Hili ni moja ya jambo ambalo inabidi tulitazame kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzito wa kazi ya Tume hauwezi kupimwa kwa idadi ya Mashirika, unaposema kuna Mashirika 400 na yatabinafsishwa kwa hiyo ukayapima kwa namba, hii nadhani si sahihi, kwa sababu kila Shirika lina uzito wake. Kwa hiyo, ni vizuri hata tunapozungumzia muda tuwe tunaangalia uzito wa kazi kwa kila Shirika ili tuweze kutoa muda ule ambao unahitajika. Mathalan kulikuwa na Mashirika 400, yamebaki Mashirika 77 hayajabinafsishwa. Je, ni sawasawa nikisema haya Mashirika 77 yaliyobaki ndiyo yenye kazi nyingi zaidi? Kwa hiyo, kuweka muda wa miaka minne ni sawasawa na Mashirika mengine hayo yaliyobinafsishwa ambayo pengine hayana uzito zaidi unaweza kuleta matatizo mengine ya kiutekelezaji. Kwa hiyo, mimi nadhani kazi hii inatakiwa kwa kweli ipimwe vizuri sana na uzito wake haujionyeshi waziwazi katika kuomba huo muda kwa sababu hakukuwa na *Action Plan* au *ActionPprogramme.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka wakati tunashughulikia kuongeza muda wa *Consolidated Holding Corporation* tulisema Serikali inapokuja kuomba kuongeza muda ni vizuri wakaja na *Action Programme* ya kusema kazi hizi zitafanyika kwa namna hii, mwaka wa kwanza itafanyia hii na hii. Kwa hiyo, pengine huu muda wa miaka minne tunaoupitisha hapa hautoshi kuweza kufanya kazi hiyo. Nasema hivi kwa nini? Ukichukua Shirika kama la *TANESCO*, ukichukua Shirika kama la Reli, huwezi

ukalipima sawasawa na Kiwanda cha Magunia haiwezekani, kwa hiyo suala la namba hapa kwa kweli haliingiliani. Kwa hiyo, nadhani tusishughulike na namba tutazame kazi iliyobakia, kazi iliyobaki ninavyoona ni nzito na huu muda wa miaka minne hii ambayo mimi ninaiunga mkono, tunakubali kwa sababu kazi ya kufanya ipo. Lakini nadhani Serikali ingetutengenezea *Action Plan* ambayo inaeleza kila Shirika lina uzito gani wa kazi na itatekelezwa kwa muda gani ili kuweka kinga katika kipindi ambacho tumekitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kazi nyingine ambayo inabidi tuitazame Sheria yenyewe iliyounda Tume. Nadhani kuna haja ya kuitazama ili kuweka bayana majukumu kati ya Tume na Wizara za Kisekta. Kwa sababu inaonekana waziwazi kabisa kwamba, Tume imeachiwa kazi nyingine, ibinafsishe halafu iende ikafuatilie utekelezaji wa majukumu, nadhani kazi ya Tume ingekuwa ni ufuatiliaji wa mikataba, lakini ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ufanywe na Wizara za Kisekta. Hili lingewekwa waziwazi katika sheria ili kila mmoja ambaye atarudi nyuma aweze kupimwa kwa jinsi alivyoweza kurudi nyuma kuliko kuiachia kazi yote *PSRC* wakati mambo mengine ni Wizara ambazo hazikutekeleza majukumu yake lakini lawama inakwenda *PSRC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa maoni yangu haya ambayo nadhani yanazidi kuboresha utekelezaji wa Azimio hili la kuiongezea *PSRC* muda wa miaka minne na ninaunga mkono Azimio hili kabisa. Ahsaante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimwita Mheshimiwa Freeman Mbowe, nasikia yuko kwenye Kamati. Sasa nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wapo niwasome wote ili ambao hawapo waliko wakatafutwe kwa sababu tukishampita mtu mimi sitarudi tena, tuna *pressure* ya *time*. Kwa hiyo, mtu asipokuwepo mimi naona tumeokoa, lakini Mheshimiwa Freeman Mbowe kokote alipo mtafuteni kwa sababu nilikuwa sijasema. Mheshimiwa Aggrery Mwanri, atafutia sasa kwa sababu Mheshimiwa Freeman Mbowe hayupo. Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Semindu Pawa. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Aggrey Mwanri.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu suala la kuongeza muda wa *PSRC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipati matatizo kuelewa jambo hili. Kinachosemwa hapa ni kwamba, *PSRC i*lipewa majukumu mazito, Mashirika ya Umma ni Mashirika ambayo ndicho kitambulisho cha Watanzania *(Public Enterprise),* ambayo unaipata kupitia jasho la wananchi na unapoambiwa ufanye kazi ya kubinafsisha hayo Mashirika ambayo yamepatikana kwa jasho la wananchi, kazi hiyo haiwezi kuwa nyepesi. Ndiyo maana tunawasikia Watanzania wakipiga kelele katika Mashirika ya aina mbalimbali. Kwa sababu dunia ingetushangaa sana kusikia sisi Watanzania tumefika mahali tukaamua kwamba, sawa uza Mashirika yote, binafsisha, hakuna mtu anayepiga kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu hilo jukumu la kwamba unauza Shirika ambalo limepatikana kwa jasho la wananchi, kazi hiyo haiwezi kuwa ni kazi ya siku moja au mbili, itakuwa ni kazi ambayo inahitaji ukae chini utafakari, ueleze, ufanye mdahalo watu waelewe halafu baadaye ubinafsishe. Leo sisi hapa hatuzungumzii *logic* ya kwa nini Mashirika haya yanabinafishwa au kwa nini yasibinafsishwe, hiyo siyo *issue*, hiyo *debate* ilishafungwa kwa maana ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambacho kimepata ridhaa ya wananchi katika nchi hii ya kuongoza nchi hii na kusema kwamba, sisi falsafa yetu ya huko nyuma ilikuwa ni falsafa yenye mwelekeo wa kijamaa, lakini tumefika mahali tunasema sasa tunaelekea kwenye mwelekeo wa kibepari hakuna tabu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliyesimama hapa ni Mbunge ninayetokana na Chama cha Mapinduzi, niliwahi kumwambia wananchi wa Tanzania katika Jimbo langu la Siha kwamba, mkituchagua sisi Mashirika haya ambayo tumeona yamekuwa ni mzigo kwenu tutayabinafsisha, *there is no question about that,* wala mimi sipati tabu, Mashirika haya yalikuwa ni *Public Enterprises. A Public Enterprises managed by the private minded manager,* yakafika mahali yakashindwa kufanya kazi. Sasa unasema mimi nataka *private* ambayo itakuwa na mtu *private,* ambaye atafanya kazi kwa ajili ya *private* na *logic* yake inajieleza waziwazi ndani yake utapata kodi ya Serikali, ndani yake utapata teknolojia ya kisasa, ndani yake utapata gawio na ndani yake watu wataajiriwa. Sihitaji kwenda Chuo Kikuu kuelewa hilo. Mimi nasema hivi, ukifika mahali ukasema haya Mashirika nimeona yamekuwa mzigo yaachie, huwezi ukaendelea kuwatoza kodi wananchi wa Tanzania, unawaambia lipeni kodi kwa ajili ya kuendesha *scrap* yakaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema yako maeneo ambayo kwa kweli nasema kabisa kwamba, hayakuridhisha. Lakini katika hili nasema kwanza kabisa, naunga mkono wazo la kuongeza muda wa *PSRC.* Kwa nini nasema hivyo? Ufanya kama hutaki kuongeza muda, useme mimi siko tayari kuongeza muda kwa sababu muda huu umekwisha basi na Shirika hili limemaliza kazi yake liondoke, hiyo kazi nyingine iliyobakia iendelee, unafanyaje? Maana yake utatakiwa sasa utafute Tume nyingine mpya kama Tume hautaipata utakachotakiwa kufanya ni kuzikabidhi hizo Wizara zinazohusika zifanye kazi ya kubinafsisha ambayo ni ngumu sana. Itabidi muda sasa utafutwe kwa sababu utahitaji watu wenye *experience* hiyo na utahitaji upate muda wa kufundisha watu namna ya kubinafsisha. Kwa hiyo, utakuta kwamba, itatugharimu sana. Nashauri kwamba, ni vizuri *PRSC* ikaongezewa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo sikuridhika nayo, mojawapo ni la wafanyakazi na Mheshimiwa Abdallah Kigoda, naomba unisikilize vizuri. Mimi sikufurahishwa sana na namna ambavyo wafanyakazi katika Mashirika haya ambayo yamebinafishwa, mambo yao yalivyokuwa *handled*. Mimi sidhani na hapa *I want to be critical*, tulijua kwamba, Mashirika haya ya Umma yanabinafsishwa na tulijua kwamba itamaanisha kwamba watu wengine wataachia ngazi wataondoka. Mheshimiwa Marehemu Kinyondo, alikuwa anasema ni mkono kwa mkono, kisogo kwa kisogo, nilikuwa namsikiliza wakati huo akiwa Waziri wa Kazi na Mendeleo ya Vijana, ndivyo alivyosema na hundi yake unamkabidhi pale anaondoka nayo.

Lakini katikati hapa tulichokiona ni maandamano ya wafanyakazi wanapiga kelele hawajalipwa haki zao. Sasa hatuwezi leo tukasema tunaruhusu *PRSC* iende bila kuipa hilo jukumu la kuona kwamba wanapofanya kazi ile lazima wa-*put into account* suala la maslahi ya wafanyakazi halafu waondoke, *otherwise* tutaonekana ni watu wa ajabu tu hapa, tunapitisha jambo hivi hivi, tunajiendea halafu watu wako barabarani wanaandamana, haiwezekani. *TANESCO* wapo barabarani, *TTCL* wapo barabarani, watu wazima. Wanatuambia kwamba, pensheni zilikuwa zinachukuliwa kwenye mishahara ya wafanyakazi, *good talk*. Sasa ulitakiwa wewe kama Serikali umwambie wewe umekusanya fedha za makato ya wafanyakazi, amekata mishahara ya wafanyakazi alitakiwa aipeleke *NSSF* hakuipeleka kule, Shirika limefika mahali linabinafishwa. Sasa sisi hapa hatuwezi kusema ni sawasawa tu hata kama walikatwa lakini hawakulipwa ni sawasawa hii,itutaambiwa ni *logic* ya wapi? Wafanyakazi wale walitakiwa uwape haki yao na kama kazi ile haikufanyika kwa Shirika lile la umma *under supervision* ya Serikali. Kwa hiyo, tunaomba tunapowapa hili jukumu kabla ya kubinafsisha, waone kwamba wafanyakazi wanaohusika katika lile Shirika haki zao zinalindwa. *(Makofi)*

La mwisho, sababu kazi hapa ni kusema kwamba, tunaongeza muda na mimi nimeseme *in principal,* ninakubaliana na hoja ya kwamba lipitishwe Azimio hili. Pale *West Kilimanjaro* katika Jimbo langu la Siha, yapo mashamba ya *NAFCO*, kila siku ninampigia kelele Mheshimiwa Waziri, namwimbia mzee wangu, mashamba haya yako chini ya Serikali, wako wananchi 22,000 pale *West Kilimanjaro,* ambao Serikali imesema kwamba, kabla ya zoezi la kubinafsisha mashamba ya *West Kilimanjaro,* watahakikisha kwamba, *squatters* wanakuwa *resettled.* Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro yuko humu ndani, anafahamu jambo hili, *PSRC* wanalifahamu jambo hili, Mheshimiwa Abdallah Kigoda analifahamu jambo hili na Serikali inalifahamu jambo hili.

Nasimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha kusema kwamba, kubinafsisha mashamba ya *West Kilimanjaro,* mashamba yaliko kule Matadi, bila ku-*put into account* suala la wananchi wa Siha ambao ni *squatters* waliokwenda kule wakati wa ukoloni, *it would be glossily unfair.* Hili nalisema kabisa wala siyo kama nataka ku-*politisize* na nina *assurance* ya Mheshimiwa Waziri na Serikali na ninauliza swali ninataka nipate majibu. Ni kwa nini zoezi hili linaonekana kama linachukua muda mrefu kiasi hicho?

Wakati huo huo nina taarifa kwamba, kuna Makampuni yamekwenda kule kupima na kujua hawa watakaa wapi na hawa watakaa wapi. Mimi kama mwakilishi wa wananchi na Madiwani wao mpaka sasa hivi ripoti ile inayosema mapendekezo hayo hatujaipata. Nimeulizia ulizia na *PSRC* wanajua. Naomba watakapokuja kule Siha, *West Kilimanjaro,* ni vizuri wakakaa na sisi wakajua mawazo yetu tunasema nini kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda ni rafiki yangu, nataka kui-*declare interest* yangu wala usiwe na wasi wasi, mimi nilisharuhusu miaka mingine minne mzee wangu ipite. Chonde chonde na kufanya maamuzi haya kwa maana yake mimi nilitaka *politically* ni-*survive* na Chama changu cha Mapinduzi ki-*survive.* Kwa hiyo, naiomba Serikali ione

hilo, isifanye ubinafsishaji katika Siha bila ya kuhakikisha kwamba, wananchi wote wale wa Siha, ambao waliomba makazi ya kudumu hawajapata maeneo hayo. Nina hakika hili sisemi kwa ajili ya wananchi wa Siha tu, ukienda Hanang, Mbeya utalikuta na hata Tanga utalikuta. Narudia tena kusema kimsingi mimi sina tatizo na hoja hii. Siwezi kuzuia *PSRC* isipewe miaka ile minne kwa sababu isipopewa maana yake zoezi zima litasimama halafu nitaambiwa wewe ndiyo uliyezuia. Mimi nabariki hili jambo lipite wala sina ugomvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nianze kwa kuunga mkono na nitumie dakika kama 5 au 6 katika kuchangia.

Hoja ya *PSRC* imeletwa wakati muafaka. Maana wakati ule tulipokuwa tunapitisha tuliipa miaka minne na kusema kwamba tunaweza tukaongeza na tulivyojua kwamba muda unakwisha na kazi bado zipo, kwa hiyo tulijua wazi kwamba kuna kuongeza muda na wakati Serikali ilipoleta, imeleta wakati muafaka na wala haikuleta kwa haraka haraka.

La pili, nilikuwa nashauri wakati ule *PSRC* imepewa miaka minne, ijaribu kutazama Mashirika ambayo ni nyeti na roho ya Watanzania katika kuyabinafsisha au kupangisha wasifanye makosa kama walivyofanya makosa katika baadhi ya Mashirika au Makampuni. Wanapotazama kwa mfano reli, viwanja vya ndege, sina uhakika nadhani Posta huwa haibinafsishwi kwa sababu ile ni roho ya wananchi, unaweza ukapinduliwa kutoka hapo. Lakini Mashirika kama vile *TANESCO* kama unaona kuna utata kwa nini wasiruhusu watu binafsi waanzishe Mashirika yao ya umeme badala ya kung'ang'ania *TANESCO* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa miaka minne inapoendelea, ninawaomba Watanzania hawa wenye kupewa chombo hiki wajiingize zaidi katika uzalendo. Wajaribu kuchambua mambo kwa uyakinifu zaidi, watumie utaalamu na sheria, lakini kubwa zaidi wawe wazalendo kwa nchi yao kwa sababu hatutegemei kwamba, hawa wanaobinafsisha ambao tumewapa kazi hii ni malaika, lakini nao wanapofanya kazi hiyo wajaribu kutazama mbele kwamba, wana watoto wao, wajukuu zao na ndugu zao wale hawatakwenda Burundi, Rwanda wala mahali popote, watabakia hapa. Kwa hiyo, wasiweke kisasi cha Watanzania dhidi ya damu yao wenyewe. Wafuate uzalendo zaidi kuliko mambo mengine ambayo sisi Watanzania yanatuchanganya changanya sana vichwani, tunaacha uzalendo tunafuata ubinafsi.

Lakini nilikuwa nadhani kwa upande wa wale waliopewa dhamana kupeleka michango ya wafanyakazi *PPF* au *NSSF* na hawakupeleka, wakati utakapofika wa kubinafsishwa kama bado wapo kwenye Mashirika hayo hawa wasilipwe chochote, lakini Serikali ichukue gharama yote ile ambayo haikupelekwa ili wafanyakazi wapewe fedha hizo mapema badala ya kukaa wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusiana na mashamba. Mnapofika kubinafsisha mashamba muwe makini sana msije mkatuwekea Zimbabwe ya Tanzania. Muwe makini kweli. Kuna mahali pengine sina uhakika kama masharti yalifuatwa watu walipewa tu kwa sababu ya ujanja ujanja na wananchi wakabaki wanahangaika. Naishukuru *PSRC* ilipokuja Mkoa wa Rukwa nadhani mwezi Aprili, kwa upande wa Nkasi ilitazama Shamba la Kalambo, ilikaa na viongozi na baadhi ya wananchi tulipeleka timu, kazi ile waliyoifanya ni nzuri na naipongeza pamoja na shamba la Malonje. Nkasi ina mashamba mawili moja limekwishachukuliwa. Limechukuliwa vipi, binafsi sifahamu, Wilaya na Halmashauri yangu hawafahamu na hata Mkoa haufahamu, kwa sababu tulisikia limeshachukuliwa. Sasa pamoja na kwamba, wananchi wa Nkasi na eneo la Sumbawanga Mjini, vijiji kama vile vya Sengelesha, Nkundi, pamoja na Kalambo yenyewe, ikiwa ni pamoja na Kalundi, walihitaji eneo si kubwa sana, dogo na wakaahidiwa na wakubwa kwamba watamegewa. Hawakusikilizwa wala hawakufikiriwa likachukuliwa tu. Sasa *PSRC* mnaposhughulikia mashamba mjue roho ya Watanzania ni mashamba na ni ardhi . Hilo muwe makini sana sana msije mkanyang'anya haki za wananchi kama baadhi ya haki za wananchi fulani maeneo mengine zilivyoweza kunyang'anywa.

Mwisho, Kamati ya Bunge inayohusika na Shirika linapochukuliwa katika sekta zilizopangwa, pengine hata katika hatua ya mwisho si vibaya au katika migogoro ile ikashirikishwa na ikafahamu kinachoendelea. Hilo litakuwa zuri zaidi na tutakwenda pamoja.

Baada ya kusema hayo nazidi kuunga mkono kwamba waongezewe muda ili wachape kazi kikamilifu kwa makini na hasa kwa kuzingatia uzalendo sio mioyo ya juu juu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe mchango wangu mdogo katika hili Azimio la kuiongezea muda *PSRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijasahau, naomba nianze kwa kuunga mkono kwamba hawa *PSRC* waongezewe muda huo wa miaka minne. Lakini vile vile naomba nikipongeze Chama Tawala, pamoja na Serikali, kwa kuwa na sera yenye mwelekeo mzuri. Tumemsikia ndugu yetu hapa Mheshimiwa Mwanri, ambaye amekuwa Mwalimu wa Siasa, naamini ametueleza vizuri tu. Kwamba kazi ya kubinafsisha Mashirika ni kutokana na ile sera tulipoona kwamba haitufikishi mbali lazima tubadili mwelekeo na huu mwelekeo tuliobadili ndio unaotupelekea kwenye hayo mafanikio. Taarifa iliyotolewa na hata mengine yaliyozungumzwa na wenzetu waliotangulia ni kwamba, *PSRC* imefanya kazi nzuri jamani, tunapaswa kuipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shellukindo, amesema hawa watu walianza wakiwa hawana ujuzi, ni kweli. Wakati wanaanza tusichukulie kana kwamba, walianza wakiwa wamejifungia kwenye chumba chao na mawazo yao peke yao, hapana. Walikuwa wana maelekezo ya Serikali lakini vyombo mbalimbali vya Kimataifa vilisaidia katika kutoa mafunzo ya

namna ya kubinafsisha. Kama nitakuwa nimekosea Mheshimiwa Waziri, atanikosoa na wengine ambao wanajua zaidi yangu, niko tayari wanikosoe. Nafikiri Benki ya Dunia ilikuwa imehusika. Sasa mambo yaliyofanikiwa ni kwamba, baadhi ya Mashirika yalikuwa yamekufa lakini leo yamefufuka, ajira zimerudi na watu wanafanya kazi na mishahara wanapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma ilikuwa baadhi ya bidhaa hazipatikani na wala hujui utapata wapi. Sabuni ilikuwa ukisikia ni foleni, ukisikia sukari ni foleni. Leo hii mama anabandika sufuria anamtuma mtoto nenda kaniletee sukari. Ukizungumzia suala la sabuni, ni wewe unataka sabuni gani. Ziko sabuni za aina nyingi. Sasa hayo ndiyo mafanikio ya *PSRC.* Mafanikio mengine ni mapato, Serikali imeweza kupata mapato ya kutosha tu na leo hii Serikali imeweza kufuta hata kodi ya maendeleo, hayo ni mafanikio madogo? Leo hii hata kama Wabunge tunakwenda katika Majimbo yetu tunajidai kuwa mafanikio ya Serikali ni pamoja na kufuta kodi ya maendeleo. Nayo imeletwa kutokana na hili. Sasa lawama nyingi zimetolewa kwa *PSRC. PSRC* inafanya kazi ya uratibu wala haibinafsishi na hili amelieleza Waziri na katika taarifa limeandikwa. Tulipaswa kuwa tumeliona. Katika kuingia mkataba wanaofanya mkataba ni Serikali, mle ndani wakati wanapofanya mipango ya ubinafsishaji *PSRC* inakuwepo, anakuwepo Mwanasheria na anakuwepo mwakilishi wa Wizara, hawawi *PSRC* peke yao. Kwa hiyo, hili nilikuwa naomba tuliangalie. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa naunga mkono nasema hawa watu waongezewe muda ili waweze kufanya kazi ya kumalizia hayo Mashirika 77 yaliyobaki, pamoja na kushughulikia Mamlaka za Udhibiti. Hili suala la kuweka Mamlaka ya Udhibiti kutokana na hizi huduma zitakazokuwa zinafanya haya Mashirika, hili ni jambo geni kwetu. Si kitu ambacho kinaweza kikafanywa haraka haraka, kinatakiwa kifanywe kwa makini. Kinatakiwa kifanywe na watu wenye uzoefu, watu wenye taaluma na hakuna wengine isipokuwa ni hawa watu wa *PSRC* wamefanya kazi nzuri katika nchi hii. Pamoja na kufanya kazi nzuri nchi nyingine zimekuja kujifunza kwetu. Hili ni jambo dogo? Lakini vile vile hata Benki ya Taifa imewasifu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba waongezewe muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo ambayo ninaomba yatazamwe ni kwamba, katika baadhi ya Taasisi na vitu vilivyobinafsishwa kuna vingine vimeshindwa kuendelezwa kama mkataba unavyotaka. Sasa nilikuwa naomba sheria itazamwe upya kuona kwamba pale ambapo mkataba utakuwa umeshasainiwa na Mwekezaji ameshachukua ile mali lakini hajaendeleza kama ilivyokubalika katika mkataba, basi itazamwe ni namna gani kama ameshindwa ili Serikali iweze kuchukua ile mali na kuweza kutafuta mwekezaji mwingine. Hapa kumetolewa lawama kwamba, kuna baadhi ya mali zimeuzwa kwa bei ya chini. Lazima tuielewe hapa kwamba, tunauza au tunabinafsisha kwa hiyo, ni utashi wa mtu anayetaka kuchukua hicho kitu kama hakupatikana au amekubali kwamba mimi nitachukua hiki kitu kwa shilingi 10,000,000, kesho anasema mimi sitaki, je, mtamlazimisha kwamba lazima uchukue? Itabidi utafute mwingine ambaye yuko tayari. Mwingine anakwambia mimi nipo tayari lakini hayuko tayari kukupa shilingi 10,000,000 unafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine mzuri tuna kiwanda chetu kile cha *SPM Mgololo.* Kwa muda mrefu kimekosa mtu wa kuwekeza. Lakini vile vile tunaambiwa kuna madawa yako pale ya hatari kama hayakuweza kushughulikiwa vizuri yanaweza yakaleta hatari kwa maisha ya watu, tunafanyaje? Nilikuwa nimesoma kwenye gazeti tumelazimika kuuzia mtu kwa thamani ya dola moja, lakini tumefanya hivyo ili kukiokoa kile kiwanda ili hayo madhara yanayodhaniwa kuja kutokea yasije yakatokea, lakini vile vile kiwanda kiweze kuanzisha *production*, bidhaa zipatikane, watu waendelee na ajira na Serikali iweze kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nataka kiangaliwe ni kwamba, kuna baadhi ya Mashirika wawekezaji hawajaonyesha nia ya kutaka kuyanunua au kuwekeza katika hayo Mashirika. Kwa mfano, kuna Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Company Limited*. Kile sina uhakika kama amepatikana mwekezaji mpaka sasa. Lakini tuna watu ambao wamekuwa wakifanya kazi pale kwa muda mrefu tu lakini kiwanda kipo katika hali nzuri. Wale wafanyakazi wamekuwa waaminifu, wanafanya kazi vizuri, hawajafanya hujuma katika kile kiwanda, wapo. Nilikuwa nasema kwa baadhi ya Mashirika au Viwanda kama hiki, Serikali iangalie kama vinaweza vikabinafsishwa kwa utaratibu wa *Management and Employment Buy Out (MEBO).* Wafikiriwe wapewe na mtaji kwa sababu ujuzi na uzoefu wa kufanya kazi wanao, waweze kukiendeleza. Nilikuwa naomba hilo kama linaweza likaangaliwa basi liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna Mashirika mengine yaliyobakia. Mashirika haya makubwa, ninaamini katika utaratibu wa kuleta wawekezaji kuna wengine watakapokuja watakuja na *interests* za zile shughuli za biashara tu. Zile ambazo zitakuwa hazina mwelekeo wa biashara ambazo ni *non-core assets,* hawatakuwa na *interests* nazo. Kwa mfano, majumba, viwanja ambavyo havijaendelezwa mpaka sasa, nilikuwa nasema kwa upande wa viwanja hasa kwa Shirika la Reli na Serikali watakapokuwa wanabinafsisha, naomba kwa upande wa viwanja basi wafanye hivyo kwa kushirikiana na Mamlaka za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, kuona je, hizi Mamlaka zenyewe hazina mahitaji ya hiyo ardhi ambayo imeachwa na haya Mashirika. Itakuwa si vizuri unatoa kiwanja kwa mtu wa Dar es Salaam kiwanja ambacho kiko Dodoma wakati Manispaa ya Dodoma na yenyewe inahitaji kiwanja hicho hicho kwa matumizi yake.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba wakati mtakapokuwa mnashughulikia vitu kama hivi hasa viwanja, hilo litazamwe na naomba niwe wazi hasa kule kwa upande wa Manyoni pale Itigi, tuna sehemu kubwa tu ya viwanja vya Shirika la Reli havijaendelezwa. Sasa mnajua mwekezaji atakayekuja atakuwa hana *interest* ya kusema ataendeleza vile viwanja, nina uhakika kabisa, hatakuwa na *interest* kwa sababu hata ile Shule ya Msingi ambayo ilikuwa inaendeshwa na Shirika la Reli, ameshaonyesha nia ya kwamba yeye hataki kushiriki labda kama mazungumzo yatafanywa. Kwa sababu ule mji unakua na hatuna eneo zuri la kuweka stendi, sisi tungependa lile eneo tulitumie kwa stendi ya magari ya abiria. Kwa hiyo, wakati wa kubinafsisha kwa kweli tutashukuru kama na sisi tutahusishwa ili tuweze kuonyesha mahitaji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja na ninakushukuru sana , ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru wewe na niwashukuru wote waliochangia. Mimi nitachangia mambo machache tu.

La kwanza, ni kueleza tu kwamba, sera ya ubinafsishaji ni sera ya Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi kina tabia ya kujikosoa na kukubali kukosolewa. Ni sera yake ya ukweli. Katika mapendekezo na hoja za Wapinzani ndugu zetu kuna mazuri, mengi waliyosema tumeyasikia. Chama cha Mapinduzi kina tabia hiyo ya kukosolewa. Jana nashukuru sana nilihudhuria kikao cha Kamati ambayo imejadili hoja hii. Waziri alisema yale yote ambayo tuliyajadili pale aliyazingatia. Ninaamini kabisa na mengi yamezungumzwa katika hoja za ndugu zetu. Sasa naomba hii hoja iliyoletwa eti tuiingize kinyemelanyemela, mimi nashauri sio wakati muafaka. Tukubaliane wazi kwamba, kwa kweli haitatusaidia, kikubwa ni kuiomba *PSRC* na Serikali ikubali yale mapungufu yarekebishwe na tumeahidiwa yatarekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika nia hiyo hiyo ya kuishauri Serikali, nitazungumza mambo machache na pengine ili nisizungumze kwa kirefu, nichangie kwa kutoa mawazo. Kwanza, ninao wasi wasi kidogo kwamba kwa maamuzi ya kuongeza muda kwa *PSRC* ni maamuzi sahihi na mimi naunga mkono. Lakini Serikali ikubali wazi kwamba katika kipindi kifupi kijacho kwa sababu Mashirika yaliyobaki ni machache *PSRC* itakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali. Ukiangalia urari wa mahesabu wa *PSRC* kwa mwaka 2002 utaona wazi kwamba, kwa sasa hivi wameanza kuingilia fungu lile la Mfuko Maalum. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaandaa vizuri na kwa sababu kazi ipo na hatuwezi kukimbia ni sera ya chama chetu, ni budi tukubali Shirika hili lina uzoefu hatuwezi kuanza upya tutakuwa ni watu wa ajabu sana. Kwa hiyo, nashauri ni kama mzigo kwa hiyo uchukuliwe kama tahadhari katika Bajeti ya Serikali. Nasema kwa sababu Mashirika 77 yaliyobaki si lazima *PSRC* ichukue miaka minne inaweza ikachukua miaka mitatu, miwili, lakini sisi tukubali kwamba, kwa miaka minne ni kipindi ambacho kitatosha kwa ajili ya kuifanya kazi iliyobaki. Lakini kwa sababu itakuwa ni mzigo wa Serikali, ninashauri kwamba waangalie hivyo, kwa sababu ni mzigo basi muda ikiwezekana upungue.

Halafu ni vizuri pia tukaangalia katika yaliyosemwa kwa wenzetu. Wala si kitu cha ajabu walichokisema kwamba kuna mapungufu. Upungufu mkubwa waliousema ambao hata sisi Wana-CCM tunauona ni suala la uwazi na uwajibikaji. Hakuna anayelikataa hilo. Sasa uwazi utakujaje? Uwazi utakuja tu kwa kitu rahisi. Mimi sioni umuhimu wa kuiangalia hata hiyo Miswada kama ilivyosemwa hapa. Lakini tunasema utaratibu wa ubinafsishaji ndio unaotakiwa uwe wazi zaidi. Kwa hiyo, ili kwa kweli tuwe wazi zaidi na tusaidie Mashirika yetu, napendekeza mambo mawili: Kwanza, ile *Public Corporation Act* ambayo iliipa madaraka *PSRC* iangaliwe kidogo hasa katika eneo la ku-*specify* Mashirika ili wakati wa *specification* usiwe mrefu na usiwe *inevitable.* Kwa hiyo, *PSRC* ibanwe kwamba wanaruhusiwa kulisimamia Shirika na kuanza kulibinafsisha pale inapoonekana imeiva wasili-*specify* mapema hatimaye kulifanya Shirika lisiwe na

uwezo kabisa hata wa kukopa. Kwa sababu linapokuwa *specified* haliwezi kufanya kazi nyingine bila kufuata kanuni na taratibu zinazoelezwa na *PSRC*.

Kwa hiyo, hii iangaliwe na itatusaidia sana katika uwajibikaji. Halafu pawepo na uwazi kwa kuwa na chombo cha kuangalia mikataba na hili si geni, tunacho chombo kama *LART, Consolidated Holding,* wanaweza wakapewa jukumu la kufuatilia mikataba tuliyowekeana na wenzetu kama wanaitekeleza kikamilifu na chombo hicho kikaja kikaripoti Bungeni. Mimi nashukuru kwamba, Waziri jana alitamka na kimsingi akasema jamani hayo yote mliyoyasema tumeyasikia tutayaangalia. Sasa sioni hitilafu ya kukubaliana. Napenda kusema kwamba, Chama cha Mapinduzi na sera zake tunakubali kukosolewa na tuko tayari kujikosoa na kujisahihisha, lakini tukubaliane hatuendi kwa kubadilisha sheria taimu za mwisho. Tukubaliane wazi kwamba, mapendekezo yaliyotolewa yanaweza yakawa ya msingi, Serikali iangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nashukuru sana kwa utayari wa Serikali kukubali kubadilika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia katika Azimio ambalo Waziri amelileta. Awali ya yote, mimi sipingi ubinafsishaji, pamoja na mambo mengine kwamba ubinafsishaji ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, sidhani kama katika Ilani ya Vyama vya Tanzania au katika Katiba zake kuna chama ambacho kinasema sisi hatukubali ubinafsishaji, hatukubali ubinafsishaji. Kama kipo sijui ni cha nani? Kwa hiyo, hoja hapa ya ubinafsishaji ni sera ya chama fulani, nadhani sio sera ya nchi tu ni nchi zote katika dunia zinaelekea huko hata Uchina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja ya msingi tunazungumzia namna na jinsi zoezi zima linavyofanyika kwamba halitendi haki. Katika Kuran Tukufu, Mtume Muhammad anasema: “Mnafiki ana sura tatu”. Sitaki kuzitaja sura hizo wale waliosoma Kuran wanajua. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Zitaje tu.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Kamati imesema, sisi wote hapa tunasema, Watanzania wanasema kwamba, imefika mahali *PSRC* na wale wanaohusika kwa kweli inafika mahali wanaiweka mahali pagumu hasa Serikali yenyewe. Kwamba, katika mikataba ambayo mnaingia hamfanyi uwazi au ukweli, mnafanya mambo ambayo baadaye yanatuletea matatizo. Sasa tukijadili hilo na tukasema tulirekebishe hili, mtu mwingine anasema pale kuna matatizo, kuna matatizo. Kwa mfano, kama kuna watu wamekwenda pale kwenye mambo ya *TTCL* kusaini ule mkataba hewa. Yuko mtu wa *PSRC* namjua. Huwezi kwenda kusaini mkataba bila aibu na mtu anaweka masharti kwamba, Mjumbe wa Bodi fulani huyu asiwekwe, awekwe fulani, unaweka kwenye mkataba nani anateua Wajumbe wa Bodi wakati wewe umeshawateua kwenye mkataba. *(Makofi)*

Serikali maana yake ni siri kali. Kuna siri nyingi, kuna uchafu mwingi. Maana unaweza kufika mahali mkaumbuka hivi hivi kwa sababu tu tunaacha hii. Lakini yako mambo mengine tukiyaleta hapa hadharani kuna watu wataumbuka. Imefika mahali sasa hivi *TTCL* walikuwa wanasema wanaandamana. Umeweka kwenye mkataba kwamba, mtawauzia hisa, sasa unataka uwaondoe kazini hisa zao hujawauzia au hujawamilikisha. Tumekubaliana kwamba, hawa *TTCL* na *PSRC* wanajua watajenga njia 840,000 halafu watajenga hizo *landline* kuzipokea, Shirika lingine likapewa kazi hiyo na wakaifanya mpaka mwaka 2005. Hamkufanya halafu mmeweka ukiritimba na Mashirika mengine mmeyazuia.

Mimi ninavyozungumza mkataba huo unasema kila Kijiji chenye watu 3,000 kilipaswa kupata simu. Halafu Wabunge tunakaa hapa tunauliza kwangu simu inakwenda lini, tunauliza hapa halafu tunasema haya ni mambo ya uchafu. Halafu mtu anasema hili pendekezo tulikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yana utata wake. Ndiyo tunasema ipite na mimi nimesema sipingi. Hiyo miaka minne tutawapa kwa sababu hatusemi zoezi lisitishwe. Tukisema lisitishwe lazima kuwepo na mtu. Sasa mtu gani, tuunde chombo kingine hatuwezi kurudi na kuunda chombo kingine. Ila hawa tunasema tuwaambie kwamba tuna *see concern.* Nchi hii ni yetu sote na Mashirika haya ni yetu sote, yalijengwa kwa nguvu zetu sisi sote. Sasa tunalipa madeni, tuna mzigo wa kulipa madeni wasingetupunguzia tungelikuwa kwenye umaskini ambao sijui ukoje halafu tunacheka. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kama kila mmoja hapa anachangia huduma za elimu, afya, kwa sababu Taifa linadaiwa madeni ya mabilioni, sasa tunakwambia tubinafsishe pale unafanya maslahi yako. Halafu sisi Wabunge tunakuwa kama mtu umezaa mtoto sasa anasema baba nataka kuoa, unampa ruhusa, halafu anasema nataka fedha za mahari unampa, wakati wa kufunga ndoa hakuiti na mkamwana hakuonyeshi, hivi unafanya nini? Amemficha huko ameleta mpaka sijui ameleta nini. Sasa haiwezekani kwenye kuongeza muda wanaita tena Wabunge. Wanaleta dakika za majeruhi. Tumekuja hapa kwenye *briefing* Jumatatu iliyopita, tungeambiwa kwamba hii itakuwepo. Lakini kwa sababu wanajua wamekwishachoka tuwapelekee wasijue. Sasa utaratibu huu kwa kweli tufike mahali tukubaliane kwamba, ninyi mnaofanya hayo mnayoyafanya sitaki kuwarejesha kwenye hadithi za Alfu Lela Ulela, siku 1001Mfalme alitumia njama akawatuma watu waibe mkia wa jini ili apate mali. Alifanikiwa kutoka kwa bibi kizee na jini likamwambia ewe mwanadamu umefanikiwa kupeleka mkia wa jini na utajiri utaupata, lakini siku moja nitakuja na nitakushughuliki, na alimshughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa haiwezekani kabisa mnakwenda mnafanya mambo ya uchafu. Kwa hiyo, tunawapa tahadhari, mimi sipingi hapa tutakubaliana muongeze. Sasa nilikuwa napendekeza litakuja kwa wakati wake kwamba, hiyo mikataba kabla hamjakubaliana mlete hapa tuone kuna siri gani. Kuna vitu gani kule na nani anajifungua kwamba wakae *PSRC* peke yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo kwa kweli lazima tuwe *serious*. Wabunge hatuwezi kukaa kwani hivi sisi Wabunge tunafaidi nini? Tunasema *NBC* watu wana-*manouver* huku wanapitisha huku, wapite huku, Mheshimiwa Mbunge utanunua hisa utazinunua wapi, labda yule mmoja ambaye sitaki kumtaja hapa. Sasa wewe unawatengenezea wengine ulaji wewe ukishaacha Ubunge halafu unakwenda wapi? Lazima tufike mahali tuseme tunasimama hapa hata kama mimi siwi Mbunge kipindi kijacho, lakini nina haki zangu ambazo nilizisimamia hapa zikatekelezwa. Usione vyaelea vimeundwa, wewe unapokuwa hapa tunapopitisha maamuzi usiseme mimi kwa sababu nimekuwa Mbunge, tutafika mahali baada ya miaka 10 au 20 haya tuliyoyaunda *negatively or positively* yatatuathiri. Sasa sisi tunapopendekeza hapa yaongezwe kwa kuwa Wabunge wamekuwa wakilalamika.

Sisi tunapopendekeza hapa wanasema, yaongezwe kwa kuwa Wabunge wamekuwa wakilalamika. Nilileta hoja hapa ya *Privatisation Trust Fund,* Mheshimiwa Shekiffu, aliniunga mkono, Mheshimiwa Anna Makinda, japo hayupo hapa aliniunga mkono, Wabunge wote waliunga mkono japo Serikali baadaye ilipokonya *agenda* yangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule mtaani wanasema hivyo na ukichukua magazeti waandishi wote wanasema, hii ionekane hii. Watu wanakaa wanasema, hakuna kuchezea mikataba hapa ya Mashirika ya Umma. Halafu sasa mtu anasema, hii isiwekwe. Isiwekwe wapi! Inakula nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono na pale mwisho tunaweka hayo maneno, wakipitia Serikalini wawe wanatuletea *draft* angalau tunaona, halafu baadaye tunawaruhusu wataalam wanakwenda kufanya hivyo, vinginevyo tutapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilimwambia Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, nilitaka kuleta hoja hapa, wakaizima wakanidanganya eti kuna kesi Mahakamani ambayo ule mkataba wa *TTCL* ulikataa Mahakama za Tanzania, sasa sijui ni Mahakama zipi wanazozitambua. Niliwatania kwamba, nilitaka kuwapiga kwa fimbo ndogo humu, nitatafuta mpini. Saa ikifika na *I don't care,* kwa sababu *if you are prepared to fight you must be prepared to get fought; you have to be fought also.* Kwa hiyo, usidhani kwamba, ninaposema hivyo sijui madhara yake, ninajua, lakini tutayavumilia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa hakuna haja ya kuzungumza mara baada ya kuona mambo mengi yanakwenda vizuri tu, lakini upo umuhimu wa kuji-*register* kwa chombo kama hiki ambacho kiliwahi kulaaniwa kwenye magazeti na watu wa Tanzania waliwahi kusema kwamba hicho ndiyo kizingiti kikubwa na ilionekana kama vile ndiyo kinadumaza uchumi wa nchi hii, kumbe sivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Wanawake kwa muda wa vipindi vitatu mfululizo, nikaamua niingie Kamati ya Biashara na Uwekezaji, ili kwenda kujifunza mwenyewe katika maeneo haya. Nikakuta kwamba, kumbe siyo kizingiti, ni utaratibu na tabia na urasimu na masuala mengine ambayo yamejitokeza katika chombo hicho ndiyo yalisababisha haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kwanza ku-*clear out* tu mambo fulani fulani ambayo yamenukuliwa kwenye upande wa Upinzani. Mheshimiwa ali-*quote* ibara ya 7, bahati nzuri katika kuangalia ibara hiyo ya Ilani ya Uchaguzi inayozungumza hivyo ni Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 1995 na sasa hivi tunashughulikia ya mwaka 2000. Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 imezungumza kukodisha yale Mashirika mengine, ile ni Ilani yetu aliyoisema na tumeshatekeleza na watu wakatuchagua mwaka 2000. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shukrani kwa nafasi. Kwa utangulizi nilikuwa nimetaka kutumia Katiba, Sera za Chama Tawala, Uwajibikaji wa Chombo, Chombo Mbadala kama kipo, Mapungufu na Ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni siku ya *send-off,* siku ambayo mtoto wako anaondoka kwenda kwa mumewe, unamwelekeza mambo kwa siku moja ambayo atayatekeleza kwa muda mrefu. Utamwambia: "Mwanangu umetembea duniani kote, umetafuta wanaume wanene hawakujazwa, wembamba hawakupunguzwa, warefu hawakunyooshwa na wafupi hawakudidimizwa na ukatafuta weupe hawakugambuliwa na weusi hawakupigwa kwa rangi, umemteua huyu ndiyo wa kwako, ni kitu kimoja. Kwa hiyo, nendeni mkaishi Mungu atapitisha ya kwenu. Kwa hiyo, nyumba hiyo ihimili kila idadi ya watu, muwe wakalimu." Ndiyo mambo nitawaambia *PSRC*, kwa sababu sisi hatubadilishi sheria, tunaongezea uhai wa chombo hicho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa hivi siwezi kuinukuu yote, naomba tafadhali sana katika kifungu namba 63 (3) (d), kinachozungumzia wajibu wa Wabunge katika kupitia maazimio kama haya, ni kwamba, kuna utendaji na majukumu ya Bunge na majukumu ya Serikali kama vyombo imara ambavyo vina uhuru katika maeneo yao. Serikali itoe majukumu yake ya kufanya, sisi tubaki kama *monitors.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisiingie jikoni sana kuomba hata vijikaratasi vinavyoandikwa *PSRC*. Kwanza, *PSRC* niliwatajeni wakati niko Tanga, kwa sababu mara ya kwanza nilikuwa siwafahamu, sasa nikawatajeni kwamba, ninyi taarifa za mwaka mnazozileta kila wakati zilikuwa zina mapungufu katika mahesabu. Vile vile, taarifa ya utendaji wa mara kwa mara mnaotuletea kwenye Bunge hii ni uwazi na ukweli wa *PSRC* katika kuliwezesha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ingine lenye utata ni hili ambalo nilikuwa nafuatilia kwa haraka, Taarifa ya Kiongozi wa Upinzani. Katika ukurasa wa 8 amesema: "Kambi ya Upinzani inapendekeza *PSRC* ipewe mwaka mmoja." Halafu huku kwenye hoja ya Mheshimiwa Mutungirehi anasema: “Baada ya mwaka 2004 tuweke nukta.”

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mutungirehi, amekubaliana na miaka minne. Kwa hiyo, anampinga kiongozi wao. Ndiyo, kwa sababu kiongozi wao amesema mwaka mmoja, lakini yeye amesema miaka minne. Kwa hiyo, amekubali hiyo hoja ya *contradiction. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimesema leo ni siku ya *send-off,* basi nitatoa taarifa tu kwamba, mambo ambayo nitawaelekeza *PSRC* mkayafanye angalau yawe *registered* kwenye *Hansard.* Kwanza, punguzeni makongamano na warsha kwani sasa hivi Tanzania tunaelewa zaidi. Pili, punguzeni misafara ya nje, tulieni. Sasa hivi zindukeni mfanye kazi mlizokuwa mmetumwa. Tatu, migongano ya takwimu kati yenu *(PSRC)* na Hazina. Kuna malalamiko kwamba, wakati mwingine watu wanapokwenda *PSRC, PSRC* wanasema, hesabu tumepeleka Hazina. Hazina wanasema, tumepeleka *PSRC*. Kwa hiyo, kiwepo chombo Hazina, ambapo atakuwepo Afisa mmoja wa kuwajibu Wafanyakazi wanapofuatilia mafao yao. Isiwe kama yule nyoka dumilakosi ana vichwa viwili unamkata anakwenda huko na huku unadhani umepunguza matatizo, umesababisha nyoka wawili, utapata kazi mbili. Kwanza, kulisha nyoka wawili, ya pili kutibu majeraha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umri huu siyo wa kumbikumbi, ni umri ambao unafaa kwa hiyo, tambeni juu, lakini kumbikumbi amepewa mbawa mbili, huruka na baadaye hukatika na kurudi juu bila kutambaa. Kwa hiyo, umri huu ni mwisho wa matumaini tu wala msiwe na tahadhari. Bunge sasa hivi kwa sababu tunawapitishieni miaka minne, litakuwa karibu na ninyi sambamba, yaani tutabanana ili kuona kwamba Mashirika yaliyobakia hayauzwi katika *full price 'FULL'* na *fool prise 'FOOL'* na *book pry-value* na bei poa, kama mfano wa Mashirika ambayo yalitokea. Kwa hiyo, tumeona kwamba mtafuatilia hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa *commissioners*, kwa mfano ni lazima mshirikishe watu wa *PPF* na *NSSF* ili wakati Shirika linabinafsishwa, basi mafao ya Wafanyakazi isiwe kitendawili, kwa sababu mtakuwa mmeshayamaliza yote mambo ya mafao. Kwa hiyo, mnapobinafsisha hakuna wanaomanga manga.

Watu wa *PPF* au *NSSF* waitwe kushiriki katika Mashirika yanayobinafsishwa kama mlivyofanya kutuita watu wa *TFCA* nilipokuwa *Board Member* na Mheshimiwa Mhellukindo alikuwa Mwenyekiti wangu, mlituita na tukashirikiana kuzungumza masuala yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, pamoja na kwamba kuna kesi karibu zaidi ya 100, pale ambapo Serikali inashtakiwa kwa ajili ya mafao, basi *PSRC* isiwe upande wowote, ieleze ukweli bayana ili kuweza kutetea Taifa, kumuweka Mungu mbele, umma kati na ubabe nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, *PSRC* wenyewe baada ya Muswada huu kupita, kuwepo na *management retreat.* Kuna *section* ikipigwa lazima *section* ile mnasema *re-organise,* vita imekuja tumepigwa, kwa hiyo, kutoka kulia namba, mnahesabu moja, mbili, tatu, nne mwisho tano. Baadaye mnasema tulikuwa

kumi, kwa nini tumebaki watano, watano wamepungua. Kwa hiyo, *section* inarudi nyuma, itakuja nyingine. Hiyo inaitwa *management retreat.*

Kwa hiyo, kuna watu pale mmewaona wabovu, ninyi wenyewe *PSRC* siyo sisi. Kama wabovu basi anzeni ku-*prune out* ili warudi kwenye maeneo mengine waende wakasaidie Taifa, *PSRC* iwe *PSRC* nyingine ya awamu nyingine inayokuja. Kama hamuwezi hilo basi nitaweza kupeleka mapendezo kwa Waziri ili kuweza kupata timu iliyo nzuri, kwa sababu hata unapocheza mpira kama kombe liko uwanjani lengo ni kufunga magoli. Wakicheza dakika 90 ikiwa hamna goli wataongeza dakika 30, kama hawakufunga ni lazima ipigwe *penalty*, ndiyo utaratibu tunaoufanya. *PSRC* mlikuwa hamjafunga goli kombe lipo uwanjani, tuliza *ball* kiwanja ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Kwanza, naomba nimtambue Mheshimiwa Musa A. Lupatu, ambaye amechangia kwa maandishi. Lakini vile vile, niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza nao ni Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi na Mheshimiwa Semindu K. Pawa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio letu msingi wake ulikuwa ni kuomba Bunge hili Tukufu liridhie kuongeza muda wa *PSRC* na kutokana na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa, kama Serikali tunashukuru kwamba, Waheshimiwa Wabunge wameridhia hoja hiyo ili *PSRC* iendelee na kazi ya kuendeleza Sera ya Ubinafsishaji ambayo ni Sera ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima nikiri kwamba, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi tutayafuatilia kama tulivyozungumza jana na baadhi ya hoja zilizotolewa, kwa mfano kama hoja ya kuangalia muda wa *specification,* tumesema kwamba hiyo ni hoja inayokubalika, Serikali itaiangalia. Nilizungumza katika utangulizi wangu kabla sijatoa lile Azimio, masuala ya ufuatiliaji niliyazungumza kwamba, tutajaribu kufuatilia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nilielezea matatizo yanayojionyesha hususan tatizo la Wafanyakazi kwa maana ya mafao yao. Yako mafao ya kisheria na mafao ambayo yanatokana na mikataba ya hiari, kwa maana ya kwamba mikataba hiyo ya hiari ni baada ya Wafanyakazi na Menejimenti kutiliana mikataba hiyo na kupanga kugawana kitakachozidi kutokana na uzalishaji wa kiwanda husika. Vile vile, kuna suala la mkono wa dhahabu, (mkono wa heri), nao pia unatokana na jinsi kiwanda kilivyozalisha na nikasema kwamba, kiwanda ambacho kitakuwa kimefilisika, kiwanda ambacho kitakuwa hakijazalisha kwa faida, kwa hali yoyote ile mafao ya aina hiyo yatakuwa ni ya matatizo sana. Lakini napenda kusema kwamba, Serikali haijakaa kimya tu, Serikali inafanya

jitihada, inazungumza na Wafanyakazi, inazungumza na vyombo mbalimbali kuona kwamba ingawa haya yalitokana na uzembe ule wa nyuma wa Menejimenti kabla Mashirika haya hayajabinafsishwa, inaangalia taratibu mbalimbali za kupunguza matatizo yanayowakuta Wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida ya Kambi ya Upinzani na ndiyo maana Kambi hiyo, itachukua muda mrefu sana kuipiku CCM kwa sababu wao wanazungumza bila ya kutoa ufumbuzi wa matatizo. Wanazungumzia matatizo tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lwakatare alizungumzia suala la Kilimanjaro. Nilifikiiri Mheshimiwa Lwakatare atazungumza mafanikio makubwa yaliyopatikana kutoka Kiwanda cha Sukari cha Kagera, ambacho mwaka kesho kitazalisha karibu tani 30,000, nilifikiri hayo nayo atayazungumza. Lakini vile vile, nilifikiri atazungumza jitihada za Serikali za kuboresha Kiwanda cha Chai cha Maruku. Pia, nilifikiri atazungumza jitihada za Serikali za kuboresha utendaji wa Kiwanda cha *TANICA* Bukoba, tena Bukoba Mjini. Yote hayo hayaoni! Ninapenda kuwaambia Wananchi kwamba, Sera hizi za CCM wakishazielewa vizuri, wataelewa ukweli uko wapi. Ndiyo maana nimekuwa nikizunguka nikisema kwamba, kunatokea upotoshaji mkubwa sana wa Sera za Chama cha Mapinduzi ambazo zilileta mafanikio zinazoendeshwa na wale wenzetu Wanasiasa hasa wa Kambi ya Upinzani, lakini mwisho wananchi wataelewa ukweli. Kama zamani walikuwa wanapanga foleni kwa sababu ya kutafuta sukari na sasa wanakwenda dukani wanapata sukari, watajua CCM imefanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja hiyo, kwa sababu bado niko kwenye mchango wa Mheshimiwa Lwakatare, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, hoja aliyoitoa kubadilisha Azimio langu itakuwa ni ngumu sana, kwa sababu hoja zile zitaweza kupishana na utaratibu uliowekwa na kama nilivyosema katika Azimio langu, baadhi ya taratibu za kutayarisha mikataba hii kwa kweli ni za Kimataifa. Sasa haiwezekani dakika mbili tu nikaingiza vipengele vile, hivyo kukiuka baadhi ya masharti yanayofuatwa, siyo kwa Tanzania tu, lakini kwa dunia nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa William Shellukindo, kazi za *Action Plan* tutapanga na ufuatiliaji wake. Sisi tunaosimamia utendaji wa *PSRC* kwa kweli hatufurahii hata kidogo kuona kwamba, viwanda vile ambavyo vinabinafsishwa havichangii kwenye uchumi wetu. Sisi tunachotaka ni uchumi wetu kama Tanzania uweze kukua, tuweze kusimamia majukumu mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishasema, hadi sasa kutokana na Sera zetu za Urekebishaji Uchumi, Tanzania sasa ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki katika kukuza uchumi wake. Lakini vile vile, Tanzania ni nchi ya tatu katika nchi za *SADC* na wengine wanasema katika Afrika katika kukuza uchumi wake. Sasa, mafanikio haya tusifikiri ni mafanikio madogo, inabidi sisi wenyewe Watanzania tujipongeze kwa kazi kubwa tuliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba sheria iliyounda Tume iwekwe vyema kati ya Tume na Wizara, kwa maana ya Wizara zikazane na ufuatiliaji na Tume zikazane na ufuatiliaji wa mikataba, hilo tumelipokea.

Mheshimiwa Mwanri, napenda nikuhakikishie kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itahakikisha kwamba, wakati ubinafsishaji huu unafanyika, wale Wananchi ambao wanaishi kwenye *squatters* watapewa maeneo kwanza ili wawe na maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami amesema Serikali tuangalie utaratibu wa kuona tunawasaidiaje hawa ambao wanakosa mafao yao kwa sababu ya Mashirika yale kutokupeleka pensheni zao kwenye vyombo husika. Hilo ni suala ambalo Serikali inalifuatilia kwa makini na kama utakavyojua hata kwenye taarifa yetu tumeripoti kwamba *PPF* peke yake inadai karibu Shilingi bilioni 18 ya mafao ambayo hayakuwasilishwa, lakini Serikali inalifuatilia hili kwa karibu sana. Hatutarajii kabisa Tanzania ikawa ni Zimbabwe nyingine kwa sababu hilo siyo lengo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kama nilivyosema, ubinafsishaji wa maeneo haya utafanywa kwa utaratibu mzuri tu.

Mheshimiwa Ismail Iwvatta, tunakushukuru umeunga mkono Azimio hili na tumesikia kauli yako kwamba katika ubinafsishaji wa reli maeneo mengine tuangalie hasa ya ardhi kama yataweza kusaidia miundombinu ya baadhi ya Halmashauri katika maeneo yako. Nakubaliana na wewe pia kwamba, tutaangalia suala la *Kilimanjaro Machine Tools* kama kweli Wafanyakazi wale wanafanya kazi vizuri. Lakini vile vile, tuna tabu ya kupata mwekezaji na kama wale wanaendelea vizuri, utaratibu wa *MEBO* upo umepangwa, ni njia moja ya ubinafsishaji. Kwa hiyo, tunaweza kuangalia tukaona tunakibinafsishaje kiwanda kile. Tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Shekiffu.

Mheshimiwa Mutungirehi yeye ameendelea na kupiga kelele tu. Ndiyo, ameendelea na kupiga kelele kwamba, kuna mchezo mchafu, Serikali inabinafsisha nini, kunatokea nini. Sasa, binafsi sikuelewa hasa kwa kweli anazungumza nini, lakini nadhani ni kelele tu. Nafurahi alisema kwamba yeye hapingi ubinafishaji. *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, enhee, Kanuni.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Namba 52.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni gani?

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Namba 51.

**NAIBU SPIKA:** 51 ipi? Mheshimiwa Waziri, endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa Vyama vingi vya Siasa, moja ya sifa nzuri ni kuvumiliana wakati tunapokosoana. Kwa hiyo, tuvumiliane sana, wote tunavumilia tu. Baada ya kusema hayo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, *PSRC* itafanya kazi kama ambavyo mmeshauri, tutahakikisha kwamba, *PSRC* inaleta taarifa zake na tuna hakika kwamba, katika maeneo yaliyojionyesha mapungufu tutayafanyia kazi kwa nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kurudia hili ambalo amelisema Mheshimiwa Waziri na ni vizuri tukavumiliana. Ningesema niingilie kati hotuba ya Mheshimiwa Mutungirehi, toka mwanzo na akarudie kusoma *Hansard,* inawezekana alikuwa na jazba. Aende akatazame *Hansard,* Bunge lisingenoga, lakini nilivumilia ili umalize.

*(Hapa Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi Alisimama)*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mutungirehi, naweza kuamua kukuondoa. Ninachosema ni kwamba, ndani ya kwa Bunge beti za namna hiyo ni za kawaida. Kuna maneno yaliyowekwa humu ndani ya kuudhi, lakini unapiga kelele na Mbunge anaweza kusema, nitaendelea kupiga kelele juu ya jambo hili. Ni kitu cha kawaida. Sasa, tuendelee. Mheshimiwa Waziri ametoa hoja tayari, lakini kwa sababu Mheshimiwa Mutungirehi ana hoja yake ya kubadilisha hoja hii ambayo imeletwa na Waziri, sasa nampa nafasi ili aiwasilishe hoja hiyo. Baada ya kuiwasilisha nitahoji kuhusu kukubalika kwa hayo yatakayoletwa na baada ya hoja hiyo ndipo sasa nitahoji hoja ya msingi ambayo imeletwa. Sasa nakupa nafasi Mheshimiwa Mutungirehi.

### Hoja ya Kuongeza Mabadiliko kwenye Azimio la Kuongeza Muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa uvumilivu wako uliouonyesha kati ya mimi na mwingine. Kwa kweli naomba radhi kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri, nilitaka tu kufanya mabadiliko kwa kutumia Kanuni ya Bunge Namba 47 kifungu kidogo cha kwanza, kifungu (a) na (c), ambacho kipo katika ukurasa wa tatu wa hoja yake, ukurasa wa pili pale anapomalizia na: "Tume iweze kukamilisha majukumu na kazi hizo." Sasa, ninapendekeza kwamba, tuongeze maneno: "Na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wa Tanzania kuhusu jinsi na namna mikataba ya kubinafsisha Mashirika ya Umma inavyozua utata na pengine kulisababishia Taifa hasara; na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge huwa hawaioni mikataba hiyo yenye utata na hasara kwa Taifa kabla ama baada ya kusainiwa."

Baada ya hapo nilikwenda kwenye kile kifungu ambacho sasa alikuwa anahitimisha anaposema: "Kwa hiyo basi, kwa mujibu wa kifungu namba 21 kifungu kidogo cha 3 cha sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992, kama ilivyofanyiwa mabadiliko ambacho kinalipa Bunge madaraka ya kupokea taarifa na kupitisha Azimio la Kuongeza Muda wa Tume, Bunge hili katika Mkutano wake wa 13 linaazimia kuwa muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma uongezwe kwa kipindi kingine cha miaka minne kuanzia tarehe 1 Januari, 2004." Sasa, nilitaka ile nukta pale iondoke tuweke maneno: "Na Tume kupitia Serikali iwe inawasilisha Bungeni, Mikataba ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma yote yaliyobaki kabla ya makubaliano ya mwisho na Mwekezaji." Ndiyo nilitaka tuweke hayo. Sasa, hata kama ikikataliwa siyo hoja, mimi kazi yangu nimeitimiza. Ninaliomba Bunge likubali. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitatoa nafasi kwa upande wa Serikali kuhusu hoja hii ya kufanya mabadiliko. Upande wa Serikali mnasemaje, mnaikubali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya jumla, hoja hii kama Serikali, tunaikataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zake ni kwamba, kama utakumbuka vizuri wakati fulani katika Bunge lako hili Tukufu liliulizwa swali hili kwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Utaratibu wa Kuleta Mikataba mbele ya Bunge, tukasema kwamba, utaratibu huo kwanza ni lazima ufanyiwe kazi, lakini vile vile tutakinzana na utaratibu ambao hatuutumii sisi Tanzania tu, lakini hata katika taratibu za Kimataifa kwamba wawekezaji wawili au watatu wanaowania kupata kiwanda au Shirika, *Investment Plan* na *Business Plan* zao ziwekwe wazi kwenye mazingira ya ushindani, hilo linakuwa ni tatizo kidogo. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kwa kweli hoja hiyo hatuikubali sisi kama Serikali. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayotaka kuleta marekebisho tunaikataa kwa misingi hasa ya kwamba, kuna mgawanyiko wa shughuli kati ya Bunge na Serikali. Kazi ya kuangalia shughuli hizi za utendaji ni ya Serikali na Waheshimiwa Wabunge wanayo nafasi ya kuiuliza Serikali. Katika mambo haya ya mikataba ukishaingiza Bunge ndani ya mikataba likiharibika jambo hivi nani atamwuliza nani?

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo tunadhani kazi hii iachiwe Serikali na ni kazi ya kitaalam, wanafanya Wataalam kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wale wanaohusika na eneo lile linalohusika. Kazi hiyo inafanywa na Serikali, kama kuna tatizo ndiyo kazi ya Bunge sasa kuihoji Serikali. Ukianza kuingiza Bunge katika jambo hilo hata Wananchi watapata matatizo sana, kwa sababu hawawezi kuwauliza Wabunge wao juu ya mambo fulani ya utendaji wa Serikali kwa kuwa na Bunge nalo limo ndani. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge mkubaliane na Serikali. Hoja hiyo tuikatae wala haiendani na utaratibu wetu wa Kikatiba wa mgawanyo wa madaraka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji juu ya hii hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Mutungirehi, kwamba mabadiliko yafanyike kwenye hoja ya msingi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Kuongeza Mabadiliko kwenye Azimio la Kuongeza Muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilikataliwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni. Kwa hiyo, sasa tunarudi kwenye hoja ya awali ambayo haina mabadiliko. Sasa muiamue hoja hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kufanya Mabadiliko kwenye Azimio la Kuongeza Muda wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani kwa kadri nilivyoambiwa na Viongozi wa Serikali, tumemaliza shughuli za leo, lakini kwa sababu kuna mwenzetu ambaye ana hoja ya kuahirisha Bunge, sasa nampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa William V. Lukuvi, ili atoe Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**HOJA BINAFSI ZA WABUNGE**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maelezo ya kumtaka Waziri wa Nishati na Madini atoe tamko la ufafanuzi juu ya Kampuni ya *Kahama Mining Limited* kutumia maeneo ya Vijiji kwa shughuli za mgodi bila kuchukua tahadhari ya uharibifu wa mazingira. Maelezo haya yameandaliwa chini ya Kanuni ya 21(9) cha Kanuni za Bunge letu Tukufu, Toleo la mwaka 2003.

Kampuni ya *Kahama Mining Cooperation Limited* ilipewa *Special Mining Licence* Namba 44/99 yenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 51.48 kwa ajili ya kuchimba dhahabu katika eneo la Bulyanhulu Wilayani Kahama.

Kwa mujibu wa Sheria yetu ya Madini ya mwaka 1998, moja ya masharti ya msingi yaliyomo katika sheria hiyo na ikiwa ni pamoja na Mkataba husika ni lazima kwa kampuni yoyote inayofanya au inataka kufanya kazi ya uchimbaji madini, kufanya *Environmental Impact Assessment* kwa lengo la kuangalia athari zinazoweza kusababishwa na shughuli hizo kwa maisha ya binadamu na viumbe katika maeneo husika.Tuna uhakika, *KMCL* walifanya tathmini hiyo katika eneo walilopewa na kwamba wanaendelea kuhifadhi mazingira hata sasa wanapoendelea na zoezi zima la uchimbaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni hasa ya *Environment Impact Assessment* ni kuangalia namna ya kudhibiti kemikali, matetemeko yanayotokana na milipuko, mavumbi na mambo mengine yanayofanana na shughuli hiyo dhidi ya athari kwa maisha ya binadamu na viumbe vingine. Kama nilivyosema hapo awali, baada ya kampuni hiyo kupata leseni ilianza kuchimba madini hayo ndani ya eneo la leseni yao, yaani leseni namba 44/99 ya mwaka 1999.

Kutokana na sababu zinazodaiwa kuwa za kiteknolojia, kampuni baada ya kuanza kuchimba dhahabu ilianza *process* ya usindikaji wa dhahabu kwa kusafirisha udongo kwa kutumia malori makubwa yanayofanana na mitambo kupitia katika barabara ya Busoka Bulyanhulu kuelekea kwenye Bandari ya Isaka kupitia kwenye Vijiji vya Kakola, Bugalama, Ilogi, Lunguya, Shilela, Segese, Masabi, Izengwabahala, Ntobo, Kalagwa, Nyambula, Busoko na Manzese kuelekea nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwa wananchi wapatao takribani 100,000 hivi wanaoishi katika vijiji nilivyovitaja hapo juu, kwa umbali wa km 76 kutoka mgodini kuathirika sana kwa kiasi kikubwa sana cha mawingu mazito ya vumbi yanayosababishwa na misafara mirefu ya malori au mitambo hiyo, inayobeba udongo kuelekea nje ya nchi, lakini pia kitendo hicho ni mwendelezo wa zoezi zima la uchimbaji madini nje ya eneo lao la leseni kwa sababu usafirishaji huo wa udongo unakuwa ni *process* ya usindikaji wa madini nje ya maeneo waliyopewa na maeneo hayo yanakuwa kama *conveyer belt* ndani ya zoezi la uchimbaji madini hayo na kwa hiyo kufanya kazi nje kabisa ya eneo walilopewa na Serikali kwa ajili ya shughuli hiyo. Kuna ukweli usiopingika kwamba, wananchi wanaokaa katika vijiji hivyo wameathirika kwa kiasi kikubwa sana kutokana na zoezi hilo kiafya na kisaikolojia. Mpaka sasa zipo kesi nyingi zinazoendelea kuripotiwa katika zahanati na vituo vya afya za maradhi ya *TB,* vikohozi, macho na kadhalika na inaaminika kwamba, ni matokeo ya mavumbi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vumbi hilo lisingekuwa na madhara yoyote kiafya kama inavyodaiwa na wachache wasiotutakia mema, hapana shaka kwamba hata wao kwenye makao yao ya mgodi wasingevaa vifaa vya kujikinga na mavumbi kama vile *noise masks, eye goggles, helmet* nakadhalika. Lakini vile vile humwagilia maji kila siku katika maeneo wanayoishi ili kuzuia kabisa vumbi linalosababishwa na mitambo yao.

Waheshimiwa Wabunge, waliopata fursa ya kutembelea mgodi huo hivi karibuni, bila shaka walijionea jinsi linavyodhibitiwa vikali vumbi katika maeneo ya mgodi. Wakazi wa maeneo niliyoyataja ikiwa ni pamoja na wana mazingira, tunaamini kuwa, vumbi hilo lina athari kubwa kwa afya za binadamu, wanyama na hata mimea yetu. Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa ninataka maelezo ya kina kabisa ya ufafanuzi toka Serikalini kwa mambo matatu yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa wananchi waishio katika vijiji nilivyovitaja wanaendelea kuathirika na zoezi hilo na hakuna utaratibu wowote wa kuondoa kero hiyo au kuipunguza; je, Serikali inakubaliana na hali hiyo na hadi lini? Madhara ya kiafya yanayoendelea kupatikana yatafidiwa na nani?

(ii) Kwa kuwa imeonekana wazi kuwa kampuni hiyo inatumia maeneo hayo bila hata kufanya *Environment Impact Assessment* kama sheria za nchi zinavyoelekeza, je, Serikali yetu inayoaminika kwa utawala wa sheria itaendelea hadi lini kuwaacha watu hawa wakivunja sheria zetu? Je Serikali iko tayari kutoa tamko la kuizuia kampuni hiyo isitumie kwa shughuli za mgodi barabara inayopita katika vijiji hivi nilivyovitaja na kwamba barabara hiyo ibaki kwa matumizi ya magari ya kawaida? *(Makofi)*

(iii) Kama kampuni hiyo imepewa au imeongezewa eneo na kwamba eneo lao sasa ni pamoja na vijiji nilivyovitaja hapo juu, Serikali inaweza kuliarifu Bunge hili na wananchi kwa ujumla na kwamba kampuni hiyo itakiwe sasa kuiwekea lami barabara hiyo, ili kuwaondolea kero wananchi wanaokaa katika vijiji hivyo, ili angalau kuwapunguzia wananchi kero kubwa yenye kuhatarisha afya na maisha yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maelezo yangu haya, naomba nikushukuru wewe tena na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge ametaka maelezo ya kina kabisa sasa sijui kama Waziri anayo ya kina kabisa kwa sasa hivi lakini pengine anayo. Upande wa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba kwanza, tumepokea maelezo ya Mheshimiwa Emmanuel Kipole na kama ambavyo umesema anahitaji maelezo ya kina kabisa, tunaomba atupe nafasi tukafanyie kazi maelezo haya ili tuje kutoa kauli hapa Bungeni wakati muafaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji hoja ya kuahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.39 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 14 Novemba, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*